# Nipashe

Jumatano Aprili 3, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579882

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Habari njema ya tiba ya saratani bila kukatwa titi

UKURASA 4




UKURASA 13

# Ajira ya CAG Assad yawekwa mtegoni



Prof. Mussa Assad    Job Ndugai

**NI** baada ya Bunge kususa kufanya naye kazi...


*Endelea ukurasa wa 2*






## Halima Mdee matatani tena, amponza Lema





UKURASA 2

## RAIS MAGUFULI AWATANGAZIA KIAMA WAONGO MALIPO KOROSHO

UKURASA 2

HABARI SIMBA YAWAZA POINTI 3 BARA UK. 32 | MAONI, KATUNI UK.6

# Ajira CAG Assad yawekwa mtegoni

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

AJIRA ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, iko shakani kutokana na Bunge kuazimia kutofanyakazi naye.

Bunge lilipitisha azimio hilo bungeni jijini Dodoma jana, baada ya Kamati yake ya Kudumu ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuwasilisha taarifa kuhusu shauri dhidi ya Prof. Assad aliyefikishwa mbele yake mwanzoni mwa mwaka akikabiliwa na tuhuma za kudharau, kudhalilisha na kushusha heshima na hadhi ya chombo hicho cha kutunga sheria.

Kutokana na uamuzi huo, hatima ya ajira ya Prof. Assad sasa iko mikononi mwa Rais John Magufuli kwa kuwa tayari kumeibuka utata wa namna Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ambayo CAG ni bosi wake, itakavyotekeleza majukumu yake bila kulishirikisha Bunge.

Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, inamtaka CAG kuwasilisha kwa Rais kila taarifa atakayotoa.

Kwa mujibu wa ibara hiyo, baada ya kupokea taarifa hiyo, Rais atawaagiza watu wanaohusika wawasilishe taarifa hiyo kwenye mkutano wa kwanza wa Bunge utakaofanyika baada ya Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika mkutano huo kabla ya kupita siku saba tangu siku ulipoanza.

**MASHARTI KUMFUKUZA KAZI CAG**

Ibara ya 144(1) ya Katiba hiyo inaeleza kuwa bila ya kuathiri masharti mengine yaliyomo katika ibara hiyo, CAG atalazimika kuacha kazi yake atakapotimiza umri wa miaka 60 au umri mwingine wowote utakaotajwa na sheria iliyotungwa na Bunge.

Ibara ya 144 (2) ya Katiba inaeleza kuwa CAG aweza tu kuondolewa katika madaraka ya kazi yake kwa sababu ya kushindwa kutekeleza kazi zake (ama kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote) au kwa sababu ya tabia mbaya, au kwa kuvunja masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Ibara ya 144 (3) ya Katiba hiyo inaeleza kuwa iwapo Rais anaona kwamba suala la kumwondoa kazini CAG kwa mujibu wa masharti ya ibara hii lahitaji kuchunguzwa, basi katika hali hiyo mambo yatakuwa ifuatavyo:

(a) Rais atateua tume maalum ambayo itakuwa na mwenyekiti na wajumbe wengine wasiopungua wawili. Huyo mwenyekiti na angalau nusu ya wajumbe wengine wa tume hiyo itabidi wawe watu ambao ni majaji au watu waliopata kuwa majaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani katika nchi yoyote iliyomo kwenye Jumuiya ya Madola.

(b) Tume hiyo itachunguza shauri lote halafu itatoa taarifa kwa Rais kuhusu maelezo ya shauri lote na itamshauri Rais kama huyo CAG aondolewe kazini kwa mujibu wa masharti ya ibara hii kwa sababu ya kushindwa kufanya kazi kutokana na maradhi au sababu nyingine yoy-

INAENDELEA UK 8

## Mdee asimamishwa tena, amponza Lema

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MBUNGE wa Kawe, Halima Mdee (Chadema), amefungiwa kuhudhuria mikutano miwili ya Bunge kuanzia jana kutokana na kuunga mkono kauli ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, kwamba chombo hicho cha kutunga sheria ni dhaifu.

Vilevile, Mbunge wa Arusha Mjini, Godbless Lema (Chadema), ametakiwa kufika mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhojiwa kutokana na kuunga mkono kauli hiyo iliyotafsiriwa kuwa inalenga kulidhalilisha Bunge.

Bunge lilitumia dakika 42 kuanzia saa 5:19 asubuhi kusikiliza uwasilishaji wa namna shauri hilo lilivyoendeshwa na kamati hiyo na kujadili mapendekezo ya kamati.

Akiwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, kuhusu shauri hilo, Mwenyekiti wa kamati hiyo, Emmanuel Mwakasaka, alisema Mdee alifika mbele ya kamati Januari 22 kwa mujibu wa hati ya wito aliyopewa.

Alisema Mdee alikuwa anakabiliwa na tuhuma za kulidharau na kulidhalilisha Bunge kutokana na kauli yake ya Januari 2, mwaka huu aliponukuliwa na kusikika kwenye mitandao ya jamii akipongeza kauli za Prof. Assad kuhusu "udhaifu wa Bunge".

Mwakasaka alinukuu kauli ya Mdee akisema: "Kitendo cha CAG kusema kwamba hali si nzuri halafu chombo kinachotakiwa kusimamia haki hakifanyi hivyo, ni cha kijasiri na nina imani wanaoongoza huo mhimili watakuwa wavumilivu. Hawatafikiria kumwita kwenye Kamati ya Maadili kwa sababu tumeitwa dhaifu, kwa sababu kweli ni dhaifu...

INAENDELEA UK 7



Rais Dk. John Pombe Magufuli akiwa na mkewe Mama Janeth Magufuli, Mbunge wa Mtwara Vijijini, Hawa Ghasia pamoja na viongozi mbalimbali wa mkoa wa Mtwara wakivuta utepe kuashiria uwekaji wa jiwe la msingi la mradi wa upanuzi wa uwanja wa ndege wa Mtwara jana. **PICHA: IKULU**

# Magufuli awatangazia kiama wapotoshaji malipo korosho

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli amemkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, boksi lenye orodha ya majina ya watu waliolipwa fedha zao za korosho na kuwataka wale watakojitokeza na kudanyanya kwamba hawajalipwa wakati wapo kwenye orodha hiyo, wawekwe ndani.

Rais Magufuli alitoa kauli hiyo jana mkoani Mtwara wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi wa upanuzi wa uwanja wa ndege mkoani humo, ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba mwakani na ujenzi wake unagharimu Sh. 50.366.

Akizungumza kwenye sherehe hizo akiwa katika ziara yake ya siku tatu, Rais Magufuli alisema serikali imeshalipa watu waliokuwa na korosho chini ya kilo 1,500.

"Nataka niwaambie orodha yao ninayo, leta lile limfuko langu hapa, weka hapo vitabu vyote, nataka niwaambie kila aliyelipwa orodha ninayo, kila wilaya, kila mkoa, kila kijiji na jina na akaunti na fedha aliyolipwa," alisema Rais Magufuli na kuongeza:

"Majina yote ya wale waliolipwa haya hapa, ninamuachia Mkuu wa Mkoa ili mshirikiane na Wakuu wa Wilaya kuhakiki wale waliokwishalipwa awali.

"Kukata mzizi wa fitina nimekuja na boksi lenye orodha ya majina ya watu waliolipwa fedha zao za korosho zilizokuwa chini ya kilo 1,500."

Rais Magufuli alimuagiza Mkuu wa Mkoa akawaumbue wale wote wanaosema hawajalipwa, wakati wameshapewa fedha zao.

"Akisema hajalipwa na kwenye orodha yupo mshike mpeleke ndani, pia kuna wale waliokuwa na kilo zaidi ya 1,500 uchambuzi yakinifu ulikuwa unafanyika, ya kwanza ni wale waliokuwa chini ya kilo 1,500 na uchambuzi ulioendelea sasa hivi na umekamilika ni wa kilo 1,500 au zaidi, hao walikuwa 18, 103 ambao wamepatikana na hawajalipwa," alisema.

Alisema wenye kilo zaidi ya 1,500 waliolipwa ni wachache ambao uchambuzi wake umekamilika na kwamba serikali isingeweza kutoa fedha bila kufanya uchambuzi.

"Humo yamepatikana majina 780 ya ambao hawana mashamba wala mkorosho, lakini walikuwa wanadai nao walikuwa na kilo zaidi ya 1,500, hawa wenye majina 18,103 Waziri wa Kilimo yupo hapa, Waziri wa Biashara yupo hapa.

"Nimeshatoa maagizo wakati ninatoka Dar es Salaam ziletwe Sh. bilioni 50 kuanzia kesho au keshokutwa hawa nao waanze kulipwa, na zikiisha tutaleta nyingine,yule mkulima ambaye ana korosho zake ameuza na ni halali siyo za kughushi nawahakikisha wote watalipwa," alisema.

Rais Magufuli alisema katika hilo wapo waliokuwa wakinunua korosho zikiwa shambani, wengine walinunua maua kwamba yakichanua ni yao.

"Kukiri ni kitu kizuri sana, sasa wale watakaokiri kwamba walikuwa makangomba walinunua korosho na serikali ilizichukua muwaangalie nao walipwe," alisema.

Rais Magufuli alisema anafahamu waliofanya biashara hiyo ni wengi akiwamo Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mtwara.

"Nikawa namwangalia tu nasema wewe Mwenyekiti wewe ninafahamu kufanya kosa siyo kosa ila kurudia kosa ndiyo kosa, wapo watu waliku-

INAENDELEA UK 8

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

02-04- 2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatano Tarehe 3/4/2019 kampuni ya **EFFCO SOLUTION LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwakutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea NAIROBI, gari hilo lenye namba za usajili:

**T116DCG/T901 CZT**

2. **Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:**

| | | |
|---|---|---|
| Urefu | - mita | 19.50 |
| Upana | - mita | 2.70 |
| Kimo | - mita | 4.60 |

3. Njia itakayotumika **DAR ES SALAAM mpaka NAIROBI Kupitia MOSHI,** gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

11515302

# Mbowe: Adhabu ya CAG ilipangwa kabla ya azimio

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

KIONGOZI wa Kambi Rasmi Bungeni, Freeman Mbowe, amedai uamuzi kuhusu Bunge kutofanya kazi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, ulikuwa umefanyika hata kabla ya kamati husika ya Bunge kupendekeza chombo hicho kitoke na azimio hilo.

Jana, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge iliwasilisha bungeni jijini Dodoma shauri dhidi ya CAG Assad na kupendekeza Bunge kutofanya kazi na mtaalamu huyo wa ukaguzi aliyekuwa anakabiliwa na tuhuma za kulidharau na kulidhalilisha Bunge kutokana na kauli yake ya mwanzoni mwa mwaka kuhusu kile alichodai "udhaifu wa Bunge".

Akichangia hoja ya kamati hiyo, Mbowe alisema inaonyesha wazi kwamba azimio hilo lilikuwa limeshafanyiwa uamuzi na kuamua kutumia vifungu vya katiba kutoa ushauri kwa Bunge hata kabla ya wabunge kuamua adhabu dhidi ya Prof. Assad.

"Kwa kuwa azimio hili limeshafanyiwa maamuzi, sitaongea mengi, nitaongea kwa kifupi sana, historia ambayo mnaiandika leo (jana), Bunge mnalipa upungufu.

"Mnataka kuwaziba Watanzania midomo, watu wasiseme wakati sisi hapa bungeni tunafanya maamuzi kwa niaba ya Watanzania, mnataka tudhulumu haki za msingi za watu kwa sababu tuna mamlaka ya kufanya hivyo.

"Ibara ya 18 ya Katiba ya nchi inasema 'kila mtu ana uhuru wa kuwa na maoni, anayo haki ya kutafuta kupokea na kutoa habari bila ya kujali mipaka ya nchi, anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake.

"Katiba ni sheria mama, Sheria ya Kamati ya Bunge haiwezi kuvunja sheria mama, kifungu kilichomtia hatiani Prof. Assad, kinavunja Katiba ya nchi," Mbowe alisema.

Mwenyekiti huyo wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), pia alilishauri Bunge kuangalia upya muundo wa kamati zake, akieleza kuwa kamati iliyomtia hatiani Prof. Assad haiwezi kutenda haki dhidi ya vyama vya upinzani na watu wanaoonekana kwenda kinyume cha mtazamo wa serikali.

"Na katika siku za usoni, mnapounda kamati ya maadili, kama tuna nia njema na nchi yetu, muangalie 'composition' (muundo) ya kamati za maadili, kwa sababu 'composition' ya kamati ya maadili leo haiwezi ikafanya 'justice' kwa vyama vya upinzani au kwa watu wanaoonekana pengine wanaikwaza serikali," Mbowe alisema.

Alilishauri Bunge, Spika na wabunge wote kusimamia vizuri na kwa haki ili uangaliwe uwezekano wa kufanya usawa katika kamati.

Mbowe alisema kuendelea kuweka wajumbe wengi kwenye kamati hiyo kutoka CCM, kutatoa mtazamo kwa umma kuwa Kamati ya Maadili ni kamati ya chama na uamuzi unafanyika nje ya Bunge kwa kuwa watu wanakuwa wanafuata maelekezo waliyopewa.

## Anayeshtakiwa mauaji aomba mahakama kumwandikia Rais Magufuli

**Na Hellen Mwango**

PRAIVETI Ramadhani Mlaku (28) wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), ameiomba mahakama kumruhusu kuandika barua ya wazi kwa Rais Dk. John Magufuli kupitia vyombo vya habari kwamba siku ya tukio alipigwa risasi mbili na kujeruhiwa.

Mlaku anayekabiliwa na shtaka la mauaji ya askari mwenzake, ametoa malalamiko hayo juzi kwamba pamoja na kushtakiwa na kuendelea kukaa mahabusu, lakini hafahamu hatima ya aliyempiga risasi na kumjeruhi ikiwezekana apewe dhamana.

Mshtakiwa alitoa malalamiko hayo mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Kevini Mhina, kesi yake ilipopangwa kwa ajili ya kutajwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Wakili wa Serikali Patrick Mwita, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kwamba jalada linaandaliwa kwenda kwa Mkuu wa Upelelezi (RCO), Mkoa wa Kipolisi Ilala kwa maandalizi ya mwisho.

Hata hivyo, mshtakiwa aliomba ruhusa kwa hakimu ya kutoa malalamiko yake.

"Mheshimiwa hakimu mimi ninaandaa barua ya wazi kwa Mheshimiwa Rais Magufuli kupitia vyombo vya habari kuhusu suala la kujeruhiwa kwangu," alidai na kuongeza:

"Mimi hapa nilipo nilishambuliwa kwa kupigwa risasi mbili na mpaka sasa sijui nani alinipiga risasi hizo, nataka kesi hii iishe nitoke nikajue nani mhusika au la naomba dhamana nikafuatilia haki yangu," Mlaku alidai.

Hakimu alisema kwa bahati mbaya kesi inayomkabili ni ya mauaji haina dhamana.

"Kesi inayokukabili haina dhamana wasiliana na Mkuu wa Gereza ambalo uko mahabusu atakusikiliza kuhusu malalamiko yako na malengo yako," alisema Hakimu Mhina.

Alisema kesi hiyo itatajwa tena Aprili 12, mwaka huu.

Machi 14, 2018 Mlaku alifikishwa katika mahakama hiyo kwa mara ya kwanza akiwa chini ya ulinzi wa Jeshi la Polisi (MP) na askari polisi akiwa amebebwa juu ya kitanda cha wagonjwa (machela).



Vijana wakishusha shehena ya miwa kutoka kwenye lori kwa ajili ya kuuzwa katika Soko la Tandale, Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

## Korti yatupa maombi wanachama wa DECI

**Na Hellen Mwango**

MATUMAINI ya wanachama 18 wa Kampuni ya Development Entrepreneurship for Community Initiative (DECI), kuvuna mabilioni ya fedha yametoweka baada ya maombi yao kwa Mahakama Kuu, Kanda ya Dar es Salaam kutupiliwa mbali kutokana na kuwa na upungufu wa kisheria.

Uamuzi huo ulitolewa jana na Jaji Stephan Magoiga, baada ya kusikiliza hoja za walalamikaji 18 akiwamo Andrew Tungaraza na wenzake 17 dhidi ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), Waendesha Mashtaka wa Serikali, Jackson Mtales, Domonick Kigendi, Timotheo Loitig'nye na Samwel Mtares.

Alisema mahakama baada ya kupitia hoja za walalamikaji na walalamikiwa, inatupilia mbali maombi hayo baada ya kubainika kwamba hayakuwa yameandikwa tarehe.

"Nayaondoa maombi haya baada ya kuonekana yana upungufu ya kisheria chini ya kifungu cha 8 sura ya 12 cha Sheria ya Makam

INAENDELEA UK 26


**REQUIREMENT OF WAREHOUSE**

We urgently require spacious warehouse for immediately long term lease with below specifications

**Capacity –** 3000 to 5000 square meters
**Location –** Along Nyerere/Pugu Road and/or Chang'ombe
**Accessibility –** Should be accessible by road throughout the year
**Entrance –** Entrance to containerized cargo is a must for both 20 & 40 feet containers 24/7

**Space –** Should have sufficient space to carry out both offloading from containers and loading customer's vehicles simultaneously

**Ownership –** The owner should possess sufficient and credible evidence regarding title, registration and other statutory requirements Middlemen not entertained

Interested parties to call
+255 784 /620 305 085; +255 713 254 912
Or send email to info@diy.co.tz

115146302



**KUMBUKUMBU**



Ni miaka ishirini (20)imepita tangu ulipotutoka baba yetu mpendwa **AARON ESLI MUNHAMBO.** Unakumbukwa na mke wako mpendwa MARGARET HELLINA, watoto wako FAITH, DOROTHY, GLORIA, EMMANUEL NA GRACE. Dada yako LOI, Mdogo wako NUHU shemeji yako GERSHON MGWENO, wakwe zako PROf. GODWILL MREMA, RUBEN MWEGOHA, MOSES LUKUMAY na wajukuu zako.

**Tuendeleza daima Upendo aliotuachia Baba yetu .**

**Zaburi 133:1- TAZAMA JINSI ILIVYO VEMA NA KUMPENDEZA, NDUGU WAKAE PAMOJA KWA UMOJA**

115152802

# Wenye saratani ya matiti kupasuliwa bila kukatwa

**Na Beatrice Shayo**

TANZANIA kwa mara ya kwanza imeanza kufanya upasuaji wa kuondoa uvimbe kwa mgonjwa mwenye saratani ya titi bila kulikata.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), Profesa Lawrence Museru, alisema jana wakati akifungua mkutano wa wataalamu kutoka Kenya walioungana na wataalamu wa hospitali mbalimbali za Tanzania ili kujifunza njia mpya za tiba ya saratani ya matiti kwa upasuaji.

Alisema dunia nzima saratani ya matiti ndiyo inayoongoza kwa vifo vya wanawake ambao ni sawa na asilimia 25 hadi 35 ya saratani zote na kwamba saratani inayoongoza kuua wanawake ni ya matiti.

"Ingawa wagonjwa wengi wako katika nchi zilizoendelea, lakini vifo vingi vinatokea katika nchi zinazoendelea na hii ni kwa sababu sisi hatuna nyenzo za kugundua saratani mapema, lakini pia wapo wagonjwa wetu wanakuja wakiwa wamechelewa kufika hospitali kwa sababu mbalimbali ikiwamo kukosekana kwa huduma za afya na vifaa vya uchunguzi," alisema.

Profesa Museru alisema wagonjwa wengi wanafika hospitali wakiwa kwenye hatua ya tatu na ya nne ambayo ni mbaya zaidi.

"Ingawa duniani saratani inayoongoza kwa kuua wanawake ni ya matiti, lakini kwa hapa Tanzania inayoongoza kuua wanawake ni ya shingo ya kizazi," alisema na kuongeza:

"Asilimia 80 ya wagonjwa wote Tanzania wanakuja wakiwa wamechelewa hili ni tatizo, hivyo ni vizuri watu wakawa wanaangalia afya zao ili mtu akibainika atibiwe mapema."

Aidha, alisema wanachojifunza ni upasuaji kwa mgonjwa aliye katika hatua za kwanza.

Alisema katika siku mbili za mafunzo hayo watajifunza upasuaji upi unaweza kuondoa saratani ili usimpe mwanamke msongo wa mawazo kwa sababu ya kuondolewa titi.

Alisema wamekutana na wataalamu kutoka Kenya, Hospitali ya MNH, Bugando, KCMC, Mbeya Ocean Road na Mloganzila na watapeana uzoefu ili wataalamu wapate uwezo wa kutibu kwa njia mpya ya kisasa bila kuondoa titi.

Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila, Julieth Magandi, alisema saratani ya matiti bado ni tatizo kubwa katika hospitali ya MNH.

Alisema kwa takwimu za Julai mwaka 2012 hadi Juni 2013, wagonjwa 856 waliofanyiwa upasuaji asilimia 20 walikuwa ni wagonjwa wa saratani ya matiti, hivyo wadau na wataalamu wanatakiwa kuchukua hatua mapema na wananchi kupima afya zao kwa wakati.

Daktari wa upasuaji wa matiti katika hospitali ya MNH, Casper Haule, alisema wamefanya mkutano wa kwanza ambao wanajengeana uwezo kwa wataalamu katika kutoa huduma bora za kisasa za tiba ya saratani ya matiti.

Alisema katika mkutano huo, watafanya upasuaji kwa wagonjwa wanne wenye saratani ya matiti bila kuondoa ziwa.

"Huu ni upasuaji wa kwanza ambao tunaanza kuufanya katika hospitali yetu kwa wagonjwa ambao wamekuja wakiwa na dalili za mwanzo za saratani ya matiti," alisema.

Dk. Haule alisema upasuaji huo unatokana na upatikanaji wa tiba za kisasa za mionzi katika Hospitali ya Ocean Road.

Alisema mgonjwa akionekana na dalili za kwanza za saratani ya matiti walikuwa wanaondoa titi kwa sababu hawakuwa na mionzi ya kisasa. "Kilichokuwa kinatuzuia kufanya upasuaji ni upatikanaji wa mionzi ya kisasa hali ambayo ilisababisha hata kwa mgonjwa mwenye dalili za awali anakatwa matiti, hivyo kwa sasa hatutakata matiti kwa yule mwenye dalili za awali tutafanya upasuaji wa kuondoa uvimbe katika matiti," alisema.

Aidha, alisema saratani ya matiti inatibika endapo mtu atafika hospitali mapema na kubainika ana dalili za kwanza na kuwaasa wananchi kufika hospitali kucheki afya zao.

## Mabweni hosteli Magufuli bil. 10/-

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, amelihakikishia Bunge kuwa ujenzi wa mabweni ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam yajulikanayo kama hosteli za Dk. John Magufuli uligharimiwa na serikali kwa Sh. bilioni 10.

Ole Nasha aliliambia Bunge jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Susan Lyimo, aliyetaka kujua ni kiasi gani kilitumika kujenga mabweni hayo.

Akijibu swali hilo, Ole Nasha, alisema mradi wa ujenzi wa mabweni hayo ulianza rasmi Julai mosi, 2016 na mabweni hayo yalikamilika na kukabidhiwa rasmi Aprili 15, 2017. "Ujenzi huo ulifanywa na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), kama mkandarasi na kusimamiwa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa," alisema.

## LHRC yaja na mwarobaini kudhibiti uchaguzi mdogo

**Na Salome Kitomari**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu Tanzania (LHRC), kimesema bado ipo haja ya kufanya mabadiliko ya katiba ili kuondoa au kupunguza gharama za uchaguzi wa marudio.

Aidha, kimesema fedha zinazotumika kwenye uchaguzi huo zielekezwe kwenye shughuli za maendeleo kama ujenzi wa shule, miundombinu na kupeleka vifaa tiba na dawa kwenye hospitali, vituo vya afya na zahanati.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, alisema uchaguzi unagharimu fedha nyingi ambazo zingeelekezwa kwenye maendeleo zingesaidia kutatua matatizo ya jamii.

Nipashe iliuliza maoni ya LHRC kuhusiana na chaguzi ndogo unazofanyika nchini kwa sababu mbalimbali kwa lengo la kukidhi matakwa ya kikatiba.

Kauli ya Mkurugezi huyo imetolewa siku chache baada ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kutangaza uchaguzi mdogo wa jimbo la Arumeru utafanyika Mei 19, mwaka huu, baada ya mahakama kutoa uamuzi wa kuunga mkono uamuzi wa Spika kumsimamisha ubunge, Joshua Nassari, kutokana na utoro.

"Kwa kweli inatuuma sana kodi ya Watanzania maskini ambao wanaishi chini ya Dola moja, mwaka jana ilifika wakati kila mwezi kuna uchaguzi mdogo sehemu na unagharimu fedha nyingi," alisema.

Alisema amekuwa mwangalizi wa uchaguzi kwa muda mrefu na anaona gharama zinazotumika, lakini changamoto kubwa ni katiba haitoi jibu la moja kwa moja katika kushughulikia hilo.

"Haisemi kama atafariki anayefuata kwa kura awe mbunge, au akihama chama basi aahame na ubunge wake, lakini katiba imekaa kimya. Naona suluhisho la jambo hili ni kubadili katiba ili kupunguza gharama nyingi zinazoletwa na chaguzi ndogo za kila mara," alisema.

Kwa mujibu wa Henga, ilifanya tathmini mwaka jana na kubaini kuwa gharama za uchaguzi mmoja ni nyingi ambazo zingeelekezwa kwenye maendeleo zingefanya kazi kubwa.

"Kwa kweli fedha zinazotumika ni nyingi sana kama zingetumika kujenga shule tungejenga nyingi sana, kama ni kugawa madaftari kwa wanafunzi wengi wangepata, kama ni kujenga visima vya maji tungewaondoa watu kwenye shida ya magonjwa yatokanayo na maji," alisema.

"Ilifika mahali tukaona kila mwezi kuna uchaguzi, tukafanya tathmini tukaona gharama ni kubwa sana ambazo zingefanya maendeleo makubwa sana," alisema.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
Tarehe 29/03/2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Ijumaa tarehe 05/04/2019 kampuni ya S.S.F Co.LTD itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka DAR kuelekea KAGERA gari hilo lenye namba za usajili: T785 CAD/T 166 ADN.

**2.Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 21.80 |
| Upana | - | mita | 3.40 |
| Kimo | - | mita | 5.20 |

3.NJia itakayotumika DAR hadi **KAGERA kupitia MWENDAKULIMA gari litasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215154002



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
Tarehe 02/04/2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Ijumaa tarehe 05/04/2019 kampuni ya **S.S.F Co.LTD** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR kuelekea KAGERA** gari hilo lenye namba za usajili: **T776 CAD/T 243 DCT.**

2.Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 18.0m |
| Upana | - | mita | 3.0m |
| Kimo | - | mita | 5.20m |

3 .NJia itakayotumika **DAR hadi KAGERA kupitia MWENDAKULIMA gari litasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215153702

## HABARI KITAIFA

# Kesi mauaji ya mwanafunzi yaanza kunguruma

**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania, Kanda ya Moshi imeelezwa kuwa wataalamu wa Hospitali ya Rufani ya KCMC waliouchunguza mwili wa mwanafunzi wa kidato cha pili wa Sekondari ya Scolastica, Humphrey Makundi, hawakuweza kutumia kipimo cha Cabon 14 ili kubaini umri sahihi wa mwanafunzi huyo kwa sababu kipimo hicho kina gharama kubwa.

Kesi hiyo inayovuta hisia za wakazi wengi wa ndani na nje ya Mkoa wa Kilimanjaro, inamkabili mmiliki wa shule hiyo, Edward Shayo, mwalimu wa nidhamu Labani Nabiswa na mlinzi wa shule, Hamis Chacha.

Mwanafunzi huyo alitoweka shuleni Novemba 6, 2017 na baadaye kubainika ameuawa na watu wasiojulikana na mwili wake kukutwa Novemba 10, 2017 katika Mto Ghona mita 300 kutoka shuleni hapo.

Kesi hiyo inasikilizwa na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu, Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi Kanda ya Dar es Salaam, Firmin Matogolo.

Wakili Mwandamizi wa Serikali, Joseph Kande wakati anasoma maelezo kuhusu kesi hiyo namba 48 ya mwaka 2017, alidai kuwa upande wa mashtaka utawaita mahakamani mashahidi 34 kutoa ushahidi wao kuhusu shauri hilo na kwamba katika siku ya kwanza mahakama hiyo itasikiliza mashahidi wawili.

Mawakili wengine wa serikali wanaounda jopo la upande wa mashtaka ni Abdala Chavula, Omary Kibwana na Lucy Kyusa, huku upande wa utetezi ukiwa na jopo la Mawakili Elikunda Kipoko, David Shilatu, Gwakisa Sambo na Patrick Paul.

Mahakama hiyo ilianza kusikilisza shauri hilo kwa kusikiliza ushahidi wa shahidi wa kwanza wa upande wa mashtaka, Mkuu wa Kitengo cha Mophologist ambaye ni Daktari bingwa wa upasuaji katika Hospitali ya Rufani ya KCMC, Dk. Alex Mremi (36).

Alieleza mahakama kuwa mnamo tarehe 19/11/2017 majira ya saa tano asubuhi akiwa ofsini kwake akitekeleza majukumu yake, alipokea simu iliyomtaka kufika katika chumba cha kuhifadhia maiti, kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

"Nilijiandaa na kutoka ndani katika chumba hicho na hapo niliukuta mwili wa marehemu ambao ulikuwa katika hali ya kuharibika na wenye harufu kali, Inspekta wa Polisi ambaye alitambulika kwa jina la Agustino na Dk. Peter Mlungwa kutoka katika Hospitali ya Rufani ya Mawenzi."

**"Nilijiandaa na kutoka ndani katika chumba hicho na hapo niliukuta mwili wa marehemu ambao ulikuwa katika hali ya kuharibika na wenye harufu kali, Inspekta wa Polisi ambaye alitambulika kwa jina la Agustino na Dk. Peter Mlungwa kutoka katika Hospitali ya Rufani ya Mawenzi."**

Aliendelea kudai kuwa akiwa katika chumba cha upasuaji pamoja na Samwel Victor ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Meno wa Hospitali ya KCMC, walianza uchunguzi na kubaini kuwa marehemu alikuwa ni wa jinsia ya kiume, aliyevalia t-shit, bukta na soksi.

Kichwani kwake kulikuwa kumepigwa na kitu kizito katika paji la uso na kupasuka fuvu ja kichwa na jeraha hilo lilikuwa linaurefu sentimita sita kwa tano, michubuko katika maeneo ya mapaja, mabega, mgongoni na majeraha yote hayo aliyapata kabla ya kifo chake na upo uwezekano mkubwa wa jeraha kubwa kwenye pagi la uso ndicho chanzo cha kifo chake.

Alidai mahakamani kuwa mwili huo wa marehemu ulikuwa ni miaka 15-17 kutokana na magego yake yaliyokuwa yanaendelea kuota ambayo yalikuwa hayajatoka licha ya kuwapo kwa meno mengine yaliyokuwa tayari yametoka kutokana na mwili huo kuharibika.

"Pia tulilazimika kumpima vinasaba ili kubaini mwili ule ulikuwa una uhusiano na kina nani, ambapo tulichukua mifupa katika maeneo mbalimbali ya mwili mapaja na mbavu, nyama katika sehemu za siri, kipande cha mfupa kwenye jeraha la paji la uso, na upande wa pili tuliotambulishwa kuwa ni baba wa marehemu Jockson Makundi tulikuchukuwa sampuli ya damu na ute wa mate na kuhifadhiwa vizuri katika kupeleka kwa mkemia mkuu wa serikali,"alisema

## Mbaroni tuhuma za kumnyonga mwanawe

**Na Futuna Seleman, PWANI**

JESHI la Polisi mkoani Pwani, linamshikilia fundi ujenzi Robison Ernest (33), mkazi wa mtaa wa Vitendo, tarafa ya Misugusugu wilayani Kibaha kwa tuhuma za kumnyonga mtoto wake mwenye umri wa miezi sita Modesta Robison kwa madai kuwa si mwanawe.

Kamanda wa Polisi mkoani Pwani, ACP Wankyo Nyigesa, alisema chanzo cha mauaji hayo ni mtuhumiwa kumtuhumu mke wake kuwa na uhusiano na mwanaume mwingine ambaye anamtuhumu kuwa ndiye baba halali wa marehemu mtoto huyo.

Alisema hali hiyo ilileta mgogoro wa mara kwa mara kati yao na kusababisha tukio hilo.

"Jeshi la Polisi lilimuhoji mama mzazi wa marehemu mtoto, alitueleza kuwa mtuhumiwa aliwahi kufanya jaribio la kumuua mtoto wake kwa kumnywesha sumu ya vidonge, lakini alimuwahi mtoto na mara ya pili alinoa panga kwa nia ya kumkata mtoto, lakini hakufanikiwa, pia mpaka tarehe 1/4/2019, mtuhumiwa alifanikiwa kumnyonga mtoto hadi kufariki dunia," alisema Kamanda.

Alisema polisi inamshikilia mtuhumiwa huyo na mwili wa marehemu umehifadhiwa Hospitali ya Rufani ya Tumbi.

"Tunatoa rai kwa wananchi wanapoona jambo la uharibifu, watoe taarifa mapema ili hatua ziweze kuchukuliwa kabla madhara zaidi hayajatokea na watuhumiwa wadhibitiwe.

## SHUKRANI



Familia ya Marehemu **Mzee Ali Tukai wa Kibamba** Dar-es-salaam inatoa shukrani za dhati kwa ndugu, jamaa, majirani, marafiki na wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine kufanikisha msiba na mazishi ya Mpendwa wao **Thomas Mgante Tukai** aliyefariki jijini Calgary, Canada tarehe **4/12/2018** na kuzikwa Kibamba Dar-es-salaam tarehe 15/1/2019. Upendo mliouonyesha hauna kipimo na umetupatia faraja isiyoelezeka.

Ni vigumu sana kumshukuru mtu mmoja mmoja kwani walioshiriki ni wengi mno. Pamoja na hayo, shukrani za kipekee ziwaendee Umoja wa Watanzania waishio Canada, hasa Familia za Dr. Kachua, Raymond Njiku, Immanuel Kijazi na Anthony Semesi; Askofu Bernadin Mfumbusa na Fr. Richard wa Jimbo Katoliki Kondoa; Fr. Prijo Joseph, Paroko wa Parokia ya Kibamba; Crimson Travel (T) Ltd; Marafiki wa Mgante wa Aga Khan Primary na Mzizima Sekondari; Marafiki wa karibu na washirika wa Mama Mgante katika mashirika mbalimbali; wafanyakazi na marafiki wa karibu wa kaka na dada wa Mgante; kamati ya mazishi na wana jumuiya.

Mwisho, familia inatoa shukrani za dhati kwa ndugu na marafiki wa karibu walioratibu shughuli za msiba kwa ujumla na mazishi.

**Familia inawakaribisha kwenye Misa ya Shukrani itakayofanyika Jumapili tarehe 7/4/2019 katika Parokia ya Kibamba kuanzia saa 2:30 asubuhi na baadae kukutana nyumbani.**

***"Kwa maana kwangu kuishi ni Kristo na kufa ni faida" (Wafilipi 1:21)***

RADIO One

POPOTE ULIPO SIKILIZA RADIO ONE KATIKA MASAFA YAFUATAYO




www.radioone.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Iwe bajeti inayolinda haki, maslahi ya wanyonge*

**MSINGI** mkuu wa haki za binadamu ni kwamba kila mtu anastahili mbalimbali si kwa kutegemea cheo, wala taifa, tabaka, jinsia, dini au sababu nyingine yoyote bali ni kwa kuzaliwa binadamu. Hivyo ni mambo anayostahili kuyafurahia bila kipingamizi.

Haki hizi zipo katika Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu lililotolewa na Umoja wa Mataifa (UN), mwaka 1948. Tamko hilo ni kamilisho la majadiliano kuhusu haki kwa wanadamu wote.

Hoja ya msingi ni kwamba, "watu wote wamezaliwa huru, hadhi na haki zao ni sawa. Wote wamejaliwa akili na dhamiri, hivyo yawapasa watendeane kindugu.

Tanzania inalinda na kuheshimu haki za binadamu. Ukweli huu unadhihirika inaporidhia mikataba mbalimbali ya kimataifa, yakiwamo ya matamko ya kimataifa yanayolenga makundi maalum. Imeridhia Tamko la Kimataifa la Haki za msingi za Binadamu la mwaka 1948, kadhalika mikataba kama ule wa haki za kiraia na kisiasa wa mwaka 1966 kulinda haki za kiuchumi na kijamii. Mikataba ya haki za wanawake, haki za mtoto pia za watu wenye ulemavu.

Pamoja na mikataba hiyo ya kimataifa suala la haki za binadamu bado ni tatizo nchini, ukatili wa kijinsia umeshamiri kiasi kwamba mabinti wanakosa haki ya kukua na kufikia utimilifu, wanabakwa na kupata mimba za utotoni, watoto hunajisiwa na kulawitiwa, wanawake kuuawa kwa kisingizio cha uchawi, wenye ulemavu kama albino huuawa, na kwa ujumla kundi hili hukosa haki za msingi kama elimu, ajira na huduma nyingine za kijamii.

Ndiyo maana wadau kama Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Mfuko wa Wanawake wa Umoja wa Mataifa (UN Women), Chama cha Wanahabari Wanawake (Tamwa), mara nyingi wanahimiza kuwa ni jukumu la serikali kulinda na kudumisha haki za binadamu na kuondoa aina zote za ukatili kwa kuandaa bajeti jumuishi yenye sura ya kijinsia na inayonufaisha watu wote.

Huu ndiyo wakati ambao bajeti ya serikali inatarajiwa kujadiliwa bungeni Dodoma, ni fursa ya kuwasilisha bajeti inayomgusa kila mtu kwa kumpaka haki na huduma anazostahili kama binadamu.

Tunategemea bajeti itakayojadiliwa itasimamia haki za binadamu kwa kuwajali wanawake na kupunguza kama si kuondoa vifo vya wajawazito na watoto wachanga. Ni bajeti itakayowagussa watu wanaoishi na ulemavu, mabinti, watoto wachanga na wazee. Tunategemea itatoa fedha na ruzuku zitakazojibu changamoto hizo. Aidha, itajenga mabweni ili mabinti wawe na haki ya kusoma na kulindwa dhidi ya wabakaji.

Ni imani yetu kuwa, bajeti hii itawalinda wazee na makundi ya wanyonge kwa kuwapa matibabu bure na huduma muhimu ili kuishi. Itawahudumia wanawake kwa kutoa huduma salama za uzazi ili kulinda haki ya afya ya mama na mtoto na kuzuia vifo na magonjwa ili kuwahakikishia haki za kuishi.

Tunategemea kuwa pamoja na kubainisha vipaumbele kama ujenzi wa miundombinu, iwe bajeti itakayosimamia miradi ya kusambaza maji na kuwatua wanawake ndoo kichwani ili kuwaepusha na kuvamiwa na kuuawa na wanyama usiku wa manane wakati wakisaka maji maporini.

Watanzania wanategemea bajeti yao itakuwa na mafungu ya kutosha ya kuwasaidia wananchi kupata dawa na matibabu ya kuridhisha hospitalini, huduma za misaada ya kisheria wanapokuwa na mgogoro wa kisheria na kwa ujumla huduma zote za msingi ambazo ni haki zao kwa kuwa wamezaliwa binadamu wanaoishi Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Salome Kitomari

# *Wananchi watimize wajibu wao NEC ikitekeleza majukumu yake*

**UANDIKISHAJI** wa wapigakura kwa majaribio kwa mfumo wa kielektroniki (Biometric Voter Registration (BVR), umeanza katika kata ya Kibuta Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani na Kihonda Manispaa ya Morogoro, mkoani Morogoro.

Uandikishaji huo unafanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), yenye jukumu la kisheria la kusimamia uchaguzi unaofanyika nchini.

Ni wa majaribio kabla ya kuanza rasmi kwa uandikishwaji wa wapigakura kwenye maeneo mbalimbali nchini, ikiwa ni pamoja na uhakiki wa daftari la wapigakura ili waweze kushiriki kikamilifu uchaguzi mkuu wa mwakani.

Kwa mara ya kwanza mwaka 2015, Watanzania waliandikishwa kwenye mfumo wa BVR na walipiga kura kwa kutumia vitambulisho maalum, lengo ni kuondokana na matumizi ya karatasi na changamoto zozote zinazoweza kujitokeza ikiwamo kuchelewesha matokeo ya kura.

Moja ya changamoto zilizojitokeza wakati wa uhakiki wa daftari la wapigakura ni majina kuingiliana, kukosekana, picha za wahusika kuonekana tofauti na kuwapo kwa picha za vitu badala ya watu.

Katika kipindi hiki cha uandikishaji wa majaribio na uhakiki, Muungwana ana imani kuwa kutakuwa na umakini mkubwa ili marehemu wasiwe wapigakura.

Jambo ambalo limekuwa likilalamikiwa kwa mfumo huo kwa nchi za Afrika ni kuwa na majina ya wapigakura ambao wapo kwenye daftari, lakini walishafariki.

Kwamba walistahili kuondolewa lakini wakati wa uchaguzi mkuu, majina yao huendelea kuwepo kwenye daftari.

Wanakuwa na nafasi ya kupigakura, jambo linaloacha maswali kwamba iweje marehemu awe na uwezo wa kupigakura au kushiriki kwa namna yoyote mchakato wa uhakiki, mbali na jina lake kuendelea kubaki kwenye daftari!

Hadi kufikia uchaguzi mkuu mwakani, imebakia mwaka mmoja na miezi sita, muda ambao ni wa kutosha kabisa kuhakiki daftari, kuandikisha wapigakura wapya ambao wamekidhi vigezo kwa mujibu wa katiba, sheria na taratibu za Tanzania.

Pia, muda huo unatosha kwa maana kwamba hata hatua ya kubandika majina ya wapigakura kwenye mbao za matangazo katika vituo vya uandikishaji ili watu wahakiki majina yao utakuwa mwingi.

Yaani kwa waliojiandikisha na kukosa majina, hatua zitachukuliwa, lakini pia majina ya wasiostahili kuwapo yataondolewa na kasoro zingine kurekebishwa ili inapofika wakati wa uchaguzi mkuu, kusiwe na zima moto.

Hata hivyo, Muungwana ana imani kuwa zima moto itajitokeza pale ambapo panabaki miezi michache ndipo hatua za uandikishaji zinaanza kuchukuliwa na wakati huo huo kuna ulazima wa kuhakiki daftari ili kuondoa makosa ya kibinadamu yanayoweza kujitokeza.

Aidha, Muungwana anaona kwamba huu pia ni wakati mwafaka wa kutolewa kwa elimu ya uraia ili wananchi wenye sifa ya kupigakura wajiandikishe na kupata vitambulisho ambavyo umuhimu wake si katika kupigakura tu, bali kama moja ya vitambulisho muhimu.

Nyaraka hizo zinakubalika kama kitambulisho rasmi kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo benki, polisi, na ofisi zingine, ingawaje umuhimu wake wa kwanza ni katika kutekeleza haki ya msingi ya kupigakura kumchagua rais, wabunge, madiwani na viongozi wa serikali za mitaa.

Katika uchaguzi uliopita kitambulisho hicho kilipewa majina mengi likiwamo la kichinjio au kisu kwa kuwa kilikuwa kinakwenda kufanya maamuzi ya nani awe kiongozi katika nafasi mbalimbali.

Ni wajibu wa kila mwananchi kupata kitambulisho hicho kwa ajili ya kupigakura katika uchaguzi mkuu wa mwakani na uchaguzi mwingine, hivyo ni vyema watu wakajitokeza kwa wingi kupata vitambulisho hivyo muhimu kwao.

Wakati Nec ikitekeleza wajibu wake, wananchi nao wanapaswa kutekeleza wajibu wao kwa kujitokeza kujiandikisha na kuwa na uhalali wa kuchagua viongozi wanaoona watafaa kuwaongoza kwa miaka mingine mitano.

Wakati wa uhakiki wa taarifa za wapigakura, na kujiandikisha utakapowadia wananchi wajitokeze kwa wingi ili kupata vitambulisho, lakini zaidi kupata haki ya kupigakura wakati wa uchaguzi mkuu mwakani.

# Mdee asimamishwa tena, amponza Lema

INATOKA UK 2

Roho ya mwenendo wa nchi inategemea uimara wa Bunge, sasa amesema Bunge ni dhaifu, ni kweli, na mimi kama mbunge wa vipindi vitatu nathibitisha hilo".

Mwakasaka alibainisha kuwa hati ya wito ilimtaka Mdee kueleza kuhusu maneno aliyoyazungumza ambayo maudhui yake yalilalamikiwa kukiuka masharti ya Kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge Sura 296 kinachoeleza kuwa mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo kwa makusudi atafanya kitendo chochote cha kudharau Bunge.

Aliongeza kuwa Mdee alifika mbele ya kamati akiwa na nyaraka mbalimbali ikiwa ni pamoja na taarifa yake kuhusu kuunga mkono kauli ya CAG Assad kuwa Bunge ni dhaifu iliyopokewa kama kielelezo 'A' na Ripoti ya CAG Kuhusu Ukaguzi wa Mashirika kwa Mwaka wa Fedha 2014/15 iliyopokewa kama kielelezo 'B'.

Mwakasaka alilieleza Bunge kuwa, akiwa mbele ya kamati, Mdee alikiri wazi kutamka maneno kuwa Bunge ni dhaifu ambayo ndiyo yanalalamikiwa, lakini alitoa maana ya neno udhaifu kwa mujibu wa Kamusi Kuu ya Kiswahili kuwa ni "hali ya kukosa nguvu kimaumbile, kifedha, kiuwezo na kiutendaji".

Hata hivyo, kiongozi huyo wa kamati alisema walifanya utafiti kwa kuangalia maana ya neno 'dhaifu' katika Kamusi Kuu ya Kiswahili iliyoidhinishwa na Baraza la Kiswahili Tanzania na Baraza la Kiswahili la Taifa Kenya (KICD) inayotafsiri neno hilo kuwa ni "isiyokuwa thabiti kiafya, nyonge, yenye kutokuwa na mashiko, goigoi, legevu, hafifu, isiyo imara, sahihi, thabiti, kiumbe kama vile mtu au mnyama asiye na nguvu, dhuli".

Mwakasaka ambaye pia ni Mbunge wa Tabora Mjini (CCM), alisema Mdee aliiambia Kamati kuwa aliunga mkono kauli ya CAG Assad kwa kuwa ni haki yake kikatiba (Ibara ya 18 na 30) kutoa maoni, lakini akakiri kukosea kutumia neno 'udhaifu' dhidi ya Bunge baada ya kuelezwa maana yake kwa mujibu wa kamusi.

Alisema kuwa katika utetezi wake, Mdee alitoa mifano mbalimbali iliyomsukuma kutoa kauli yake kuwa Bunge ni dhaifu ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa Deni la Taifa, hasara ya Shirika la Ndege (ATCL), serikali kukopa fedha katika mifuko ya hifadhi ya jamii na kutorejesha kwa wakati, kuondolewa kwa matangazo ya moja kwa moja ya Bunge, utunzi wa Sheria ya Makosa ya Mitandao na ile ya Huduma za Habari alizodai "zinazokandamiza na kupunguza uhuru wa raia" na shinikizo la wenyeviti wa kamati walio mwiba kwa serikali kujiuzulu.

Kiongozi huyo wa Kamati alieleza kuwa baada ya kumweleza Mdee maana ya neno 'dhaifu' lililotumiwa na Prof. Assad dhidi ya Bunge kwamba ni 'legelege, goigoi, isiyo imara' kwa mujibu wa kamusi ya Kiswahili Sanifu, alikiri kufanya makosa kuunga mkono kauli ya CAG, lakini hakuonyesha kujutia.

Kutokana na mbunge huyo kutojuta mbele ya kamati kitendo chake cha kumuunga mkono CAG Assad, Mwakasaka alisema kamati iliona alikuwa na dhamira ovu ya kulidharau na kulidhalilisha Bunge mbele ya umma.

Mwakasaka alisema kamati yake inapendekeza Mdee afungiwe kushiriki mikutano miwili ya Bunge kuanzia jana, huku akidokeza kuwa mbunge huyo alitakiwa kupewa adhabu kubwa zaidi kutokana na rekodi yake ya kufanya makosa mara kwa mara, hiyo ikiwa ni mara yake ya nne kufikishwa mbele ya kamati hiyo katika kipindi chake cha miaka 14 bungeni.

Alisema wamependekeza adhabu hiyo ya kukosa mikutano miwili kwa kuzingatia kwamba Bunge la 11 limebakisha muda mfupi kufika ukomo.

Baada ya kujadili pendekezo hilo, Bunge liliazimia kumfungia Mdee kushiriki mikutano miwili ya Bunge kuanzia jana. Kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, mbunge aliyefungiwa, kwa kipindi chote cha adhabu atapokea nusu mshahara na posho zote za kibunge.

**LEMA KIKAANGONI**

Kabla ya Bunge kuridhia pendekezo la Bunge kumfungia Mdee, Mbunge wa Arusha Mjini (Lema), wakati akichangia hoja, alinukuu maneno yaliyomponza mbunge wa chama chake (Mdee) kisha akaunga mkono kuwa Bunge ni dhaifu.

"Mheshimiwa Naibu Spika, sidhani kama ninaweza kushawishi Bunge kuondoa adhabu ambayo imeshapendezwa na Mwenyekiti wa Kamati. Maneno yafuatayo ndiyo yanamfanya Halima apendekezewe adhabu kubwa kiasi hicho, nayanukuu;

'Kitendo cha CAG kusema kwamba hali si nzuri halafu chombo kinachotakiwa kusimamia hali hakifanyi hivyo, ni cha kijasiri na nina imani wanaoongoza huo mhimili watakuwa wavumilivu. Hawatafikiri kumwita kwenye Kamati ya Maadili kwa sababu tumeitwa dhaifu kwa sababu kweli ni dhaifu...

'Roho ya mwenendo wa nchi inategemea uimara wa Bunge, sasa amesema Bunge ni dhaifu, ni kweli, na mimi kama mbunge wa vipindi vitatu nathibitisha hilo'.

"Mheshimiwa, na mimi mbunge wa vipindi viwili, nathibitisha Bunge hili ni dhaifu," Lema alisema.




# Ajira CAG Assad yawekwa mtegoni

INATOKA UK 2

ote au kwa sababu ya tabia mbaya.

Ibara ya 144(4) ya Katiba hiyo inaeleza kuwa ikiwa tume iliyoteuliwa kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya tatu (3) itamshauri Rais kwamba huyo CAG aondolewe kazini kwa sababu ya kushindwa kufanya kazi kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote au kwa sababu ya tabia mbaya, basi Rais atamwondoa kazini.

Ibara ya 144(5) ya Katiba hiyo inaeleza kuwa ikiwa suala la kumwondoa kazini CAG limepelekwa kwenye tume kwa ajili ya uchunguzi kwa mujibu wa masharti ya ibara hii, Rais ataweza kumsimamisha kazi huyo CAG, na Rais ataweza wakati wowote kufuta uamuzi huo wa kumsimamisha kazi, na kwa hali yoyote uamuzi huo utabatilika ikiwa tume itamshauri Rais kwamba huyo CAG asiondolewe kazini.

Ibara ya 144(6) ya Katiba hiyo inaeleza kuwa mtu ambaye ni CAG au aliyepata kuwa CAG hawezi kuteuliwa kushika au kushikilia madaraka ya kazi nyingine yoyote katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

**ILIVYOKUWA BUNGENI**

Kupitishwa kwa azimio la Bunge kutofanya kazi na CAG kumetokana na uamuzi wa Spika Job Ndugai, kuiagiza Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, kufanya uchunguzi kubaini kama CAG Assad alihusika kusema kuwa Bunge ni dhaifu alipohojiwa na Idhaa ya Kiswahili ya Umoja wa Mataifa Januari 9, mwaka huu.

Akiwasilisha taarifa ya shauri hilo bungeni jana, Mwenyekiti wa kamati hiyo, Emmanuel Mwakasaka, alisema kwenye mahojiano hayo, mtangazaji alimhoji CAG Assad: "Naona Ofisi ya CAG kwa upande wa Tanzania inafanyakazi nzuri sana ya kutoa ripoti kila mwaka zinazoonyesha ubadhirifu wa fedha, lakini hawaoni hatua zinazofuata baada ya hapo..."

Mwakasaka alisema kufuatia swali hilo, Prof. Assad alijibu: "Kimsingi ni kazi ya Bunge, kama tunatoa ripoti kuna ubadhirifu lakini hatua hazichukuliwi, huo kwangu ni udhaifu wa Bunge. Bunge linatakiwa lisimamie na lihakikishe kuwa pale penye matatizo hatua zinachukuliwa, kazi yetu ni kuripoti tu na huo udhaifu ni jambo la kusikitisha.

"Lakini tatizo kubwa nahisi Bunge linashindwa kufanya kazi yake inavyotakiwa, labda nasema jambo hili kwa sababu kuna husisha watu fulani, lakini nafikiri Bunge likifanya kazi yake vizuri hata udhaifu unaoonekana..."

Kiongozi huyo wa kamati alisema kutokana na kauli hizo za CAG Assad, Spika kwa niaba ya Bunge aliona maelezo hayo yana walakini na dalili za dharau kwa chombo hicho ndiyo maana akaelekeza kamati ikutane ili kuchunguza kauli hizo na kutoa mapendekezo kwa mujibu wa kanuni.

Alisema baada ya maelezo hayo, Prof. Assad alipewa hati ya wito kwa mamlaka ya Bunge chini ya vifungu vya 15 na 16 vya Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge, Sura ya 296 ya kuamuru mtu yeyote kufika mbele ya Bunge au kamati kutoa ushahidi kuhusu jambo lolote kama litakavyofafanuliwa katika hati ya wito.

"Hati ya wito ilimtaka shahidi (CAG Assad) kutoa maelezo ya kuhusika au kutohusika kwake kwenye tuhuma zinazomkabili na kama ikibainika, aeleze kwanini asichukuliwe hatua kwa kukiuka Kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge," alisema.

Mwakasaka alilieleza Bunge kuwa Januari 21, mwaka huu, CAG Assad alifika mbele ya kamati na alipohojiwa, alithibitisha kuwa Januari 9, mwaka huu, akiwa Marekani, kupitia Idhaa ya Kiswahili ya Umoja wa Mataifa, ni kweli yeye ndiye aliyetoa kauli zinazolalamikiwa.

"Ni kweli nilifanya mahojiano na UN Radio, New York, Marekani. UN Radio ipo ndani ya makao makuu ya UN, ni chombo cha Umoja wa Mataifa ikiwamo Tanzania. Nilihojiwa na mtangazaji Arnold Kayanda, aliniuliza swali ambalo mmelisikia au kulisoma na nililijibu kitaaluma... Maneno yaliyotumiwa ni udhaifu wa Bunge," Mwakasaka alinukuu maneno yaliyotolewa na CAG Assad mbele ya kamati.

Alisema CAG aliieleza kamati kuwa



Mthibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Profesa Musa Assad

hakuwa na nia ya kudharau Bunge, bali tatizo lililopo ni tofauti ya tafsiri ya maneno aliyoyatumia.

"CAG alisema maneno aliyoyatumia katika mahojiano "udhaifu wa Bunge" ni maneno ya kawaida kwa kuwa neno dhaifu ni neno la kawaida katika lugha ya ukaguzi wa hesabu," Mwakasaka alisema.

Alimnukuu CAG akisema: "Majibu yangu katika mahojiano, hayakuwa na nia ya kudhalilisha Bunge hata kidogo. Katika lugha ya kikaguzi, udhaifu huja kwa namna mbili, kwanza ni katika tathmini za taasisi na mifumo na pili ni katika kukazia hoja kuonyesha kiwango cha upungufu ndani ya taasisi moja.

"Hapa nashadadia kuwa neno dhaifu ni neno la kawaida sana katika mazungumzo yetu ya kazi ya kikaguzi. Tukizungumzia udhaifu wa Bunge, tulikuwa tunaongelea udhaifu katika utekelezaji wa mapendekezo ambayo tumeyatoa. Si jambo jingine katika utekelezaji wa majukumu ya Bunge."

Mwakasaka ambaye pia ni Mbunge wa Tabora Mjini (CCM), alisema CAG alipohojiwa kuhusu maana ya neno 'udhaifu' kwa wananchi wa kawaida na watu ambao taaluma yao siyo wahasibu wa wakaguzi, alijitetea kuwa alikuwa na maana ya upungufu na si vinginevyo.

Alisema alipoonyeshwa tafsiri ya neno dhaifu kama lilivyotafsiriwa kwenye Kamusi ya Kiswahili Sanifu inayoeleza kuwa ni 'goigoi au gonjwa', CAG Assad alionyesha kutounga mkono tafsiri hiyo ya kamusi.

Mwakasaka alieleza kuwa kutokana na ushahidi wa CAG wa kukiri kutoa kauli zinazolalamikiwa na jambo hilo kuthibitishwa na ushahidi wa video iliyosambaa kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, ikimwonyesha Prof. Assad akihojiwa, kamati ilimtia hatiani kwa kutoa kauli hiyo dhidi ya Bunge.

"Kwa sababu hiyo, kamati imejiridhisha ni kweli Prof. Assad alitamka maneno yaliyolalamikiwa kuwa yanaonyesha dharau na yanadhalilisha Bunge," Mwakasaka alisema.

Kiongozi huyo wa kamati alisema kauli hiyo ni dhahiri ililenga kulishushia hadhi Bunge na hivyo kulidharau na kulidhalilisha Bunge mbele ya umma na duniani ambako taarifa hizo zitakuwa zimefika kwa kuwa CAG alihojiwa nje ya nchi na chombo cha habari cha kimataifa.

Alisema utetezi na ushahidi kuwa alipohojiwa alimaanisha udhaifu wa Bunge hakuwa na maana kama Bunge ni dhaifu hauna mashiko kwa kuwa maana ya neno dhaifu haibadili udhalilishaji uliofanywa kwa chombo hicho cha kutunga sheria.

"Neno udhaifu ni mnyumbulisho tu wa neno dhaifu ambalo vyovyote litakavyotumika katika matumizi ya lugha ya Kiswahili linaeleza na kuleta hadhi hasi ya kitu kinachozungumzwa.

"Mazingira aliyotumia neno dhaifu hayakuwa katika kutekeleza kazi za kihasibu au kikaguzi, bali aliongea na ulimwengu mzima ambao si wote ni wahasibu au wakaguzi," Mwakasaka alisema.

Aliongeza kuwa kamati iliridhika kuwa shahidi (CAG Assad) hakutoa angalizo lolote kuwa anazungumza katika tafsiri za kihasibu ili kuzuia tafsiri ya kawaida ya lugha.

"Akiwa kwenye kamati CAG, alikiri kuwa maneno aliyoyatumia yameleta tafrani na malumbano makali hasa kwenye magazeti na mitandao mbalimbali ya kijamii.

"Kamati iliona kuwa ujumbe uliotolewa haukuwalenga wakaguzi wala wahasibu, bali yeyote aliyemsikiliza. Kushindwa kwake kuchukua tahadhari, kunadhihirisha kuwa alidhamiria kufanya kitendo hicho chenye kudharau na kudhalilisha Bunge na shughuli zake," Mwakasaka alisema.

"CAG alipoulizwa kama kuna kamusi ya kiuhasibu inayoeleza kuwa neno 'dhaifu' ni upungufu, alijibu kuwa hakuna mahali palipoandikwa tafsiri hizo. Aliulizwa pia kama amewahi kuiita ofisi yake kuwa dhaifu kwa kuwa ni neno la kawaida, pia alikana kuwa hajawahi.

"Pamoja na shahidi kukiri neno dhaifu alilolitumia halikupokelewa vema na umma, lakini hakuwa tayari kukiri kukosea au kuacha kutumia neno hilo lenye kudhalilisha," Mwakasaka alisema.

**MAPENDEKEZO YA KAMATI**

Mwakasaka alisema kamati inaona CAG alikusudia kufanya udhalilishaji na alikuwa na nia ovu dhidi ya Bunge kwa kuwa alipohojiwa, aliithibitishia kamati kwamba aliyapima maneno aliyoyatumia kabla ya kufanya mahojiano husika na alijiridhisha kuwa yote ni sahihi, hivyo ni wazi hata athari zilizojitokeza alizijua.

Kiongozi huyo wa kamati alisema kamati pia imejiridhisha pasipo shaka kuwa CAG hakuwahi kujutia kauli yake akiwa mbele ya kamati au nje ya kamati.

"Hakuwa tayari kuona kuwa, kitendo alichofanya kina dosari licha ya kuwa wakati wote wa mahojiano kamati ilijitahidi kumfahamisha juu ya madhara ya kauli yake kwake kama kiongozi.

"Kitendo cha CAG kushindwa kuona tatizo alilosababisha kwa kauli yake, madhara aliyosababisha kwa Bunge, wabunge kwa watu wanaowawakilisha, kushindwa kuomba radhi na kusahihisha kauli yake, hayo yote yameifanya kamati kuona kuwa hilo ni tatizo kubwa la kiongozi huyo," Mwakasaka alisema.

Baada ya maelezo hayo, mwenyekiti huyo alisema kamati yake imejiridhisha bila kuacha shaka kuwa kauli za Prof. Assad zililenga kudharau Bunge, kudhalilisha na kushusha heshima na hadhi ya chombo hicho.

"Kitendo cha Prof. Assad kutumia chombo ambacho kinasikilizwa ulimwengu mzima kutamka maneno yanayodhalilisha na kushusha hadhi heshima ya Bunge, si kitendo cha kuvumilika.

"Hivyo basi, kamati inatoa rai kwa wananchi, viongozi wa serikali kuheshimu Bunge na sheria za nchi tulizojiwekea ili kulinda hadhi na heshima ya Bunge," Mwakasaka alisema na kuhitimisha kwa kutoa hoja Bunge liazimie kutofanya kazi na CAG, hoja ambayo iliungwa mkono na wabunge wengi baada ya majadiliano.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Ijumaa tarehe 05-04-2019 kampuni ya MEGA BEVERAGES LIMITED itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka KILOMBERO kuelekea ARUSHA, gari hizo zenye namba za usajili: **T 228 DDS / T 572 DCV na T 227 DDS / T 570 DCV**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

**T 228 DDS / T 572 DCV**
**Urefu - mita 15.30**
**Upana - mita 2.4**
**Kimo - mita 4.6**

**T 227 DDS / T 570 DCV**
Urefu - mita 15.30
Upana - mita 2.4
Kimo - mita 4.6

3. Njia itakayotumika: **KILOMBERO hadi ARUSHA kupitia CHALINZE,** Gari zitasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215155302

# Magufuli awatangazia kiama wapotoshaji

INATOKA UK 2

wa na kilo chache ni kawaida katika maisha ya kawaida. Nafikiri watakuwa ni hawa 780, ila wasirudie kwenye msimu unaokuja kuwaumiza wananchi wadogo," alisema.

Rais Magufuli alisema vyama vya msingi vimekuwa vikighushi kwa kuandika majina ambayo hayapo.

"Nataka Mkuu wa Mkoa, OCD, na Kamanda wa Polisi Mkoa na Wakuu wa Wilaya muwashughulikie hawa wanaoorodhesha majina ambayo hayapo, wanatucheleweshea kwenye zoezi hili ambalo tunataka tuwalipe wananchi mapema waanze kuandaa msimu unaokuja," alisema.

"Hatuwezi kuendekeza maovu haya na Mkuu wa Mkoa siku nyingine nikija uniambie hawa tayari wameshahukumiwa miezi kadhaa, viongozi wa vyama vya shirika warudishieni wananchi korosho zao mnazotaka kuzidhurumu, kangomba jisalimisheni mseme mna kilo ngapi," alisema.

**FEDHA ZILIZOLIPWA**

Rais Magufuli alisema fedha za malipo ya korosho ambazo zimeshalipwa ni Sh. Bilioni 578.7, malipo mengine usafiri ni Sh. bilioni 5.1, magunia Sh. bilioni 6.4, Amcom Sh.bilioni 3, vyama vikuu vya ushirika Sh. bilioni 670, waendeshaji wa maghala Sh. bilioni 6.6, uratibu Sh. bilioni 1. 3.

"Tulianza wa wananchi 390,765 wenye korosho chini ya kilo 1,500 waliokuwa na tani zaidi ya 160,669.3 ambazo gharama yake ni Sh. bilioni 521.8, wakulima wengine waliolipwa ni 373, 146 walikuwa na tani 156, 865.2.

"Wakulima 170,616 waliokuwa na kilo 1500 hawajalipwa kwa sababu mbalimbali, wapo waliowekewa fedha kwenye benki lakini majina ya akaunti ni tofauti na lake wengine walikuwa hawana akaunti na niwaambie fedha ya serikali haiendi hivyo. Mpaka sasa asilimia 99 waliokuwa na kilo chini ya 1500 tumeshawalipa," alisema.

Rais Magufuli alisema wameanza kazi ya kubangua korosho kwa tani 15,000 na baadaye wataendelea.

HABARI KITAIFA

# Watatu mbaroni kwa tuhuma za mauaji

**Na Stevie Chindiye, TUNDURU**

JESHI la Polisi wilayani Tunduru mkoani Ruvuma linawashikilia watu watatu kwa tuhuma za mauaji ya mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Muhuwesi, Tariki Issa Mohamed, yaliyotokea Machi 28, mwaka huu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Marwa, aliwaambia waandishi wa habari kwamba watuhumiwa hao walikamatwa kufuatia jeshi hilo kupokea taarifa kutoka kwa msiri.

Aidha, katika taarifa hiyo Kamanda Marwa alisema miongoni mwa watuhumiwa hao yupo mnunuzi wa baiskeli aina ya Apolo namba M.990026507 yenye rangi ya bluu na thamani ya Sh. 150,000 ambayo walichukua kwa marehemu baada ya kutekeleza mauaji hayo.

Kamanda Marwa aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Bakari Omari Said (21), ambaye kabla ya kukamatwa alionekana kuwa na baiskeli aliyoporwa marehemu katika tukio hilo.

Alimtaja mtuhumiwa wa pili ambaye alitajwa kushirikiana na mtuhumiwa namba moja kuwa ni Sadid Mtila Said (26), aliyetajwa na mtuhumiwa namba moja kuwa alishirikiana naye katika tukio hilo na kueleza eneo ambako walikwenda kuiuza baiskeli hiyo.

Alisema baada ya ufuatiliajai wa taarifa hizo pia walifanikiwa kumnasa Thabit Mohamed Makunula (23), akiwa na baiskeli hiyo aliyodai kuuziwa na watuhumiwa hao mbele ya Mtendaji wa Kijiji cha Ligunga, Samama Amidu Matola.

Alisema baada ya tukio hilo baiskeli hiyo ilichukuliwa na kupelekwa katika Kituo cha Polisi Wilaya ya Tunduru na baadaye kutambuliwa na baba mzazi wa marehemu Isa Mohamed, kuwa ni mali yake.

Alisema watuhumiwa wote wanatarajiwa kufikishwa mahakamani baada ya taratibu za awali za upelelezi kukamilika.



Mhandisi kutoka Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi), kitengo maalum cha ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara, Upendo Sanze, akielekeza jambo kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Kwa Mtoro, wilayani Chemba mkoani Dodoma, kuhusu umuhimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi waomba 50% bei ya maji

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

WANANCHI mkoani Mwanza wameomba mabadiliko ya ongezeko la bei ya huduma za majisafi nyumbani iwe kwa asilimia 50 na siyo 100 kama Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (Mwauwasa) ilivyopendekeza.

Wananchi hao walisema hawakubaliani na pendekezo la ongezeko la bei la asilimia 100 kwa matumizi ya maji nyumbani kwa kuwa gharama hiyo ni kubwa ikilinganishwa na maisha ya Watanzania wengi ambao wanakipato cha chini.

Miongoni mwa wananchi hao akiwamo Omary Masanja, Sabina Haruni na Jerome James, walitoa ombi hilo katika mkutano (taftishi) wa wadau wa kutoa maoni kuhusu maombi ya marekebisho ya bei za Mwauwasa ulioandaliwa na Mamlaka ya Udhibiti Nishati na Maji(EWURA), jijini Mwanza.

Walisema hawaoni sababu ya ongezeko la bei kwa asilimia 100 wakati Mwanza chanzo chake cha maji ni Ziwa Victoria tofauti na mikoa mingine, hivyo wanapendekeza gharama iongezeke kwa asilimia 50, pia waongeze uniti za ujazo kutoka 0-10 kwa matumizi ya nyumbani hadi 0-20 huku wakiipongeza mamlaka hiyo kwa kuondoa tozo za huduma (service charge).

Pia waliomba mamlaka hiyo kuangalia taasisi kama shule na nyumba za ibada ziwe zinalipa katika viwango maalum, kwa kuwa zinasaidiwa na jamii na ikizingatiwa uhitaji wa maji ni mkubwa husussani shule nyingi za msingi kukatiwa maji na kufanya utaratibu wa kuweka mita za Luku kama za Shirika la Umeme nchini (Tanesco), ambayo unalipia kwa kadiri ya unavyotumia.

Aidha, walisema mamlaka hiyo inapaswa kudhibiti upotevu wa maji mitaani ambao unasababisha kukusanya fedha kidogo, huku gharama za uendeshaji zikiwa kubwa na kuiomba serikali kuondoa tozo kwenye vifaa vyote vinavyotumika katika suala la maji.

Meneja Ewura Kanda ya Ziwa, George Mhina, ambaye alikaimu nafasi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, alisema mkutano huo ni sehemu ya uchunguzi unaofanywa na Ewura kupata maoni ya wadau wa huduma ya maji kabla ya kutoa maamuzi kuhusu maombi yaliyowasilishwa na Mwauwasa ya kurekebisha bei ya maji na waamini kupitia taftishi hiyo yatasaidia kufikia uamuzi wa haki wa maombi hayo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mwauwasa, Anthony Sanga, alisema sababu ya kuomba mabadiliko hayo ya bei ni kutokana na watu kuongezeka na uhitaji kuwa mkubwa.

Alisema, mamlaka hiyo inakusudia maombi ya ongezeko bei na gharama itawasaidia kuboresha huduma ya majisafi na taka katika jiji hilo kwa kufanya matengenezo na kuongeza mtandao wa maji kwa maeneo yasiyokuwa na huduma hiyo.

Pia alisema, mabadiliko ya bei wanayopendekeza kwa matumizi ya nyumbani ni asilimia 100 ambayo sawa na Sh. 1,400 kwa matumizi ya nyumbani kwa kundi linalotumia uniti za ujazo 0-10 na iliyopo ni Sh. 700, kwa kundi la pili linalotumia uniti za ujazo 11-25 ni asilimia 95 sawa na Sh. 1,690 iliyopo ni Sh. 865, huku kundi la tatu linalotumia uniti za ujazo 25 na kuendelea ni asilimia 94 sawa na 1,745 huku iliopo ni 900.

## Wanafunzi wa kike watakiwa kuchangamkia fursa

**Na Siti Said**

WAHANDISI wa kike wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi), kupitia kitengo maalum cha ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara, wamewataka wanafunzi wa kike mkoani Dodoma, kuchangamkia fursa za usomaji wa masomo ya Sayansi na Hisabati ili kuongeza wataalamu katika fani ya uhandisi.

Akizungumza kwa niaba ya wahandisi hao katika Shule ya Sekondari ya Kwa Mtoro, wilayani Chemba mkoani Dodoma, Mhandisi Rahma Mwinyi, amesema kuwa sekta hiyo bado ina uhaba wa wataalamu wa kike, hivyo inahitaji wanafunzi kusoma masomo hayo ili kuongeza idadi ya wataalamu hao na kufikia uchumi wa viwanda ifikapo 2025.

"Hakikisheni mnasoma masomo ya Sayansi na Hisabati kwa bidii, ufaulu wa masomo haya utategemea ufanyaji wa maswali na mazoezi ya kujipima mara kwa mara ambayo yatawajengea uelewa na kupelekea kufaulu vizuri, serikali bado inahitaji wataalamu wa fani hii na pia fursa za ajira kupitia fani hii zipo nyingi, kazi kwenu kujipanga ili mfikie malengo yenu," alisema.

Aidha, Mhandisi Mwinyi aliwataka wanafunzi hao kuachana na dhana potofu ya kuwa masomo hayo ni magumu na badala yake kutafuta njia mbadala ikiwamo ya kupanga ratiba ya masomo yao vizuri na kuzingatia yale wanayofundishwa na walimu darasani.

Kwa upande wake, Mwalimu wa Shule ya Sekondari ya Kwa Mtoro, Neema Muna, kwa niaba ya walimu wenzake ameishauri serikali kuhakikisha wanapeleka vifaa vya maabara kwa shule ambazo hazina vifaa hususan vijijini kwa kuwa ufaulu wa masomo hayo hutegemea mazoezi kwa vitendo.

Alisema ipo haja kwa serikali kuajiri na kupeleka walimu wa kutosha katika shule zilizopo vijijini kulingana na idadi ya wanafunzi na pia huduma za maji na umeme ziboreshwe ili kukidhi mahitaji ya ufanyaji wa mazoezi kwa vitendo kupitia katika maabara zao.

Mwanafunzi Siminza Mambo wa shule hiyo, ameiomba serikali kuongeza walimu wa kike wa sayansi shuleni hapo kwa kuwa kwa sasa shule hiyo ina mwalimu mmoja pekee wa jinsia hiyo, hali inayowakatisha tamaa wanafunzi wa kike kujiunga na masomo hayo.

Pia, mwanafunzi Lucy Isack, kutoka shule hiyo ameiomba serikali kuongeza walimu wa Sayansi na Hisabati, vitabu na kuboreshea miundombinu ya maabara ikiwamo vifaa vya kupimia kemikali.

Ziara ya wahandisi hao katika shule mbalimbali za sekondari za mkoa wa Dodoma inalenga kuhamasisha usomaji wa masomo ya Sayansi na Hisabati kwa wasichana.

# Serikali imetwaa viwanda 14 vilivyobinafsishwa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

BUNGE limeelezwa kuwa hadi kufikia Februari 2019, serikali imetwaa viwanda 14 vilivyobinafsishwa kutokana na kutoridhishwa na baadhi ya wawekezaji ambao hawakutekeleza mikataba ya mauzo.

Hayo yalibainishwa jana bungeni na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Devotha Minja.

Minja alihoji bungeni ahadi ya Rais aliyoitoa wakati wa kampeni mkoani Morogoro kuhusu kumaliza tatizo la ajira kwa vijana kwa kuhakikisha anarudisha viwanda vilivyokufa na kuwashughulikia walioviua ili kurudisha ajira kwa vijana na wanawake.

Akijibu swali hilo, Manyanya alisema kati ya viwanda hivyo viwili ni vya Mkoa wa Morogoro ambavyo ni Mang'ula Mechanical and Mashine Tools na Dakawa Rice Mill Ltd.

"Kwa sasa viwanda vyote 14 vilivyorejeshwa serikalini vinaandaliwa utaratibu wa kutafuta wawekezaji wenye uwezo wa kuvifufua," alisema.

Hata hivyo, alisema kiwanda cha Morogoro Canvas Mill Ltd ambacho nacho kimefungwa, majadiliano yanaendelea kati ya mwekezaji na Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Aidha, alisema wizara hiyo kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina inaendelea kufuatilia kwa karibu viwanda vilivyobaki ambavyo havifanyi kazi vikiwamo viwanda vya Mkoa wa Morogoro ili kuchukua hatua stahiki.

Alifafanua kuwa mpango wa serikali ni kuhakikisha kuwa viwanda vyote vilivyobinafsishwa visivyofanya kazi vinafufuliwa na kuanza kazi ili vichangie katika uchumi na kutoa ajira kwa vijana.

Aidha, alisema serikali inahamasisha ujenzi wa viwanda vipya kutegemeana na fursa zinazopatikana nchini.

"Mkoa wa Morogoro una jumla ya viwanda 14 vilivyobinafsishwa kati ya viwanda hivyo, viwanda nane vinafanya kazi na viwanda sita havifanyi kazi," alisema.

Manyanya alisema wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina imefanya tathmini ya viwanda vilivyobinafsishwa nchini vikiwamo vya Mkoa wa Morogoro na kubaini kuwa baadhi ya wawekezaji hawajatekeleza kikamilifu makubaliano ya mikataba ya mauzo ikiwa ni pamoja na kutofanya uwekezaji kulingana na mpango uliokubaliwa.



Mbunge wa Viti Maalum kundi la wanawake kutoka mkoani Mara, Agnes Mathew wa pili kutoka kulia, akikabidhi mchango wa Sh. 500,000 kwa mchungaji wa kanisa la A.I.C. Ezron Shimba, kwa ajili ya uzinduzi wa albamu ya pili ya kwaya ya A.I.C. Neema.
**PICHA: AHMED MAKONGO**

# Vibali wasafirishaji mazao misitu usiku kuanza kutolewa

WIZARA ya Maliasili na Utalii imetangaza kuanza kutoa vibali maalum kwa wasafirishaji wa mazao ya misitu ya kupandwa kusafirishwa saa 24.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Naibu Waziri wa Wizara hiyo Constantine Kanyasu, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mafinga Mjini (CCM), Cosato Chumi. Chumi alihoji kama serikali iko tayari kubadilisha sheria au kanuni ili kuruhusu mazao ya misitu kusafirishwa usiku na mchana (masaa 24).

Akijibu swali hilo, Kanyasu alisema Sheria ya Kuzuia Kusafirishwa kwa Mazao ya Misitu Namba 68 ya Mwaka 2000 iliwekwa kutokana na changamoto za usafirishaji haramu wa mazao ya misitu na kwa wakati huo ilikuwa ni vigumu kudhibiti uhalifu huo wakati wa usiku.

Alieleza kuwa ukaguzi wa kina wa mazao ya misitu hufanyika kwenye kituo cha mwanzo cha safari na vituo vya ukaguzi vilivyoko barabarani kwa kukagua nyaraka mbalimbali ikiwa ni pamoja na kibali cha usafirishaji na kuangalia aina ya mazao, jamii ya miti na kiasi kinachosafirishwa.

"Kutokana na ugumu wa ukaguzi nyakati za usiku serikali ilitunga sheria kuzuia kusafirisha mazao ya misitu nyakati za usiku," alisema.

Alitaja sababu nyingine ya kuwapo kwa zuio la kusafirisha mazao ya misitu usiku wakati huo ni pamoja na uhaba wa watumishi, udanganyifu na ubadhirifu hali ambayo kwa sasa imeimarika.

"Hivyo, wizara itaanza kutoa vibali maalum kwa wasafirishaji wa mazao ya misitu ya kupandwa kusafirishwa saa 24," alisema.

Alitoa mfano kuwa mwaka 2018 kupitia Tangazo la Serikali namba 478, serikali imetoa kibali cha kusafirisha usiku nguzo za umeme kwa saa 24 ili kuharakisha usambazaji wa umeme vijijini.

Katika swali la nyongeza, Chumi alisema kama hali imeimarika kwanini serikali isiruhusu mazao hayo kusafirishwa muda wote.

Akitoa majibu ya nyongeza, Waziri Dk. Hamis Kigwangala alisema wapo kwenye mchakato wa kuruhusu usafirishaji huo na kwamba yeye sio muumini wa kuzuia watu wasifanye kazi usiku.

"Mabasi hayasafiri usiku, malori hayasafiri usiku, mbao hazisafiri usiku tunakwamisha ukuaji wa uchumi, lazima watu wafanye kazi mchana na usiku ndio maana nimetoa agizo kwa wataalamu wa wizara walete ushauri wa namna gani tutaweza kudhibiti uhalifu na vitu vingine, lakini watu wasafirishe mazao usiku,"alisema.

# Mbunge ataka maji yalipwe kwa mfumo wa Luku

SERIKALI imeagiza mamlaka zote nchini kuendelea kuwafungia wananchi dira za kulipa maji kadiri utumiavyo ili kupunguza malalamiko ya wananchi.

Hatua hiyo pia imeelezwa kuwa itapunguza tatizo la malimbikizo ya madeni ya matumizi ya maji.

Naibu Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Dk. Jasmine Bunga.

Alisema kumekuwapo na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi dhidi ya mamlaka za maji katika halmashauri kwa kuwapatia wananchi bili kubwa za maji ambazo haziendani na uhalisia.

"Je, ni lini serikali itaanzisha utaratibu wa kulipa maji kadiri utumiavyo katika utoaji wa huduma za maji kama ilivyo kwenye umeme," alihoji.

Aweso akijibu swali hilo, alisema serikali imeshaanza kutumia utaratibu wa kulipa maji kadiri unavyotumia katika maeneo mbalimbali nchini.

"Kwa sasa utaratibu huo umeanza kutumika katika maeneo yanayohudumiwa na Mamlaka za Arusha, Iringa, Songea, Dodoma, Tanga, Mbeya, Tabora, Mwanza, Moshi na Dawasa," alisema.

**"Kwa sasa utaratibu huo umeanza kutumika katika maeneo yanayohudumiwa na Mamlaka za Arusha, Iringa, Songea, Dodoma, Tanga, Mbeya, Tabora, Mwanza, Moshi na Dawasa," alisema.**



**Na Augusta Njoji, DODOMA**

# Wanafunzi wapewa elimu ya fedha

**Na Mwandishi Wetu, ARUSHA**

SHIRIKA la Maendeleo la Brac Tanzania, limetoa elimu ya fedha kwa wanafunzi na kutembelea wakopaji walioji-funza shughuli wanazofanya zikiwamo za kupunguza umas-kini na kuwawezesha watu maskini.

Kwa mujibu wa Meneja wa Fedha wa Kanda wa shirika hilo, Mohamed Madati, walipata elimu ya fedha na shughuli wa-nazofanya mwishoni mwa wiki.

Alizitaja shughuli wanazo-fanya na ambazo wakopaji walijifunza kuwa ni Mpango wa Usalama wa Chakula, Programu ya Elimu, Uwezeshaji na Uishi kwa Vijana (ELA) zote zikiwa na lengo kuu la kupunguza umaskini na kuwawezesha watu maskini.

Alisema wanafunzi kutoka Shule ya Kimataifa ya St' Con-stantine walitembelea tawi la Brac lililopo Sakina jijini hapa na ambako walijifunza elimu ya fedha. Alisema elimu kama hiyo itatolewa pia kwa Shule ya St' Joseph jijini Dar es Salaam.

Aidha, alisema waliwa-tembelea wakopaji ambapo waliwafundisha shughuli wanazofanya za kuwapunguzia umaskini.

Mwaka jana Brac ilihusika na kufanya shughuli kadhaa chini ya Microfinance, programu ndogo ya biashara na programu za elimu.

Kwa mujibu wa Meneja Mawasiliano wa Brac, Cesilia Bosco, utaratibu huo ume-fanyika ikiwa ni kuadhimi-sha mpango wa kila mwaka wa kampeni ya ufahamu wa kifedha (GMW) unaoongozwa na Shirika la Kimataifa la Wa-toto na Vijana linaloshughulika na Fedha (CYFI) na hufanyika mwezi Machi kila mwaka.

# Nyara za serikali zawatupa watatu lupango miaka 30

**Na Mwandishi Wetu, BABATI**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Babati, im-ewahukumu watu watatu kwenda jela miaka 30 baada ya kutiwa hatiani kwa uwindaji haramu na kukutwa na silaha haramu.

Akisoma hukumu hiyo jana Hakimu Neema Gabasile, alimhukumu mkazi wa Magugu wilayani hapa, Seleman Abdalah, kutumikia jela miaka 20.

Aidha, washtakiwa wengine, John Ju-manne na Samwel William, walihukumi-wa kwenda jela miaka mitano kila mmoja.

Katika usikilizaji wa kesi hiyo, mawakili wa serikali walidai kuwa Abdalah alikutwa na nyara za serikali, Novemba 20, mwaka 2017 kinyume cha sheria.

Pia walisema katika kesi hiyo namba 12/2017 Abdalah alikutwa na ngozi ya fisi, kucha ya simba, kwato ya pundamilia na mafuta ya simba.

Mtuhumiwa alikamatwa na askari wa wanyapori wa Tarangire akiwa na nyara hiyo kwenye Hifadhi ya Taifa ya Tarangire.

Waendesha mashtaka walimuomba hakimu atoe adhabu kubwa kwa mshtak-iwa ili iwe fundisho na hakimu akaamuru aende jela miaka 20.

Hakimu Neema aliamuru nyara hizo kurejeshwa serikalini kwa kuwa ni mali yake. Pia Hakimu Neema alimuhukumu John Jumanne na Samwel William kwen-da jela miaka mitano kila mmoja kwa kosa la kukutwa na bunduki iliyotengenezwa kienyeji aina ya gobore bila kibali.

Alisema washtakiwa hao walikamatwa na silaha hiyo inayodaiwa kutumika kwa uwindaji haramu, hivyo akatoa hukumu hiyo ili iwe funzo kwa wengine.

Aliamuru bunduki hiyo aina ya gobore kutaifishwa na kuwa mali ya serikali.



Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara, Ester Mahawe (CCM), akishiriki kujenga msingi wa madarasa mapya ya Shule ya Sekondari Kiru, wilayani Babati mkoani humo, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wauza pombe, baruti wapigwa marufuku Mirerani

**Na Mwandishi Wetu, ARUSHA**

OFISI ya Madini ya Mkoa wa Kimadini wa Simanjiro, imepiga marufuku uuzwaji wa pombe, vibanda vya kuuza baruti ndani ya ukuta unaozunguka migodi ya tanzanite.

Ofisa Madini wa mkoa huo, Daudi Ntal-ima, alipiga marufuku hiyo juzi, wakati akizungumza na wamiliki wa migodi pamoja na wanaapolo juu ya utaratibu mpya wa kuingia kwenye machimbo ya-nayozunguka ukuta huo.

Aidha, aliwaagiza wamiliki wote wa migodi iliyopo ndani ya ukuta huo kuzun-gushia uzio wa mabati kwenye migodi yao ndani ya miezi miwili kuanzia sasa pamo-ja na kambi wanazolala wachimbaji kuwa ndani ya uzio.

Alisema watakaoshindwa kutekeleza agizo hilo watafutiwa leseni zao za uchim-baji.

Alisema utaratibu huo mpya ulianza kutumika rasmi Aprili Mosi, mwaka huu, kwamba watu wasiokuwa na kazi maal-um hawataruhusiwa kuingia ndani ya eneo hilo lililozungushiwa ukuta.

Kuhusu machinga wasiokuwa na vi-tambulisho vya JPM, Ntalima alisema ni marufuku kuingiza kwenye eneo hilo na kwamba machinga wenye vitambulisho watafanya biashara zao maeneo mapya ya masoko yaliyotengwa kwa kupewa namba maalum ya kufanya biashara na siyo kuzunguka ovyo kwa kutembeza bid-haa zao maeneo ya migodi.

Alisema vibanda vya biashara na maka-zi yoyote nje ya uzio wa mgodi husika hayaruhusiwi tena na wenye vibanda, hivyo wanatakiwa kuwa na vitambulisho vya wamachinga vilivyotolewa na Rais.

Lakini alisema biashara zao wanatak-iwa kuzihamishia maeneo maalum yali-yotengwa kwa ajili ya soko na wasiokuwa na vitambulisho watatakiwa kuondoka eneo hilo mara moja.

"Kuanzia Aprili Mosi wafanyabiashara wote humu ndani ya ukuta huu lazima tuwatambua kwa kujua ni aina gani ya bi-ashara wanayoifanya ikiwa ni pamoja na kuwa na kitambulisho cha machinga na wale wote wanaofanya biashara ya kuuza aina zozote za pombe ikiwamo pombe haramu ya gonga na vibanda vya kuuza baruti hatutawaruhusu kuingia ndani ya ukuta huu," alisema.

"Watu wote ambao hawana kazi maal-um wanaorandaranda kwenye migodi na siyo wachimbaji pia hawaruhusiwi kuone-kana humu ndani, waondoke wakatafute kazi nyingine ya kufanya kabla hatujaan-za kuwachukulia hatua kali za kisheria," alisema.


Ntalima alitumia fursa hiyo kuwaonya watu wanaokata miti ovyo ndani ya mae-neo ya machimbo ya madini kuacha tabia hiyo mara moja na yeyote atakayetaka ku-kata mti ni lazima aeleze sababu za kuka-ta mti huo ili kama kuna umuhimu apewe kibali maalum.

Baadhi ya wananchi walipongeza hatua hiyo kutokana na wingi wa watu wasiokuwa na kazi maalum wakiwamo wauza pombe haramu ya gongo, dawa za kulevya kama bangi na mirungi ambayo inachangia kuharibu vijana wao kwa kuanza kutumia aina hizo za vilevi am-bavyo siyo salama.

Hassan Juma alisema hivi sasa kuna ongezeko kubwa la watu maeneo ya mi-godini, huku huduma za vyoo zikiwa ni changamoto kubwa hali ambayo inaweza kusababisha magonjwa ya mlipuko.

Alisema biashara nyingine ambazo haz-ina umuhimu wa ndani ya ukuta huo zi-napaswa kukomeshwa mara moja haswa machinga na wanawake wanaojiuza kwa wana apolo.

"Watu ni wengi migodini na huduma za vyoo hazikidhi mahitaji, lakini pia idadi ya wanawake wanaojiuza ni kubwa hivyo ni lazima udhibiti uwepo na vumbi la ulanga linatimka mno na tunahofia maradhi ya vifua," alisema.





# Serikali yaagiza wananchi wapewe ekari 100 za ardhi

**Na Godfrey Mushi, HAI**

SERIKALI imeagiza wananchi zaidi ya 200 kutoka Kijiji cha Foo, Wilaya ya Hai, kumegewa ardhi kiasi cha ekari 100 katika eneo ambalo wawekezaji wameshindwa kuliendeleza kwa miaka mitatu sasa.

Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, ametoa agizo hilo jana wakati akizungumza na wananchi wa Foo katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Machame.

"Mkurugenzi Mtendaji, Katibu Tawala wa Wilaya na Ofisa Ushirika na Mwenyekiti wa wakulima, naomba mkae mjadiliane kesho (leo) muone mnavyogawiaje ekari 100 katika eneo walilopewa watu wa EPK (wawekezaji waliopo katika Shamba la Lambo Estates)," alisema Ole Sabaya.

Aidha, katika mkutano huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Yohana Sintoo, alisema tatizo kubwa la mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira linatishia zaidi maeneo ya ukanda wa tambarare.

Amesema suala la kupanda miti milioni 1.5 katika ukanda huo ili kukabiliana na uharibifu huo sio la lelemama, isipokuwa watajifunga kibwebwe kila mwananchi kupanda walao miti 10.

Alisema tayari wananchi wa Kijiji cha Foo kilichopo Kata ya Machame Kaskazini uongozi wa wilaya hiyo umeshiriki zoezi la kupanda miti 3000.

"Hali ni mbaya sana katika ukanda wa tambarare wa Wilaya ya Hai na kama viongozi tumeliona hilo na tumeamua kuzunguka kuhamasisha wananchi kukabiliana na hali mbaya ya hali ya hewa," alisema Sintoo.



Kijana aliyejiajiri kwa kuokota chupa tupu za plastiki akijitahidi kuifikia chupa iliyokwama kwenye maji machafu ya Mto Ng'ombe, katika eneo la Mwananyamala Kwa Manjunju, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# DC atoa siku 7 kumsaka anayedaiwa kubaka

**Na Godfrey Mushi, HAI**

MKUU wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, ametoa siku saba kwa Jeshi la Polisi liwe limemtia mbaroni Makamu Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Sawe anayetuhumiwa kumtia mimba mwanafunzi wake wa kidato cha nne.

Alitoa agizo hilo jana, wakati akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Machame.

"OCD Z.A Zahoro (Mkuu wa Polisi wa Wilaya) nawapa tena siku saba kuanzia leo muwe mmemkamta huyo mwalimu na mnieletee taarifa ofisini kwangu kwamba mmemfungulia mashtaka ya ubakaji," alisema.

Kamanda wa Polisi mkoani humo, Kamishna Msaidizi, Hamisi Issah, amethibitisha kuwa jeshi hilo kwa sasa linamsaka mwalimu huyo kwa udi na uvumba, baada ya kudaiwa kutokomea kusikojulikana.

"Ni kweli hilo tukio limeripotiwa na tunamtafuta lakini siwezi kulizungumzia kwa sasa kwa sababu ya upelelezi," ameeleza Kamanda Issah.

Juzi, baada ya taarifa hizo kuzagaa, Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya hiyo, alisema kwa mwaka huu peke yake, mwanafunzi huyo ni kati ya wanafunzi watatu waliokatisha masomo yao kutokana na kupata ujauzito wakiwa shuleni.

"Jumla ya wanafunzi watatu katika Shule ya Sekondari ya Sawe, wamefukuzwa shule baada ya kugundulika kuwa ni wajawazito. Wanafunzi waliofukuzwa shule ni wa kidato cha pili, tatu na nne," amesema Ole Sabaya.

Kwa mujibu wa Ole Sabaya, baada ya polisi kupokea taarifa hizo za mwalimu huyo, Machi mosi mwaka huu, saa 10:00 jioni, walikwenda shuleni hapo na kukuta mwalimu huyo ameondoka na kwenda kusikojulikana na mpaka sasa hajulikani alipo.

Alipotafutwa Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Sawe, Emmanuel Mushi, kuzungumzia mdai hayo, alisema wanafunzi wa kike katika shule hiyo kupewa ujauzito, ni matendo yasiyokubalika na ni fedheha kubwa kwao na hivyo akatoa rai kwa vyombo vya dola kuongeza juhudi kuwasaka wote waliohusika.

Mkuu wa shule hiyo, Cecilia Kulawa, ameeleza kuwa makamu mkuu wa shule alitoweka tangu Machi mosi mwaka huu na kwamba mpaka sasa hawana taarifa zake mahali alipo.

Alisema wanafunzi watatu wa kidato cha pili, tatu na nne, waligundulika kuwa ni wajawazito Februari 28, mwaka huu na kusimamishwa kuendelea na masomo.

Kikao cha Bodi ya Shule hiyo kilichofanyika Machi 22, mwaka huu, kiliridhia kufukuzwa shule kwa wanafunzi hao.

# Same yaongoza kwa migogoro ya ardhi

**Na Godfrey Mushi, SAME**

MIGOGORO ya ndoa, ardhi na matunzo ya watoto inaongoza kusumbua wananchi wa Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, huku ikielezwa kuwa kuongezeka kwa mashauri hayo kunaonyesha jinsi wananchi wengi wanavyohitaji huduma ya msaada wa kisheria.

Ofisa utunzaji wa data na tathmini wa Shirika la Wasaidizi wa Kisheria la Wilaya hiyo, Hassan Seleman, alisema kanzi data ya SPO, inaonyesha kukua kwa uhitaji wa huduma za msaada wa kisheria na kwamba migogoro hiyo ni tatizo linalokuwa kwa haraka na limejitokeza katika maeneo mengi.

"Migogoro iliyokithiri sana kwenye wilaya yetu ya Same ni migogoro ya ardhi, ndoa na matunzo ya watoto, ambapo katika kipindi cha mwaka 2017/2018 tulipokea mashauri mengi zaidi. Mpaka sasa tunahaha kwenda kila kijiji kutoa huduma za kisheria hususani sheria ya ndoa, mirathi, matunzo ya watoto na ardhi," alisema.

Alisema baadhi ya wataalamu wa elimu ya jamii wamewashauri katika eneo hilo kwamba wanandoa wanaweza kutumia njia moja kuu ili kudhibiti migogoro isiwapeleke kuvunja ndoa zao, kuwa ni lazima kutambua hasira ni hisia au mihemko ya kawaida tu katika maisha.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, akizungumzia kazi inayofanywa na kada hiyo alieleza: "Hawa Wasaidizi wa Kisheria wanahitaji kujenga movement (harakati) ya para legal ambayo itaisaidia zaidi jamii kwa kiwango kikubwa kupaza sauti zao katika yale yanayowasumbua hasa migogoro ya ardhi, ndoa, ukatili wa kijinsia, mirathi na umiliki wa mali. Ni kweli Same inahitaji nguvu kuyakabili haya katika jamii."

Pamoja na hali hiyo, wasaidizi wa kisheria katika wilaya hiyo wamedai kuwa hadi sasa wameweza kuwapa faraja wanyonge na kufanikiwa kutimiza malengo ya utekelezaji wa mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (Mtakuwwa), hasa kutokana na kusaidia zaidi watu wasio na uwezo wa kumudu gharama za mawakili.

Kwa mujibu wa Sheria ya Huduma ya Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2017 na Kanuni zake za Mwaka 2018, ushauri wa msaada wa kisheria maana yake ni ushauri na msaada unaotolewa kwa mtu asiye na uwezo katika mashauri ya jinai na madai kuhusu sheria husika, taratibu za kisheria na uandaaji wa nyaraka za kisheria.

Kazi ya kuwanoa wasaidizi hao wa kisheria katika mkoa wa Kilimanjaro, imekuwa ikitekelezwa na Shirika la Kwieco kwa ufadhili wa Shirika la Legal Service Facility (LSF).

Ukurasa 18



MKUTANO WA KILIMANI ULIVYOSABABISHA VUTA NIKUVUTE KUHUSU HOJA TANGANYIKA

## MAKALA:

Kenyatta atamudu kuwasuluhisha 'mahasimu' Kagame na Museveni?



Ukurasa 14

## KIMATAIFA:



Rais Cyril Ramaphosa ashutumu mashambulizi dhidi ya wageni

Ukurasa 17

siasa

JUMATANO APRILI 3, 2019

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU



Wadau, CCM wahitimisha mjadala wa muhula urais

Ukurasa 19

# MAALIM SEIF AFUNGUKA:

## Si lazima nigombee urais

- Ushirikiano upinzani haukwepeki
- Wanaodai muosha huoshwa sijaosha mtu

**Na Mwandishi Wetu**

MAALIMU Seif Sharif Hamad, ambaye kwa miaka mingi ameweka historia ya kugombea urais wa Zanzibar mfululizo kuanzia mwaka 1995, safari hii anawaambia wanaomuunga mkono kuwa yuko ACT- Wazalendo kuendeleza harakati za upinzani, hivyo linapokuja suala la nani atagombea uongozi 2020 wanachama wataamua.

Akiwa Katibu Mkuu wa zamani wa CUF, Maalim Seif, anasema hayo katika mahojiano maalum na Nipashe jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, alipoulizwa iwapo anatarajia kuwania uongozi kwenye uchaguzi mkuu au atabaki

ENDELEA UK 16






Maalim Seif Sharif Hamad.

UCHAMBUZI

# Kenyatta atamudu kuwasuluhisha 'mahasimu' Kagame na Museveni?

Na Mashaka Mgeta

KWA hali ya uhusiano wa kidiplomasia uliopo kwa baadhi ya nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), ni sawa na kusema, bundi anaendelea kuunyemelea ushirikiano huo.

Mgogoro kati ya Uganda inayoongozwa na Yoweri Museveni na Rwanda iliyo chini ya Rais Paul Kagame, unaongeza wigo wenye kufifisha uhusiano katika nyanja tofauti hasa biashara.

Ikumbukwe kwamba mgogoro huo unatokea wakati Rwanda ikiwa inakabiliwa na mgogoro mwingine kati yake na Burundi.

Hivi sasa Rwanda kupitia Rais Kagame, ndio Mwenyekiti wa EAC yenye nchi wanachama sita ambao ni Tanzania, Kenya, Uganda, Burundi, Sudani Kusini na Rwanda yenyewe.

Wakati mgogoro kati ya Rwanda na Burundi ukionekana kama 'kupotezewa', mvutano mkubwa unaohusisha kauli za mafumbo za marais wa nchi mbili hizo unaelekea kuhatarisha zaidi ushirikiano na uhusiano wa kikanda uliopo kwa miongo kadhaa sasa.

Hivi karibuni, Uganda iliishutumu Serikali ya Rais Kagame kwa kuzuia malori ya mizigo na magari mengine kutoka nchini humo kuingia Rwanda, kufuatia hatua ya kuufunga mpaka wa Gatuna.

Pia Uganda 'ikainyooshea mkono' serikali hiyo kwa kuwazuia raia wake wasivuke mpaka kuingia nchini humo (Uganda) kwa sababu ya usalama wao.

Taarifa ya utawala wa Rwanda kuyazuia maroli na magari mengine kutoka Uganda kuingia chini humo ikatolewa na Msemaji wa Serikali ya Rais Museveni, Ofwono Opondo.

Kwa mujibu wa Opondo, maroli ya mizigo yanayofikia 129 kutoka Uganda yalikuwa 'yamekwama' kwenye mpaka wa Gatuna kwa wakati huo.

Hata hivyo, serikali ya Rais Kagame kupitia kwa Waziri wa Mambo ya Nje ya Nchi, Richard Sezibera, ilikanusha shutuma hizo na kufafanua kwamba magari hayo yalielekezwa kupitia mpaka wa Kagitumba ulioko Kaskazini mwa nchi hiyo ili kupisha ujenzi wa barabara yenye shughuli nyingi katika mpaka wa Gatuna.

"Walioitikia wito wa kupitia mpaka wa Kagitumba wameingia Rwanda na kuendelea na shughuli zao," akasema Sezibera.

Kwa upande mwingine, Mamlaka ya Mapato Rwanda (RRA) ilisema hatua hiyo iliyofikiwa kwenye mpaka wa Gatuna unaojulikana pia kama Katuna, ilikusudia kupisha ujenzi wa jengo la kituo kimoja cha mpakani.

Ikaelezwa kuwa barua iliyoandikwa na RRA kwenda kwa Kamishna wa Forodha wa Mamlaka ya Mapato Uganda (URA) ilifafanua kuhusu hatua ya kuyahamishia magari hayo kupita kwenye mpaka mwingine.

Barua hiyo iliyosainiwa na Kamishna wa Forodha wa RRA, Rosina Uwamariya ilisomeka, "Tumefikiria kwa makini kupunguza msongamano na foleni za malori ili kufanikisha ujenzi wa kituo hicho cha pamoja."

Pia Sezibera anasema zuio la raia wa Rwanda kuingia Uganda linatokana na kukamatwa kwao kwa kuhisiwa kuwa ni mashushushu wanaokwenda kufanya shughuli za upelelezi na kitendo cha kutopewa huduma muhimu walipokamatwa.



Rais Paul Kagame wa Rwanda (kushoto), akiwa na Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya. PICHA: MTANDAO

> "Kwa namna anavyofanya kazi huko Kenya, anaweza kutumia uzoefu huo na kuwashawishi kirahisi Rwanda na Uganda waondokane na tofauti walizonazo kwa maslahi ya wananchi wao na ukanda wa EAC,"

Sezibera akaongeza, "Si juu yetu (Rwanda) kulitatua hilo, bali lipo kwa upande wa Uganda. Kwa maana Waganda wanakaribishwa kwetu (Rwanda) na hatuna matatizo kwenye upande wa mpaka wetu."

Aidha, Msemaji wa Serikali ya Rais Museveni anakanusha madai ya kushikiliwa kwa raia wa Rwanda kutokana kwa tuhuma za ushushushu.

Badala yake anasema kama wapo Wanyarwanda kwenye magereza ya nchi hiyo watakuwa wanatokana na makosa yaliyoshughulikiwa kupitia Jeshi la Polisi na mfumo wa Mahakama nchini Uganda.

### KAULI ZAKUZA MGOGORO

Mgogoro umezidi kukua katika siku za karibuni hasa baada ya marais Museveni na Kagame kukaririwa wakitoa kauli zinazotafsiriwa kuwa ni mashambulizi kati yao.

Rais Museveni alikaririwa akiwaonya wenye kupanga njama za kuihujumu Uganda kwamba wanajua uwezo wa taifa hilo kuwa ni mkubwa na kwamba hawawezi wakaumudu.

Lakini Rais Kagame naye akakaririwa akisema amewasikia watu wanaotangaza kwamba hawataki kubughudhiwa na hivyo akawasihi nao wasiwabughudhi wenzao.

### KENYATTA

Katikati ya mzozo huo, ndipo Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya anapojitokeza kuwa msuluhishi wa mgogoro huo, hivyo kutoa tumaini jipya la kupatikana kwa suluhu kati ya nchi mbili hizo.

Francis Mgaya ni mfuatiliaji na mchambuzi wa masuala ya siasa katika EAC, anasema ushiriki wa Rais Kenyatta unaweza kuleta matumaini ikiwa marais Museveni na Kagame watakuwa tayari kuweka kando tofauti zao.

Mgaya anasema ingawa Rais Kenyatta hana historia ya kusuluhisha migogoro ya kidiplomasia, lakini zaidi akitoka katika taifa lenye historia ya mizozo kama hiyo na mingine ikimhusisha mwenyewe, bado ana nafasi kubwa ya kuzileta pamoja Rwanda na Uganda.

Kwa Mgaya, stadi alizozitumia kupunguza kiwango cha uhasama wa kisiasa hasa kati yake na kiongozi wa upinzani nchini Kenya, Raila Odinga, zinaweza kuwa nyenzo za kumsaidia kusuluhisha mgogoro huo.

"Ingawa hana historia ya usuluhishi, lakini namna alivyofanikiwa kuwaunganisha Wakenya hasa baada ya Mahakama ya Juu kutengua ushindi wake kabla ya kushinda tena katika uchaguzi wa marudio, kunaleta matumaini ya kupata mafanikio katika jukumu hilo," anasema.

Kiongozi mmoja wa masuala ya vijana katika Taasisi ya Okoa Kizazi Chako Tanzania (Sageta), Isdory Mkwama anasema ukiondoa mzozo uliopo kati ya Kenya na Uganda kuhusu kisiwa cha Migingo, Rais Kenyatta anaonekana kutokuwa na upande aliouegemea kati ya Rwanda na Uganda.

"Viongozi wanaozozana (Kagame na Museveni) ni waandamizi katika utawala wa nchi zao, wamewahi kuwa marafiki, wakakwaruzana pia kwa nyakati tofauti, lakini Kenyatta hajafikia kiwango chao hivyo ni rahisi akakubalika na kusikilizwa," anasema Mkwama.

Kiongozi mmoja wa kisiasa nchini ambaye hataki jina lake kuandikwa gazetini anasema, Rais Kenyatta amejijengea heshima katika utatuzi wa migogoro nchini mwake na kujielekeza katika ujenzi wa miradi na maendeleo, biashara na kukuza uchumi kwa kuwashirikisha raia wake.

"Kwa namna anavyofanya kazi huko Kenya, anaweza kutumia uzoefu huo na kuwashawishi kirahisi Rwanda na Uganda waondokane na tofauti walizonazo kwa maslahi ya wananchi wao na ukanda wa EAC," anasema.

### AKUTANA NA MUSEVENI, KAGAME


Tayari Rais Kenyatta ameshafanya ziara jijini Kigali, Rwanda na kuzungumza na Rais Kagame ikiwa ni moja ya jitihada za kuupatia suluhu mgogoro huo.

Wakati akiondoka nchini humo, Rais Kenyatta alipitia Uganda na kufanya mazungumzo na Rais Museveni kwenye Ikulu ya Entebbe.

Akiwa nchini Rwanda, Rais Kenyatta alikaribishwa na mwenyeji wake, Rais Kagame kuhutubia mkutano wa viongozi uliofanyika Gabiro na kusisitiza umuhimu wa ushirikiano wa kikanda.

"Tunakabiliwa na changamoto tukiwa nchi majirani na wanachama wa umoja wa kikanda. Lakini kutokana na dhamira na nia njema, tutapata suluhu

Inaendelea Uk.15



Rais Yoweri Museveni wa Uganda (kushoto), akiwa na Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya. **PICHA: MTANDAO**

# Kenyatta atamudu kuwasuluhisha 'mahasimu'

**Inatoka Uk.14**

ya mgogoro huu," Rais Kenyatta alisema alipozungumza jijini Kigali.

Akihutubia kwenye mkutano wa viongozi wa Rwanda huko Gabiro, Rais Kenyatta alisema uhusiano wa nchi yake na Rwanda upo katika kiwango cha juu na akaongeza:

"Mara nyingi tunapokutana ndivyo tunavyoingiliana mara nyingi na tunawafungamanisha watu wetu."

Akahimiza kuwapo ushirikiano mkubwa kati ya wananchi wa nchi mbili hizo.

"Serikali zote mbili zimefanikiwa katika hilo kwa kiwango kikubwa... tumerahisisha wananchi wetu na bidhaa kuvuka mipaka yetu... tumeunganishwa na mtandao wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) na katika maeneo mengine," alisema Rais Kenyatta.

Hata hivyo, Rais Kenyatta akaeleza kutambua tofauti zilizopo kwa baadhi ya viongozi wa nchi wanachama wa EAC na kuwasihi kuzipatia suluhu.

**KAGAME AMUITA KAKA**

Naye Rais Kagame anamtambulisha Rais Kenyetta kama kaka na rafiki yake, akisema kuna uwezekano wa mtu kuwa na kaka asiye rafiki yake.

Na wakiwa jijini Entebbe, Uganda, marais Museveni na Kenyatta wakazungumzia masuala ya utengamano wa EAC, kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ikulu ya Entebbe.

**EAC NAYO YAINGILIA KATI**

Baada ya kuibuka mgogoro huo, EAC ilituma ujumbe kwenda Rwanda na Uganda kubaini chanzo chake.

> "Tumekwenda kwa nyakati tofauti kwa wakuu wa nchi wa Rwanda na Uganda kwa ajili ya kuwajulisha nia yetu ya kuwasuluhisha,"

Katibu Mkuu wa Sekretarieti ya EAC, Liberat Mfumukeko, akaahidi kuyahusisha mataifa hayo katika jitihada za kutafuta suluhu ya mgogoro huo uliodhoofisha biashara kwenye eneo la mpaka wa nchi hizo.

"Wataalamu wetu wapo Rwanda na Uganda katika jitihada za kuutafuta ukweli na tutatoa ripoti itakayotuwezesha kuyahusisha mataifa hayo... Siwezi kusema itafanyika kwa muda gani, lakini itakuwa ndani ya siku chache zijazo," Mfumukeko anakaririwa Machi 19, mwaka huu baada ya kuhojiwa na gazeti la The East African jijini Nairobi, Kenya akisema.

Mfumukeko akalaumu kuibuka kwa mgogoro huo uliosababisha, pamoja na mambo mengine, kuanguka kwa ushirikiano wa kibiashara katika ukanda wa EAC.

Kwa mujibu wa Mfumukeko, pande mbili hizo zinapaswa kupata suluhu vinginevyo, kama usafirishwaji wa bidhaa utakwama (mpakani mwa nchi hizo), basi biashara zitayumba.

"Wajibu wetu ni kuhakikisha nchi zinatekeleza ahadi zao... kwa mfano nchi wanachama zimesaini Itifaki ya Soko la Pamoja na Umoja wa Forodha. Tunawakumbusha kwamba bidhaa zinapozuiwa wanakuwa wamevunja itifaki hizo,"anasema Mfumukeko.

**ATHARI ZA KIBIASHARA**

Tofauti zinazojitokeza kati ya nchi wanachama wa EAC, zinaathiri mtengamano unaohusisha muingiliano wa kibiashara.

Mwenyekiti wa Baraza la Biashara za Afrika Mashariki (EABC), Nick Nesbitt, amekaririwa akisema, kunapotokea mgogoro kwenye eneo la mpaka mmoja, hali hiyo inawaathiri wanapokuwa kwenye mipaka mingine.

"Tunahitaji kujua nini kinachotokea na masuala ya kisiasa yanayohusika... EABC inataka mgogoro huo upatiwe ufumbuzi kwa maslahi ya kulinda mkataba ulioanzisha EAC pamoja na itifaki ya soko la pamoja ya jumuiya hiyo vinavyotoa fursa ya usafirishaji huru wa bidhaa, watu na huduma," akasema.

Hatua ya kuondokana na migogoro inachochea kuwapo sera rafiki zinazochagiza kasi ya ukuaji wa biashara kwenye ukanda huo.

**ZIARA YA KAGAME TANZANIA**

Kabla ya ziara ya Rais Kenyatta nchini Rwanda, Rais Kagame alifika jijini Dar es Salaam katika ziara ya siku mbili ambapo pia alifanya mazungumzo na Rais John Magufuli.

Ziara ya Rais Kagame ilitafsiriwa kama sehemu ya jitihada za Rwanda kutafuta fursa ya kupitishia bidhaa zake kwenye bandari ya Dar es Salaam.

Rwanda ambayo ni nchi ndogo isiyokuwa ama kuzungukwa na bahari, inatumia bandari za Dar es Salaam na Mombasa.

Hata hivyo, bidhaa zinazopitia Mombasa zinasafirishwa kupitia nchini Uganda kabla ya kuingizwa Rwanda.

Takwimu zinaonyesha kuwa takribani asilimia 80 ya bidhaa za Rwanda zinaingizwa kupitia bandari ya Dar es Salaam, lakini sehemu kubwa ya bidhaa inayosafirishwa nje kama madini, chai na kahawa vinapitia Uganda hadi bandari ya Mombasa.

Ni dhahiri kwamba kushamiri kwa mgogoro huo kunaibua hisia za kuwapo uwezekano wa kufutwa kwa njia ya Uganda hivyo kuiathiri Kenya inayotumia bandari ya Mombasa kusafirisha bidhaa za Rwanda.

**TAASISI ZA KIJAMII**

Mgogoro huo haujawagusa wanasiasa tu, bali pia taasisi mbalimbali za kijamii ikiwa ni pamoja na Chama cha Wanasheria wa Afrika Mashariki walioonyesha nia ya kuzisuluhisha Uganda na Rwanda.

Gazeti la Monitor la nchini Uganda liliandika kuwa EALS ilijitolea kuwatafuta wanadiplomasia wakongwe, wanasheria waandamizi, asasi za kijamii zenye ushawishi na wawakilishi wa jumuiya za wafanyabiashara kuunda jopo la watakaoshiriki kuleta suluhu hiyo.

"Tumekwenda kwa nyakati tofauti kwa wakuu wa nchi wa Rwanda na Uganda kwa ajili ya kuwajulisha nia yetu ya kuwasuluhisha," anasema Rais wa EALS, Willy Rubeya na kukaririwa na gazeti hilo kutokea jijini Arusha.

**Makala haya yameandikwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali. Mwandishi anapatikana kupitia simu namba 0754691540 ama barua pepe:mgeta2000@yahoo.com**

MAKALA

Inatoka Uk.13

# Si lazima nigombee urais

kukijenga chama.

"Si lazima Maalim Seif agombee. Yeyote anayepewa ridhaa na wanachama atagombea iwe urais wa Zanzibar, Tanzania Bara na nyinginezo. Lakini niseme mipango ya kugombea kwenye uchaguzi mkuu ipo, kubwa zaidi wanachama wataamua. Ni suala la siku zijazo na liko mikononi mwa wanachama... nia ni kuwaletea Watanzania maendeleo." anasema.

**UKAWA**

Anapoulizwa juu ya hatma ya umoja wa upinzani unaoundwa na ushirikiano wa Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa) na iwapo ACT-Wazalendo ina mpango wa kujiunga, Maalim Seif, anajibu:

"Ni lazima kuendeleza ushirikiano wa vyama vya upinzani...hili halikwepeki ili kutimiza kazi zetu na kufikia lengo... ni lazima kuunganisha nguvu."

Anasema hata kama hawatatumia jina la Ukawa kwenye jukwaa la ushirikiano, lakini wana nia ya dhati na watаunda ushirika kwani haiwezekani kwenda mbele bila ushirika wa vyama.

Anasema kuwa umuhimu umeanza kuonekana wakati huu wa kujadiliana athari za sheria mpya ya vyama vya siasa ambayo inawafanya wapinzani kuwa makini zaidi, kuamka na kushirikiana kikamilifu.

Maalim Seif, anasema hadi sasa ushirika upo na kwamba vyama nane kati ya 10 viko pamoja na kuongeza kuwa ADC cha Hamad Rashid na CUF vimejiweka pembeni, lakini wapinzani wengine watashirikiana na kujiimarisha kwenye uchaguzi mkuu mwakani na katika mikakati ya maendeleo.

**HUJUMA Vs CUF**

Maalim Seif akijibu swali kuhusu malalamiko ya mali za CUF, mfano bendera na kadi kuchomwa na hata ofisi kubadilishwa rangi na mali kumilikishwa ACT-Wazalendo, anasema ni jambo linalokuzwa na si kweli kwa jinsi ambavyo linatangazwa.

"Kwa hili nasema kwamba kuna agenda nyingine... naomba iwekwe wazi, ifahamike," anabainisha.

Kiongozi huyo anafafanua kuwa inawezekana wapo wanaochoma bendera, lakini ni binadamu wenye hasira.

"Labda si wanachama wa CUF wala si ACT-Wazalendo, ni wavurugaji. Hivyo ni jukumu la polisi kuwasaka watuhumiwa na kuwafikisha mahakamani na si kukiadhibu chama," anasema.

Anafafamua kuwa ni kama wahalifu wengine.

"Mfano mwanafunzi ameharibu mazao yaliyoko jirani na shule, haiwezekani kuiadhibu shule nzima... anasakwa mhalifu na kuchukuliwa hatua... hilo ndilo polisi wanalotakiwa kulifanya sasa," anasema na kuongeza:

"La pili niseme, kuna waliokuwa wanachama wa CUF, ambao walitoa mali zao kama nyumba na vifaa wakaiazima CUF ichore nembo na kuweka bendera zake, sasa hawaitaki tena CUF."

> "Leo chuki zipo zinatokana na mfumo, kwa mfano vijana wanadai hawapati kazi wala fursa za kuendelea na masomo ya elimu ya juu kama si wanachama wa CCM. Kuna fomu maalumu unajaza na eneo mojawapo unaulizwa kuhusu chama chako. Ukijitetea kuwa huna chama unaulizwa vipi familia yako ni wanachama wa chama gani?"




Maalim Seif Sharif Hamad (kushoto), akiwa na Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi.

Anasema nyumba ni mali zao na haiwezekani kuwa na mali za chama kingine kwa vile wameshageuka na kuwa wanachama wa ACT-Wazalendo.

"Hivyo hawawezi kubaki na alama za chama wasichokitumikia... isitoshe hizo ni mali zao, chama hakimiliki ni mapenzi yao kwa chama," anafafanua.

Anasisitiza, watuhumiwa binafsi wasakwe na si chama kwani hakihusiki.

"Kama ni suala la kushusha na kuchoma bendera anayehusika ashtakiwe na adhabu yake inafahamika miezi sita gerezani au faini ya Sh. 1, 000,000," anasema.

Anamtaka Msajili wa Vyama, kuwabaini watuhumiwa na kukiarifu chama kuwa wanachama kadhaa wameharibu mali za CUF, kwa sababu ana uwezo wa kuwafutia uanachama na kuwachukulia hatua badala ya kukitisha chama.

**TAKBIR**

Akijibu kuhusu onyo la kutumia vionjo vya dini kwenye mikusanyiko ya ACT-Wazalendo kwa mfano Takbir, anaishauri Ofisi ya Msajili kuangalia zaidi kuhusu masuala ya salamu za kidini kwenye jamii, kwani Watanzania wana imani zao na wanazitumia kusalimiana, hivyo ni jambo linaloweza kuleta changamoto sana kwa vile Takbir ni sawa na Wakristo kusema Bwana Yesu asifiwe, Tumsifu Yesu Kristo. Na Takbir ni Mungu Mkuu si kitu kigeni.

Anasema kwa Wazanzibari ambao asilimia zaidi ya 90 ni Waisalamu, hutumia salamu hiyo.

"Zanzibar shughuli zote zinaanzishwa kwa jina la Mwenyezi Mungu, harusi, misiba, dua na hata serikalini. Kila jambo linaanzia kwa dua. Leo wanachama wa ACT-Wazalendo kusema Mungu Mkuu inakuwa shida?" anahoji na kuongeza kuwa wataendelea kumtukuza na kumshukuru Mungu.

Anataja mikusanyiko ya kiserikali kuwa ina maombi na viongozi wa kidini wanashirikishwa kumsifu na kumuomba Mungu.

Hata hivyo anashauri kuwa iwapo salamu hizo zinaonekana kuibua mijadala ni vyema kukawa na orodha ya mambo ya maadili ya kitaifa ili kuchambua na kukubaliana yanayokubalika na yasiyotakikana ikiwamo kutumia salamu za kidini.

**MUUNGANO**

Anapoulizwa iwapo kabla ya kujiunga na ACT-Wazalendo walijadiliana kuhusu Muungano kwa vile CUF ilikuwa na msimamo wa Muungano wa Mkataba, wakati chama alichojiunga nacho kinasimamia muundo wa serikali tatu-ya Muungano, ya Tanganyika na ya Zanzibar, Maalim Seif, anasema suala la Muungano halijajadiliwa kwani CUF ilikuwa na msimamo wa serikali tatu tangu mwanzo.

"Msimamo wa CUF ni serikali tatu, muungano wa mkataba ni maoni na mapendekezo yangu binafsi si ya chama... Mimi ndiye niliyependekeza..." anasema mwanasiasa huyo ambaye aliwahi kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar (SUKI) iliyowaleta pamoja CCM na CUF kuongoza serikali kwa kipindi cha miaka mitano hadi 2015.

Anaongeza: "Wakati wa kukusanya maoni ya wananchi kuunda rasimu, Tume ya Warioba ilifika Zanzibar na kukusanya maoni. Wapo waliokuwa na msimamo wa serikali moja, kuna waliotaka mfumo wa sasa wa serikali mbili uendelee, wapo wa serikali ya shirikisho na wengine kama mimi waliotaka mkataba. Lakini Tume, ilileta mapendekezo ya kuwa na serikali tatu. CUF ilikubali na tangu mwanzo ilikuwa na nia ya kuwa na muundo huo."

**KILIO CHA PEMBA**

Mara kadhaa Wana CUF walidai Wapemba hawashirikishwi kwenye uongozi na kuachwa nyuma kimaendeleo ikilinganishwa na Unguja, je, hali ikoje leo?

Ni swali jingine analoulizwa, akijibu, Maalim Seif anasema wakati akiwa SUKI kulikuwa na mafanikio mengi, mojawapo ni kuinua hali za wakulima wa karafuu ambao wengi wako Pemba.

Anasema SUKI iliongeza bei kutoka Sh. 2,500 hadi 15,000 kwa kilo. Yote hayo yalibadilisha mno maisha ya Wapemba.

Aidha, anasema CUF iliishawishi serikali kubadili na kuimarisha baadhi ya mambo ambayo yameleta tija kwa Wazanzibari kwani pamoja na kwamba SUKI ilikuwa na upinzani na CCM hakukuwa na ubaguzi wala itikadi za kichama.

Anasema matokeo yake waliondoa uhasama, ubaguzi na chuki, yote hayo yaliakisiwa kwenye jamii ambayo ilianza tena kushirikiana hasa kisiwani Pemba.

"Leo chuki zipo zinatokana na mfumo, kwa mfano vijana wanadai hawapati kazi wala fursa za kuendelea na masomo ya elimu ya juu kama si wanachama wa CCM. Kuna fomu maalumu unajaza na eneo mojawapo unaulizwa kuhusu chama chako. Ukijitetea kuwa huna chama unaulizwa vipi familia yako ni wanachama wa chama gani?" anasema na kuongeza:

"Hayo yanaongeza mpasuko na kuzidisha uhasama."

Anasema kuwa ndani ya SUKI, CUF iliongoza wizara saba, kati ya hizo nyeti zilikuwa nne- afya, utalii, mawasiliano na biashara.

"CCM ilikuwa na wizara 11 na kila kitu kilifanywa kwa umoja na ushirikiano ulioleta mabadiliko makubwa kwa Wazanzibari, lakini mgogoro ulioondoa SUKI madarakani umesababisha kurudisha nyuma juhudi hizo," anasema.

**KUFURAHIA KUJIONDOA**

Maalim Seif anapoulizwa kujibu madai ya mahasimu wake akiwamo Hamad Rashid, anayedaiwa kumwondoa CUF, anajibu akijitetea kuwa kama Katibu Mkuu hakufukuza mtu, bali ni maamuzi ya wanachama.

Anakumbusha kuwa Mwenyekiti mwanzilishi James Mapalala alisusia mkutano mkuu ambao Msajili wa Vyama Jaji George Liundi (marehemu), alishuhudia, alidai hakutoa udhuru wala kujali kikao hicho ambacho wanachama waliridhia kumuondoa.

"Hamad Rashid, alichukuliwa hatua na Baraza Kuu la Chama, lililojiridhisha kuwa anaelekea kuleta mgogoro ndani ya CUF, hivyo likamfukuza si Maalim Seif. Vikao vya chama uwe mkutano mkuu, baraza kuu, halmashauri kuu vinaongozwa na mwenyekiti au makamu wake kama hawapo kikao kinamchagua mwenyekiti mwingine na si Katibu Mkuu wala mjumbe wa sekretarieti, kwa hiyo nasema mimi sijaosha mtu, chama ndicho kiliwaosha wanachama hao," anasema.



Rais Cyril Ramaphosa wa Afrika Kusini. **PICHA: MTANDAO**

## Rais Cyril Ramaphosa ashutumu mashambulizi dhidi ya wageni

RAIS wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, ameshtumu ghasia za mashambulizi dhidi ya wageni yanayofanywa na raia wake na kutoa wito kwa taasisi za kiusalama kuwakamata wanaotekeleza vitendo hivyo.

Amesema kuwa ghasia hizo, ambazo zimekuwa zikiwalenga raia wa Malawi na raia wengine wa Afrika katika jimbo la Kwazulu Natal, ni suala la kujutia hususan katika mkesha wa siku ya mwezi wa uhuru ambapo taifa hilo linaadhimisha miaka 25 tangu uchaguzi wa kidemokrasia nchini humo.

Wiki iliyopita, raia wengi kutoka nje ya nchi hiyo walilazimika kutoka katika nyumba zao baada ya waandamanaji waliojawa na hasira kuwashambulia na kufanya wizi kwenye maduka wanayoyamiliki.

"Leo uchumi wetu na faida za jamii yetu zinatokana na biashara na uwekezaji kutoka kwa washirika wetu katika bara la Afrika na wengi wanaishi hapa nchini Afrika Kusini, ambapo wanachangia pakubwa maendeleo ya taifa hili," anasema na kuongeza:

"Maendeleo ya Afrika yanatokana na ongezeko la watu na mizigo kutoka eneo moja hadi jingine kati ya mataifa tofauti ili sote tuweze kufaidika...hatutakubali kuwaacha wahalifu kurudisha nyuma hatua zilizopigwa."

Kwa mujibu wa Egbert Mkoko ambaye ni raia wa Tanzania anayeishi katika jimbo la kwazulu Natal, hali si shwari hususan miongoni mwa raia wa Zimbabwe, Malawi na Ethiopia ambao ndio wengi wanaotafuta maisha katika eneo hilo.

Mkoko anasema kuwa kuna baadhi ya watu wanaodaiwa kuuawa katika eneo hilo.

"Vurugu zilizotokea hapo awali zimeibuka tena na chanzo ni kwamba raia wa kigeni wanaoishi nchini humo wanadaiwa kuchukua kazi za raia wa taifa hilo," anabainisha.

Anasema kuwa bado hakuna suluhu yoyote iliyotolewa na serikali, hatua ambayo imewafanya raia wengi wa kigeni kuamua kusalia majumbani.

Anaongeza kuwa hali ni ngumu kwa raia wengi wa kigeni kwa kuwa wanaishi pamoja na raia wa kipato cha chini.

Mkoko anasema kuwa katika kipindi cha siku mbili zilizopita, raia wengi wa kigeni walijaa katika vituo vingi vya polisi katika mji wa Durban.

**WAATHIRIWA**

Takriban watu 100 walishambulia maduka ya vyakula siku ya Jumapili usiku na Jumatatu alfajiri, wakiiba na kuchoma majumba.

Mwanamke mmoja alifariki wakati alipoanguka kutoka kwenye paa la nyumba wakati alipokuwa akiwatoroka waandamanaji hao.

Watu wengine wawili waliuawa kutokana na majeraha ya risasi, baada ya mwenye duka moja kudaiwa kuwapiga risasi.

Juzi, wageni walianza kutafuta hifadhi katika misikiti na vituo vya polisi.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Lindiwe Sisulu, aliwaagiza maofisa wa polisi kuwakabili watu wanaowashambulia wageni.

"Vitendo vyovyote vya kihuni pamoja na wizi wa mali ya raia wa kigeni havitakubalika na maofisa wa polisi na taasisi za kiusalama zinafaa kuchukua hatua za dharura bila kupendelea upande wowote," alisema katika taarifa.

Baadhi ya watu wamekuwa wakiwalalamikia wageni wanaofanya kazi nchini humo ambapo ukosefu wa ajira uko juu ukiwa asilimia 72 mwisho wa mwaka uliopita.

Mwaka 2015, ghasia katika miji ya Johannesburg na Durban zilisababisha mauaji ya watu saba, baada ya wahamiaji kuwindwa na kushambuliwa na magenge.

Afrika Kusini ilikumbwa na ghasia mbaya zaidi dhidi ya wageni mwaka 2008 ambapo zaidi ya watu 60 waliuawa. **BBC**

# Mkutano wa Kilimani ulivyosababisha vuta nikuvute kuhusu hoja Tanganyika

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kundi la wabunge 55 maarufu kama G55 kuwasilisha hoja ya kutaka kuundwa kwa serikali ya Tanganyika na hatimaye Bunge kupitisha azimio, mwasisi wa taifa la Tanzania na baadaye Tanzania, Mwalimu Julius Nyarere, aliingilia kati kutaka jambo hilo lisiendelee kujadiliwa na hatimaye kutekelezwa.

Katika kutimiza azma hiyo, Nyerere alitumia vikao halali vya CCM ikiwamo Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) kwa kuitisha mkutano uliofanyika kweye ukumbi wa Kilimani, Dodoma.

Licha ya kwamba mkutano huo wa NEC mwenyekiti wake alikuwa Rais Ali Hassan Mwinyi ambaye alikuwa pia Mwenyekiti wa Taifa wa CCM, mzungumzaji mkuu alikuwa Nyerere ambaye alitumia muda mrefu kupinga azimio la bunge la kuanzishwa kwa Tanganyika.

Katika hotuba yake hiyo, aliyekuwa Mbunge wa Chunya na Mratibu wa G55 aliyewasilisha hoja hiyo, Njelu Kasaka, anasema Nyerere alidai kuwa azimio la bunge kuhusu Tanganyika lilifikiwa kutokana na chuki dhidi ya Waislamu hasa Wazanzibari.

Sambamba na hilo, Kasaka anasema Nyerere pia alimlaumu aliyekuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais, John Malecela, kwa kushindwa kuishauri vyema serikali na pia kutozuia hoja hiyo akiwa kiongozi wa shughuli za serikali bungeni.

Akisimulia katika kitabu chake cha 'Njelu Kasaka- Maisha, Siasa na Hoja ya Tanganyika', mwanasiasa huyo anasema wabunge walishangazwa na kauli ya Nyerere kwa sababu hakukuwa na ajenda yoyote ya siri wala ubaguzi wa kidini.

"Walimu Nyerere alileta hoja ile juu ya ubaguzi na udini kwa lengo la kungwa mkono na Wazanzibari kwa upande mmoja na Waislamu kwa upande wa pili... Wajumbe wa G55 walitoka dini zote, yaani Wakristo na Waislamu na wabunge katika mkutano wa Kilimani walielewa hivyo," anasema Kasaka.

Kwa mujibu wa Kasaka, baada ya hotuba ya Mwalimu Nyerere, Rais (mstaafu) Mwinyi aliahirisha mkutano na kuwataka wajumbe kupata muda wa kutafakari hotuba ya Mwalimu na pia kuisoma hotuba ya aliyekuwa Katibu Mkuu wa CCM, Horace Kolimba.

**KAWAWA ATIBUA MAMBO**

Baada ya kuahirishwa kwa mkutano siku ya kwanza, mkutano huo uliendelea siku ya pili kwa aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM na mwanasiasa mkongwe, Mzee Rashidi Kawawa kutoa hotuba. Ambayo pamoja na mambo mengine ilieleza kuwa wabunge wamekiuka sera ya CCM kwa kuwasilisha hoja hiyo ya Tanganyika.

Katika hotuba hiyo, Kawawa alisema Nyerere alikuwa amemaliza mambo hivyo mkutano huo ulipaswa kufungwa huku akisisitiza kuwa mbunge aliyekuwa hakubaliani na hilo, arudishe kadi ya CCM kwa hiari na asipofanya hivyo atafukuzwa uanachama.

Kasaka anasema Kawawa alitoa hotuba hiyo bila kujua hali halisi ilivyokuwa ndani ya mkutano huo kwani hakutarajia kilichotokea baada ya kutoa hiyo.

"Hotuba ya Mwalimu Nyerere haikuwafurahisha wabunge wengi na hata baadhi ya wajumbe wa mkutano na kusema kweli iliimarisha msimamo wao wa kutetea azimio la bunge. Baadhi ya wajumbe waliteta na mimi nje ya mkutano kuonyesha kuwa walikuwa hawakubaliani na mtazamo wa Mwalimu Nyerere.

> Baada ya mkutano wa Kilimani, CCM iliendesha kura ya maoni ndani ya chama ili kupata maoni ya wanachama kuhusu azimio la bunge la kuanzishwa kwa serikali ya Tanganyika. Hatua hiyo, Kasaka anasema kwa kuzingatia upinzani wa azimio hilo kutoka kwa Nyerere, G55 walitabiri matokeo ambavyo yangekuwa.

"Hata wabunge waliopata kuzungumza katika mkutano huo, walisisitiza utekelezaji wa azimio la bunge. Hali ya upinzani ilijitokeza pale Mwenyekiti, Rais Mwinyi, alipoelekeza kwamba mkutano ujadili hotuba ya Nyerere ambayo imeonyesha kuwa bunge lilikuwa limekiuka mipaka yake kwa kukubali sera ya serikali mbili bila kibali cha chama-CCM," anasema Kasaka.

Kutokana na kauli hiyo ya Mwinyi, Kasaka anasema alinyoosha mkono kutaka kuungumza na kupewa nafasi na kuweka bayana kwa kumwambia Mwenyekiti (Mwinyi) kwamba alikuwa anayumbisha mkutano na kuwaondoa wajumbe kutoka katika suala lililowaleta na kutaka wajadili jambo tofauti.

Anazidi kubainisha kuwa alimweleza Mwenyekiti kwamba kama anataka kujadili hotuba ya Nyerere wakubaliane kuwa uongozi wa CCM ni dhaifu na kwamba Waziri Mkuu Malecela na Kolimba wameshindwa kumpa ushauri mzuri kuhusu hoja ya Tanganyika.

"Pia nilisema ili kujiepusha na uwezekano wa mkutano kujiingiza kwenye mambo yasiyohusika ni vyema tukazingatia ajenda za mkutano. Pia nilikataa pendekezo la Kawawa kwamba wabunge wasiokubaliana na msimamo wa Mwalimu Nyerere wajitoe CCM," anasema.

Baada ya kusema hayo, Kasaka anasema Mwinyi alimkatisha na kusema aanze kujadili hoja ya mkutano jambo ambalo anasema lilimfurahisha kuona kwamba Mwenyekiti huyo alikubaliana naye kutoifanya hotuba ya Nyerere kuwa moja ya ajenda kuu za mkutano.

Kwa mantiki hiyo, kwa mujibu wa Kasaka, hotuba ya Nyerere ambayo ingewagawa wajumbe kutokana na kusisitiza kuwa kulikuwa kumepandikizwa chuki na ubaguzi wa kidini, iliwekwa kando na haikujadiliwa kabisa.

Wajumbe kadhaa walipewa nafasi ya kuzungumza huku baadhi wakidai kuwa Nyerere alikuwa na hoja kuhusu azimio la bunge la kuundwa kwa serikali ya Tanganyika lakini hawakulikataa azimio hilo.

Hata hivyo, Kasaka anasema wabunge Edward Ayila (Rorya) na Mussa Nkhangaa (Singida Mjini), walikataa katakata kuhusisha Uislamu na azimio la bunge kwa kuweka msimamo kuwa hakuna wakati wowote suala la udini lilijadiliwa kupitia azimio la bunge.

"Abel Mwanga (Musoma Mjini) akirejea tishio la Kawawa kwamba wabunge wa G55 warejeshe kadi za CCM kama hawakubaliani na msimamo wa Nyerere, alimtaka yeyote aliyefikiria kwamba yeye ni CCM asimame mbele ya mkutano ili wabunge wa G55 wamkabidhi kadi. Hakuna aliyejitokeza," anasema.

**AZIMIO LAFUTWA**

Baada ya mkutano wa Kilimani, iliundwa kamati ya wawakilishi wa G55 na NEC kwa ajili ya kuandaa makubaliano ya mkutano huo. G55 iliwakilishwa na Kasaka, Mateo Qaresi, Mussa Nkhangaa, Arcado Ntagazwa na Kasaka.

Kimsingi, Kasaka anasema mkutano ulikubaliana CCM iendeshe kura ya maoni kubaini kama wanachama wake walikuwa tayari kuachana na sera ya serikali mbili, hivyo kutoa mwanya wa kuundwa kwa serikali ya Tanganyika na kwamba baada ya kukamilika, ndipo azimio la bunge litekelezwe.

Kuwapo kwa maridhiano hayo yaliyotokana na mkutano wa Kilimani, Kasaka anasema: "Kwa makubaliano hayo, nilielewa wazi kwamba huo ulikuwa ndio mwisho wa azimio la bunge."

Baada ya mkutano wa Kilimani, CCM iliendesha kura ya maoni ndani ya chama ili kupata maoni ya wanachama kuhusu azimio la bunge la kuanzishwa kwa serikali ya Tanganyika. Hatua hiyo, Kasaka anasema kwa kuzingatia upinzani wa azimio hilo kutoka kwa Nyerere, G55 walitabiri matokeo ambavyo yangekuwa.

Hatimaye Agosti, 1994 viongozi wa CCM walitoa matokeo kuhusu kura hiyo ya maoni ambayo ilionyesha wana CCM Tanzania Bara, asilimia 31.17 walitaka serikali moja, asilimia 57.72 serikali mbili na asilimia 8.91 walitaka serikali tatu.

Kwa upande wa Zanzibar, asilimia 0.52 walitaka serikali moja, asilimia 98.78 serikali mbili na asilimia 0.45 serikali tatu. Kwa mantki hiyo, asilimia kubwa ya wana CCM wa pande zote walitaka serikali mbili.

Kutokana na matokeo hayo, kabla ya mwisho wa bunge la bajeti la 1994/95, Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Samuel Sitta, aliwasilisha bungeni hoja ya kutaka bunge kulifuta azimio la bunge la mwaka 1993 lililokuwa na lengo la kuanzishwa kwa serikali ya Tanganyika.

Hata hivyo, kundi la G55 ambalo wakati huo lilikuwa limekimbiwa na wabunge wengi, lilisimama kidete kupinga hoja hiyo lakini lilizidiwa na hatimaye azimio hilo likafutwa kwa njia ya kura.

Haya ni mambo machache yanayoeleza mchakato mzima juu ya hoja ya Tanganyika. Undani kamili umo ndani ya kitabu hicho ambacho kimesheheni mambo mbalimbali yakiwamo mafunzo kwa viongozi. Mwendelezo zaidi wiki ijayo.



Njelu Kasaka

# Wadau, CCM wahitimisha mjadala wa muhula urais

Na Sabato Kasika

'IWAPO taifa litasimamia mifumo imara ya kisheria na taratibu zinazoongoza masuala ya utawala wa umma na uongozi itakayofuatwa na kila kiongozi, nchi haiwezi kutumbukia kwenye mijadala ya kutaka kubadili katiba ili kuwaongezea muhula marais wanapokuwa madarakani.'

Ni msimamo wa mwanasheria na mwanaharakati mbobezi Dk. Hellen Kijo-Bisimba, anapozungumza na Nipashe kuhusu kuibuka kwa mjadala unaotaka kubadili katiba ili kuongeza muhula wa uongozi wa serikali ya awamu ya tano.

"Hao walioanzisha mjadala ni haki yao, lakini pia uwezo wao wa kufikiri hatuupingi... pengine wanatakiwa kupewa elimu waelewe zaidi kwamba katiba iko wazi kuhusu ukomo wa muhula wa rais madarakani. Katiba inasema muhula ni miaka mitano na iwapo rais atachaguliwa tena ataongoza miaka mingine mitano tu ," anasema Dk. Bisimba, ambaye ni mwasisi na mkurugenzi mstaafu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (HLRC) cha jijini Dar es Salaam.

Anasema, kila baada ya miaka mitano nchi inafanya uchaguzi na kama rais aliyeko madarakani anashinda, anaongoza miaka mingine mitano na muhula huo ukiisha, katiba haimruhusu kuendelea.

Anasema miaka 10 imewekwa ili kuepuka kiongozi kukaa madarakani kwa muda mrefu na kwamba anaweza kujisahau na kwenda kinyume na matarajio ya wale anaowaongoza.

"Nisema wanaotaka kuongeza muhula ni haki yao kikatiba kuzungumza, lakini watambue kwamba katiba iko wazi kuhusu ukomo wa rais madarakani, ambao ni miaka 10 tu baada ya hapo anakaa pembeni," anakumbusha.

Anasema badala ya kujadili kuongeza muda wa urais madarakani, ingependeza kama wangesaidia kupatikana kwa mfumo wa kudumu, ambao kila rais atakayekuja atafuata kama ilivyo kwa Marekani.

"Nirudie tena kwamba umefika wakati sasa kuweka mfumo imara, ambao utadumu badala ya kuhangaika kushawishi watu kubadili katiba ili viongozi wakae madarakani kwa miaka mingi," anaonya.



Dk. Hellen Kijo-Bisimba. **PICHA:MTANDAO**

### UDHIBITI UNAHITAJIKA

Mwanasiasa Thomas Ngawaiya, ambaye amewahi kuwa mbunge kupitia chama cha TLP na pia mwanachama wa NCCR-Mageuzi kabla ya kurejea CCM, anasema wanaohamasisha kampeni za kubadili katiba kuongeza muhula wa viongozi wadhibitiwe.

Ngawaiya aliye Mkurugenzi wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo (CEGODETA), anasema ili Tanzania iendelee kujiwekea mazingira ya kudumisha amani, utawala bora, ni vyema walioanzisha mjadala wa kuongeza muda wa rais wakadhibitiwa.

Mwanasiasa huyu anahofia kwamba wanaoibua mijadala hiyo wanaweza kuiingiza nchi kwenye malumbano na mabishano kwasababu ya 'kujikomba' ili watimize haja binafsi badala ya kuangalia maslahi makubwa ya nchi.

"Utawala wa sheria maana yake ni kuheshimu katiba... wanapotokea watu wanashawishi muhula wa urais uongezwe, hawa hawaitakii mema nchi, wanajikomba kupata vyeo... lakini wajue wanaweza kuiingiza nchi katika machafuko na mabishano yasiyo na sababu," anasema Ngawaiya.

Anaonya kuwa kuwashawishi wabunge na wananchi kuvunja katiba kuna madhara yakiwamo kuongoza kwa mabavu na matokeo yake ni kusababisha uvunjaji sheria na misingi ya utawala wa sheria.

Ngawaiya anasifu hatua ya Rais John Magufuli kukataa mapendekezo hayo.

Anamsifu kuwa ni mwanademokrasia asiyetaka kuvunja katiba na kwamba hilo alishaliweka wazi, lakini ni ajabu kusikia baadhi ya watu hadi kwenye mitandao ya kijamii wanashawishi jambo ambalo ni kinyume na katiba liendelee.

Anasema zipo baadhi ya nchi za Afrika ambazo viongozi wake wamejaribu kuongeza muda wa kukaa madarakani na kusababisha machafuko, lakini Tanzania ina utamaduni na kubadilishana viongozi bila kuongeza muda.

Mkurugenzi huyu anasema utamaduni huo ni muhimu na ni vyema uheshimiwe na watu wote ili Tanzania iendelee kuwa kisiwa cha amani na kwamba wasiirudishe nchi kwenye enzi za ujima, ambayo nchi ilishatoka miaka mingi.

"CEGODETA tunasema hao wanaojipendekeza ili kuvunja katiba hawaitakii mema nchi hii, wanafikiria mambo binafsi, hivyo wasipewe nafasi na kwa kuwa serikali na chama vilishakataa, basi wanyamaze," anashauri mwanasiasa huyo.

Anasema Rais Magufuli amefanya mambo mengi mazuri na anaendelea kudhihirisha zaidi kuwa ni kiongozi thabiti wa Watanzania.

"Pamoja na kwamba wanatamani aongozewe hata miaka 20, lakini kwa sababu katiba hairuhusu, inabidi wakae kimya na kuiheshimu," anasema na kuongeza:

"Jambo la kuzingatia ni kwamba viongozi watapita, lakini nchi itaendelea kuwapo, ndiyo maana kumekuwapo na utaratibu wa kuachiana vijiti katika uongozi, hivyo tunatamani utaratibu huo uendelee."

### KUIBUKA MJADALA

Mwaka 2017 mbunge wa Chemba (CCM), Juma Nkamia, alikaririwa na vyombo vya habari akisema ameshawasilisha kwa Katibu wa Bunge barua ya kutaarifu kuhusu mpango alionao wa hoja yake binafsi ya kutaka muda wa rais kukaa madarakani uongezwe kwa miaka miwili zaidi.

Lengo lake lilikuwa kama mpango huo ungepita, basi uandaliwe muswada wa mabadiliko ya 15 ya Katiba ili uchaguzi uwe unafanyika kila baada ya miaka saba, huku moja ya sababu kubwa ya kutaka kufanyika kwa mabadiliko hayo ikiwa ni gharama za kuendesha uchaguzi kwa wakati mmoja, yaani uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu.

Nkamia anasema hoja yake haimaanishi kuwa rais aliye madarakani ndiye aanze kwenda miaka saba, bali ni kwa viongozi wote, na kwamba kama wazo lake lingetimia wakati Rais John Magufuli, akiwa madarakani, nayo si vibaya.

Hoja hiyo iliungwa mkono na baadhi ya wanasiasa akiwamo aliyewahi kuwa mbunge wa Korogwe Vijijini mkoani Tanga, Stephen Ngonyani (marehemu), ambaye naye aliwahi kuomba rais aongezewe muda.

Hata hivyo, Rais Magufuli alikataa ombi la mbunge huyo aliyekuwa maarufu kama 'Profesa Maji Marefu,' alilolitoa kwenye mkutano wa hadhara na kusema hayuko tayari kuvunja katiba.

Rais Magufuli alikemea na kusema amefunga mjadala huo usio rasmi, lakini inaonekana kulikuwa bado kuna watu wanauendeleza.

Ilikuwa Januari 2018, alipokutana na kufanya mazungumzo na Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM, Itikadi na Uenezi, Humphrey Polepole, Ikulu Jijini Dar es Salaam na kumpa maelekezo kuhusu mjadala huo.

Polepole alikaririwa na vyombo vya habari akisema Rais amemuelekeza kuwajulisha wana CCM na umma kwamba anasikitishwa na hafurahishwi na mjadala unaoendelea juu kuongezwa kwa kipindi cha urais kutoka miaka mitano iliyowekwa kwa mujibu wa katiba, hadi miaka saba.

### CCM YANENA

Kwa upande wake chama tawala, yaani CCM, kimepuuza matakwa hayo na kuwataka Watazania kutupilia mbali mjadala unaohusu kuongeza kipindi cha urais.

Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, amefunga mjadala huo na kwamba kulingana na utaratibu wa chama hicho, Rais Magufuli hawezi kuongeza muda baada ya mwaka 2025.

Anasema atamaliza muda wake na kupumzika, anawataka wanaodai ataongeza muda waachane na kauli hizo.

"Rais Magufuli atamaliza muda wake na kumpuzika na tutapata rais bora, naomba kuhitimisha mjadala huu," Bashiru anakaririwa na vyombo vya habari akisema hayo.

MAKALA

# Uhuru atafuta muafaka na Ruto

## ■ Wafuasi wa Raila wazidi 'kupigilia'

**Na Ani Jozeni**

SIASA za Kenya sasa zimeanza kufanana na za Tanzania kwa miaka kadhaa kabla ya uchaguzi mkuu wa 2015 na kwa kipindi fulani baada ya hapo, huku masuala kadhaa yakiendana, ila mifumo ya ushindani ni tofauti.

Kuanzia mwaka 2007 hadi takriban 2015 aliposhindwa katika uchaguzi mkuu, jina la Edward Lowassa lilitawala katika medani ya siasa, wakati wanaomuunga mkono wakijitahidi kuwasiliana na kuondoa shaka miongoni mwa wapiga kura wao kuhusu hatma ya kiongozi huyo, huku wapinzani wake wakitumia kila mbinu kumuondoa katika kinyang'anyiro cha kugombea urais 2015.

Ni uasi dhidi yake uliomwondoa Lowassa CCM.

Kama ilivyokuwa kwa Lowassa, uasi dhidi ya Naibu Rais William Ruto umejikita katika kundi la vyama vya siasa lililoko madarakani, kwa jina la Jubilee (kutokana na kuundwa mwaka 2013, ambako Kenya ilisherehekea miaka 50 ya uhuru wake).

Harakati hiyo imejipambanua kwa vita dhidi ya rushwa, ambako wakuu wa wizara na mamlaka kadhaa serikalini wanaotuhumiwa kwa matumizi mabaya ya fedha za umma, zabuni feki, ujenzi wa miundombinu chini ya kiwango au makisio ya gharama yanayoleta kigugumizi serikalini, wanaondolewa katika nyadhifa zao.

Hakuna ubishi wowote nchini humo kuwa wengi wao wana uhusiano wa karibu na Naibu Rais.

Nafasi ya Naibu Rais nchini Kenya inafanana kiasi fulani na Waziri Mkuu hapa nchini, kwani Makamu wa Rais hapa ni cheo chenye ladha ya Muungano na siyo mifungamano ya vyama na makundi ndani ya chama tawala, kama ilivyo nafasi ya Waziri Mkuu au Naibu Rais kwa upande wa Kenya.

Ushindani kuhusu Lowassa ulijikita katika kampeni ya 'kujivua gamba' ambayo ni lugha ya kiitikadi wakati hakuna suala kama hilo Kenya, ila ni kampeni halisi serikalini ya kukagua na kugundua mapungufu, kama ilivyo kampeni dhidi ya rushwa katika awamu ya tano.

Ukinzani wa 'kujivua gamba' ulilenga uhalali wa anayelengwa kuongoza, na siyo kubadili nchi.


Tofauti ya msingi kati ya mielekeo hiyo tofauti ya 'vita dhidi ya rushwa' ni kuwa harakati ya kiitikadi inajikita katika uhalali au kukubalika kwa mtu mmoja na baadhi ya watu wake wa karibu (kwa mfano aliyekuwa mbunge wa Igunga, Rostam Aziz) kushika madaraka au kurudi madarakani.

Vita halisi dhidi ya rushwa inatokana na sintofahamu ya chama tawala kwa mustakabali wa kukubalika kwake na wananchi, hasa kuhusiana na uchaguzi mkuu unaofuata, na kwa maana hiyo inatekelezwa na serikali iliyoko madarakani ili kukifagilia chama tawala katika uchaguzi mkuu unaokuja.

CCM iliingia katika hali hiyo baada ya uchaguzi 2015, na Jubilee mwaka jana.

Hatua ya utawala wa Rais Uhuru Kenyatta kuingia katika vita dhidi ya rushwa, hivyo kuumiza vigogo maridhawa wenye uhusiano wa jadi na viongozi waandamizi wa Jubilee ulifuatia 'kupeana mkono' Rais Kenyatta na kiongozi wa upinzani Raila Odinga.

Ni pale sokomoko ya nini kilitokea katika uchaguzi mkuu 2017 ilipofikia



Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya (kushoto) akiwa na Naibu Rais William Ruto. **PICHA: MTANDAO**

> "Baadhi ya vichwa vya habari katika magazeti na televisheni za Kenya hivi karibuni vinaonyesha upana wa siasa kizungumkuti kuhusu suala hilo, mojawapo ikiwa ni Citizen TV ikisema 'Uhuru, Raila wawashutumu wafuasi wa Ruto kwa siasa za kugawa watu.'

kuapishwa nje ya katiba kwa Odinga, viongozi wa kundi lake la Orange Democratic Movement (ODM) kuanza kutishiwa maisha (na huko Kenya suala hilo si utani, viongozi wa upinzani au mawaziri wasio watiifu wanapigwa risasi mchana kweupe).

Akijua kuwa kundi lake litalengwa zaidi kwa hujuma, Raila 'alibadili gia angani,' wakaafikiana.

Ni kuanzia hapo ambapo moto wa kisiasa ukawa unawakia kambi ya Naibu Rais, kwani Uhuru na Raila walianza kuwa 'kitu kimoja' katika mapambano dhidi ya rushwa, watu waking'olewa na kufikishwa mahakamani, huku maumivu ya wazi yanasikika kambi ya Ruto katika mkusanyiko wa Jubilee.

Hivi karibuni mvutano ndani ya Jubilee ukafikia hatua ngumu ambako Kenyatta amekosana waziwazi na wafuasi wa Jubilee eneo la katikati ya nchi hiyo (maskani yake kiasili ya kisiasa) ambako wengi wao wanamuunga mkono Ruto.

Pia aliwatingisha wafuasi wa Jubilee eneo la Bonde la Ufa anakotoka Ruto, alipomteua Fred Matiang'i kuwa 'Waziri Kiongozi.'

Ni katika mazingira hayo ambako sasa Uhuru amejikuta akihitaji kupatana angalau kwa kiasi fulani na Ruto, huku wafuasi wa Raila wakiwa hawana mpango wa kusikia 'la mwadhini au la mteka maji' kuhusu kampeni ya kumwondoa Ruto madarakani kutokana na kuhusishwa na watajwa wengi katika kampeni dhidi ya rushwa.

Hilo si jambo geni nchini humo na hasa katika siasa za vyama vya bungeni, kwani kiongozi au msemaji wa masuala ya sheria wa upinzani, Seneta James Orengo (wa jimbo la Siaya, Nyanza anakotoka Raila) aliwahi zamani kuitisha kura ya kutokuwa na imani na Rais Daniel arap Moi akiwa madarakani, na Ruto alipigiwa kura kama hiyo wakati mmoja, akiwa Waziri wa Kilimo. Ila ni mchecheto kwani mjadala wenyewe unaondoa sifa kwa mhusika.

Ndiyo hapo tunaingia katika matukio ya hivi karibuni ambako mkutano wa Uhuru na Ruto ni kama umebadili upepo wa kisiasa nchini humo, ikielezwa kuwa walifanya mazungumzo ya saa tano katika ofisi ya Naibu Rais, hali inayoashiria kuwa ni Uhuru aliyekuwa akitafuta maelewano kiasi fulani.

Hata hivyo, alisisitiza baada ya maongezi hayo kuwa Naibu Rais naye achukue nafasi yake katika vita dhidi ya rushwa, hali ambayo iliwashtua baadhi ya wafuasi wa karibu wa Raila, kuwa badala ya kuendesha kampeni hiyo na Raila, inaelekea Uhuru anarudi nyuma, kuifufua Jubilee kama mkusanyiko.

Orengo akataka Ruto apigiwe kura ya imani, kabla hali haijaharibika zaidi, kwani kwa wakati uliopo Uhuru ameonyesha waziwazi kutokuwa na imani na Naibu Rais.

Hatua hiyo ya Orengo ilimuundhi Raila kwani inakuwa ni kutingisha kiberiti na kuhatarisha uwezo wa kufanya kazi pamoja kati ya rais na kiongozi wa upinzani, kwa kuheshimu kuwa Uhuru bado ni kiongozi wa Jubilee na kuwa Ruto ni naibu wake.

Kufanyia mchezo jambo hilo kutaondoa 'kupeana mikono' kutoka katika mkataba wa kisiasa na kugeuka urafiki binafsi ambao hautabiriki, wakati mkataba wa kisiasa lazima uwe na mipaka ili uweze kufanya kazi ipasavyo.

Orengo alivuruga mikakati ya Uhuru na Raila ambao walilenga kuunganisha nchi nzima katika vita dhidi ya rushwa, kwani kutaka Naibu Rais aondolewe ni kumtaja kuwa ni mla rushwa kiongozi.

Baadhi ya vichwa vya habari katika magazeti na televisheni za Kenya hivi karibuni vinaonyesha upana wa siasa kizungumkuti kuhusu suala hilo, mojawapo ikiwa ni Citizen TV ikisema 'Uhuru, Raila wawashutumu wafuasi wa Ruto kwa siasa za kugawa watu.'

Kichwa kingine cha mblogi binafsi Lee Makwiny kilisema 'Uhuru atoa somo kwa hasira kwa wafuasi wa Ruto kuhusu muafaka na Raila,' wakati kingine kinatoa majibu makali ya Ruto kwa pendekezo la Seneta Orengo la kura ya kutokuwa na imani naye.

NTV Kenya ikatoa nafasi ndefu kiasi kwa mada ya 'Uhuru amtembelea Ruto kwa chakula cha mchana: Waliongea nini?" Citizen TV ikaja na kichwa kingine "Naibu Rais Ruto, washirika wake wamshambulia kiongozi wa ODM Raila Odinga," halafu mblogi Lee Makwiny akatoa uchambuzi, 'Undani wa Mkutano.





# Wananchi wadaiwa kuleta uharibifu mazingira

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

BAADHI ya wananchi wanaoishi katika eneo lenye mgogoro kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na Jiji la Mbeya, wanadaiwa kufanya vitendo vya uharibifu wa mazingira, huku halmashauri zote mbili zikishindwa kuwachukulia hatua.

Inadaiwa kuwa wananchi hao wakiguswa na viongozi wa halmashauri moja wapo wanadai kuwa wao hawapo kwenye utawala wa eneo husika na badala yake wao ni wakazi wa halmashauri ya pili.

Hayo yalisemwa na Diwani wa Kata ya Nsalala katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, Kissman Mwangomale, wakati wa mkutano wa hadhara wa wananchi wa kata hiyo uliofanyika katika Mtaa wa Mapinduzi.

Alisema wananchi hao wanalima kwenye maeneo yasiyoruhusiwa na kukata miti ovyo, lakini kila wakiguswa wanadai wameruhusiwa na viongozi wa Kata ya Iwambi, hivyo akadai kuwa hali hiyo inasababisha hali ya utawala kuwa ngumu.

Alisema wananchi hao wamelima mahindi na wanachimba mawe na kokoto kwenye mlima, hali inayolifanya eneo hilo kuwa wazi bila miti na baadhi yao wameanza kujenga makazi ya kudumu kwenye eneo hilo bila kuwa na vibali.

"Tuna shida ya mpaka kati yetu na wenzetu wa Jiji sasa kuna baadhi ya watu ambao wapo ndani ya eneo la mgogoro wanafanya mambo ambayo ni kinyume na sheria, lakini tunashindwa kuwazuia kutokana na wao kuutumia mgogoro huu kutuvuruga," alisema Mwangomale.

Aliwaomba wananchi wa kata hiyo kutowafanya chochote watu hao na badala yake wasubiri mpaka mgogoro huo utakapokuwa umepatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Kwa upande wao baadhi ya wananchi wa kata hiyo walidai kuwa mpaka kati ya Jiji na Mji wa Mbalizi upo katika eneo ambalo pana kibao lakini watu wa Jiji wamehamisha mpaka na kuusogeza katika eneo la reli ya Tazara.

Baadhi ya wananchi hao walitishia kwenda kufyeka mahindi yaliyolimwa na wenzao hao ili kuokoa mazingira, lakini wakazuiliwa na viongozi wao kwa madai kuwa hali hiyo inaweza kuzua mgogoro zaidi.

**"Tuna shida ya mpaka kati yetu na wenzetu wa Jiji sasa kuna baadhi ya watu ambao wapo ndani ya eneo la mgogoro wanafanya mambo ambayo ni kinyume na sheria...**

# Chalamila anusa ufisadi ujenzi wa vituo vya afya

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amesema kituo kimoja kati ya vitatu vilivyojengwa na serikali katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kina harufu ya ubadhirifu wa fedha za umma ambao umefanywa na baadhi ya wajanja.

Chalamila aliyasema hayo alipokuwa anazungumza na wananchi wa kata za Ilembo na Santilia ambako alitembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa vituo vya afya vilivyojengwa kwa ushirikiano kati ya wananchi na serikali.

Alisema wilaya hiyo ilipewa zaidi ya shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vitatu vya Ilembo, Ikukwa na Santilia, lakini kituo kimoja wapo wanjanja wamepiga fedha hizo, hivyo akasema uchunguzi unafanyika na kwamba watakaobainika watachukuliwa hatua. "Serikali ya sasa sio ya mchezo, hivyo sisi tunaendelea na uchunguzi wa kituo hicho ambacho sitakitaja na ikibainika kuwa ni kweli kuna ufisadi ni lazima watu wachukuliwe hatua kali za kisheria ili iwe fundisho kwa wengine," alisema Chalamila.

Aidha, alisema Serikali Kuu imetoa zaidi ya shilingi bilioni 6.7 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya katika wilaya zote za mkoa huo, ambavyo baadhi vimekamilika na vingine vipo katika hatua mbalimbali za umaliziaji.

Chalamila alisema Mkoa wa Mbeya umepata sifa nzuri kwenye usimamizi wa ujenzi wa vituo hivyo ambavyo vinajengwa kwa kutumia mfumo wa akaunti ya dharura (Force account) na kuufanya mkoa kuwa wa mfano.

Alisema kituo cha kwanza cha mfano kilijengwa katika Kata ya Ikuti wilayani Rungwe na kituo ambacho ni bora kuliko vyote nchini ni Kituo cha Afya cha Ipinda wilayani Kyela, hivyo akawataka wachache wasichafue sifa hiyo.

Aliwapongeza wananchi wa kata zote ambazo zilipatiwa fedha kwa ushiriki wao katika ujenzi wa vituo hivyo ambavyo vitachangia kupunguza tatizo la huduma ya afya mkoani humo.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Mwalingo Kisemba, alisema vituo vyote vitatu vilivyojengwa ndani ya halmashauri yake vina hadhi ya hospitali isipokuwa havina majengo ya huduma za mionzi.

Alisema Kituo cha Ikukwa kilijengwa kwa zaidi ya shilingi milioni 800, Kituo cha Afya cha Ilembo milioni 400 na cha Santilia kimejengwa kwa zaidi ya shilingi milioni 560.

Alisema wananchi wa maeneo yote vilikojengwa vituo hivyo walishiriki kuchangia nguvu zao kwa kufyatua tofali, kubeba mawe na mchanga pamoja na kushirikiana na mafundi kwenye ujenzi hasa kwa kuwasogezea vifaa.

"Mbali na vituo hivi Mkuu wa Mkoa, pia wilaya yetu imepewa na mheshimiwa Rais shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ambayo tunaijenga katika eneo la Inyala ambako wananchi wamejitolea eneo lenye ukubwa wa zaidi ya ekari 32," alisema Kisemba. Alisema hospitali hiyo pia itajengwa kwa kutumia mfumo wa Force account ambao unaruhusu kuwatumia mafundi wa mitaani ili kuharakisha na kwamba watazingatia ubora.



Meneja Masoko wa Benki ya NBC, Alina Maria Kimaryo (kushoto), akikabidhi pikipiki kwa mmoja wa washindi wa kampeni ya Shika Ndinga inayodhaminiwa na benki hiyo, kwa upande wa wanaume, Ally Rashidi, wakati wa kampeni iliyofanyika katika Uwanja wa Kibaha stendi ya zamani, mkoani Pwani jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madereva waungana TBS vilainishi feki

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

BAADHI ya madereva jijini Mbeya, wameiomba serikali kupitia Shirika la Viwango nchini (TBS) kuendelea kufanya operesheni za mara kwa mara kwenye maduka yanayouza vilainishi ili kudhibiti uuzwaji wa vilainishi feki.

Walitoa ombi hilo jana walipokuwa wanazungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti kuhusu matumizi ya vilainishi vinavyouzwa kwenye maduka mbalimbali jijini hapa, ambapo walisema vilainishi hivyo vinasababisha magari kuharibika mara kwa mara.

Mmoja wa madereva hao, Juma Mwamwenda, alisema vilainishi hivyo visivyokidhi ubora huwa vinatumika zaidi maeneo ya karakana za kutengeneza magari, ambapo mafundi huwa wanavinunua kwa ajili ya kukwepa gharama kuwa kubwa.

Alisema ili kuepuka kuwekewa vilainishi hivyo ni lazima madereva na makondakta wawe wanawasimamia mafundi wanapotengeneza magari hayo ama waende wakavinunuwe wenyewe badala ya kuwaachia jukumu hilo mafundi.

"Vilainishi hivyo huwa vinauzwa kwa bei ya chini na kwenye maduka huwa vinafichwa, kwa hiyo hata wanaouza wanawauzia watu wanaofahamiana nao ili wawafichie siri, sasa njia pekee ya kukwepa ni mwenye gari kwenda kununua mwenyewe," alisema Mwamwenda.

Alisema mfundi wa magari huwa wanavinunua kwa bei ya chini, lakini kwa mwenye gari wanataja bei ya vilainishi vinavyokidhi vigezo ili wapate faida zaidi.

Aliwaomba maofisa wa TBS kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye maduka na kuviondoa vilainishi hivyo visivyokidhi viwango ili kuvikomesha kabisa.

Naye Lazaro Mbilinyi ambaye ni dereva wa malori yanayosafirisha mizigo kwenda nchi za nje alisema vilainishi visivyokidhi viwango hasa vya breki husababisha kuharibika kwa mifumo ya gari na hivyo kusababisha ajali.

Alisema mbali na TBS kuvikamata vikiwa madukani lakini pia wahakikishe wanadhibiti maeneo ya bandarini ili visiingizwe kabisa sokoni na kuwaletea watu shida. Alidai kuwa vilainishi hivyo vikidhibitiwa nchini na elimu ikatolewa kwa wananchi juu ya matumizi ya vilainishi hivyo, ajali za barabarani zinazogharimu maisha zitapungua na hata kuisha kabisa.

"Mtu anayeweza kuepuka kununua vilainishi hivyo ni yule ambaye amepewa elimu na anavielewa lakini wengine wananunua tu, lakini pia Watanzania tunapenda vitu vya bei ndogo na ndio maana vilainishi hivyo vinauzwa," alisema Mbilinyi.

Hivi karibuni, Maofisa wa TBS kutoka Makao Makuu jijini Dar es Salaam na wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, walifanya ukaguzi wa kushtukiza kwenye maduka yanayouza vilainishi jijini Mbeya na kukamata shehena kubwa ya vilainishi feki na kuvikusanya kwa ajili ya kwenda kuviteketeza.

Mkaguzi Ubora wa TBS kutoka Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mhandisi Yekonia Sanga, alisema vilainishi hivyo vinaingizwa nchini kwa njia za magendo na vinauzwa madukani bila kuwa na nembo ya ubora inayotolewa na shirika hilo.

Alisema wananchi wanatakiwa waache kuvitumia kutokana na kuwa hatari kwa maisha yao kwa maelezo kuwa havina uwezo wa kufanya kazi inayokusudiwa kwa ufanisi.

Alisema shirika hilo litaendelea kufanya kaguzi mbalimbali za kushtukiza kwenye maduka na kuviondoa ikiwa ni pamoja na kuwatoza faini wahusika.





# RC Mahenge apigia debe wawekezaji kutumia ATCL

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, amewataka wawekezaji kutumia fursa za kutangaza bidhaa zao kupitia Shirika la Ndege Tanzania ATCL ili kujiongezea kipato.

Dk. Mahenge alitoa wito huo jijini Dodoma baada ya kutembelea wajasiriamali wadogo wanaojishughulisha na utengenezaji wa bidhaa mbalimbali ikiwamo vyakula na vinywaji, ambapo amesema bidhaa hizo zinaweza kutumika kama viburudisho wakati wa safari za anga kupitia Shirika la Ndege la ATCL.

Alisema watengenezaji wa bidhaa mbalimbali nchini wanatakiwa kuitumia fursa hiyo ili kuweza kujitangaza ndani na nje ya nchi kupitia safari mbalimbali za anga.

"Rais wetu ametengeneza fursa hii kwa kulifufua shirika letu la ndege kwa kununua ndege zaidi ya sita, lakini pia ametoa fedha kwa ajili ya ukarabati wa viwanja vya ndege, hivyo wazalishaji wa bidhaa mbalimbali za vinywaji pamoja na vyakula wanatakiwa kuitumia fursa hii ili kuweza kujiongezea kipato," alisema Dk. Mahenge.

Aidha, alisema kuwa haitakuwa jambo jema kama shirika hilo katika ndege zake litaweka bidhaa za mataifa ya nje badala ya kuzitumia za ndani ya nchi ili kuweza kujitangaza kimataifa.

Aliwataka wajasiriamali ambao watapata fursa ya kuweka bidhaa zao kwenye ndege za ATCL kutengeneza bidhaa zenye ubora chini ya uangalizi wa mamlaka husika zinazosimamia viwango kama vile shirika la viwango nchini TBS.

Kwa upande wake Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Shirika la Ndege nchini ATCL, Josephat Kagirwa, alisema lengo lao ni kuona bidhaa zinazotumika ndani ya ndege ni zile za kutoka nchini na siyo vinginevyo.

Alisema kuwa wamekuja Dodoma kukutana na wazalishaji wa bidhaa mbalimbali ili kuweza kuona zile bidhaa ambazo shirika hilo linaweza kuzitumia katika kutoa huduma ndani ya ndege zake.

"Tayari tulishaanza na bidhaa kama vile mvinyo katika ndege zetu, mvinyo unaotumika hivi sasa ni kutoka hapa Dodoma, lakini pia bado zipo huduma ambazo sisi tunazitoa katika ndege zetu kama vile vyakula pamoja na mablanketi kwa ajili ya zile safari za mbali hivyo tumekuja kuona hizi bidhaa ili tuweze kutoa uamuzi wa kuzitumia," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Kiwanda cha Mvinyo (SETAWICO) kilichopo jijini hapa, Catherine Mwimbe, alitoa wito kwa wananchi kupatiwa elimu ya utambuzi wa fursa kufuatia uwepo wa safari za anga.

Alisema fursa nyingi zipo, lakini bado wananchi wamekuwa waoga kujitokeza katika kuthubutu kuzitumia kila zinapojitokeza.



Mkurugenzi wa Huduma za Afya, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Kapologwa Ntuli (kushoto), akikata utepe kuashiria uzinduzi rasmi wa kampeni ya kuzuia ugonjwa wa sikoseli, itakayoendeshwa kwenye shule za sekondari nchini, uliofanyika jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wananchi walalamikia diwani wa CCM

**Na Peter Mkwavil, DODOMA**

WANANCHI wa mtaa wa Mkalama Kata ya Kikuyu Kusini jijini Dodoma wamemlalamikia diwani wao (CCM), Anselim Kutika, pamoja na watendaji wake wa chini kutokana na migogoro ya ardhi isiyoisha.

Wakizungumza kwenye mkutano wa hadhara ulioandaliwa na Katibu wa CCM Wilaya ya Dodoma Mjini, Grace Shindika, kwa lengo la kutaka kusuluhisha mgogoro huo, wananchi hao walisema kuwa mgogoro huo umekuwa wa muda mrefu toka mwaka 2015, wakati huo ikiwa chini ya Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (CDA).

Javan Majen, mmoja wa wananchi wa kata ya Kikuyu Kusini akiongea kwa niaba ya wananchi wenzeke katika mkutano huo alisema kuwa kudumu kwa mgogoro huo kumesababishwa na uongozi mzima wa kata chini ya diwani huyo pamoja na watendaji wake.

Alieleza kuwa wakati wanapimiwa viwanja na manispaa wakati huo kabla haijawa jiji upimaji wa makazi ulifanyika vizuri na hata kwenye mashamba, ila zoezi lilikuja kubadilika baada ya uongozi wa kata kutaka kuhakiki wao wenyewe bila ya kuwashirikisha wananchi.

Alisema pamoja na jitihada za kulipeleka suala hilo kwa ngazi mbalimbali ikiwamo kwa Waziri Mkuu wa wakati huo Mizengo Pinda ambaye naye aliamuru wapatiwe haki yao na kupatiwa viwanja, lakini hata hivyo mpaka sasa wamegonga mwamba.

"Sisi wakazi wa mtaa huu wa Kikuyu kwa kupitia mkutano huu mbele ya katibu wetu huyo wa CCM wilaya tunaiomba serikali yetu tukufu inayojali wanyonge na sikivu kuingilia kati, ili tatizo hili tupatiwe haki yetu ya msingi ya madai ya viwanja vyetu, ikumbukwe tulifika hadi kwa Waziri Mkuu wa zamani Mizengo Pinda na tukamwelezea na yeye aliagiza mradi huo ufuatiliwe kwa makini na iliyokuwa CDA kwa wakati huo juu ya wananchi kupewa haki zetu, lakini mpaka leo bado tuna mgogoro," alisema Magdalena Mathias.

Kwa upande wake Katibu wa CCM, Grase Shindika, akizungumza na wananchi hao kwenye mkutano huo alisema kuwa mgogoro huo umejitokeza kutokana na wananchi hao kutopata haki zao za msingi pamoja na kutoelewa mkataba wa upimaji wa ardhi kwenye makazi yao na mashamba.

Shindika alisema kutokana na wanachi hao kutopata mkataba huo ambao walitakiwa waupate kabla ya kufanyiwa uhakiki wa kuboreshewa maeneo yao au kupimiwa, hivyo kushindwa kuelewa asilimia ngapi zitakwenda kwa serikali na ngapi zinazobaki kwa wananchi.

Akijibu tuhuma hizo dhidi yake Diwani wa Kata hiyo, Anselim Kutinka, alidai yeye viwanja anavyomiliki ni vinne tu na kama kuna zaidi vingine ambavyo anavyovimiliki wananchi wanatakiwa kuleta vithibitisho.

# Wachinjaji kuku wapewa ushauri

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

WACHINJAJI wa kuku na wauzaji wa samaki wabichi waliopo kwenye masoko ya Jiji la Dodoma wametakiwa kuzingatia usafi katika maeneo yao wanayofanyia kazi, ili kujilinda na milipuko ya magonjwa ambayo yanayoweza kuleta madhara kwao pamoja na walaji.

Ushauri huo ulitolewa na Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yunah, alipokuwa akizungumza na wachinjaji na wauzaji wa kuku wa soko la Miembeni jijini katika kampeni yake ya kukagua na kuhakikisha masoko yote yanakuwa safi kwa matumizi.

Yuna alisema kuwa ili kuondokana na madhara kwenye maeneo hayo ya kuchinja na kuuza ni muhimu wahusika wakazingatia vigezo vya kujilinda na maambukizi yanayoweza kujitokeza kama vile magonjwa kwa kuweka mazingira katika hali ya usafi.

Aidha, aliwataka kuhakikisha vifaa vinavyotumika kuchinjia vinakuwa katika hali ya usafi, hii ikiwa na pamoja na mavazi yao.

"Ushauri wangu huu ni kwa masoko yote yaliyopo jijini hapa na yazingatie huo usafi ili kuepukana na milipuko inayoweza kujitokeza kwa wafanyabiashara na walaji wa nyama hiyo ya kuku na samaki," alisema.

Hata hivyo aliwataka wafanyabiashara kwenye masoko mbalimbali kushirikiana na jiji katika suala zima la usafi kwa kuunga mkono serikali ambayo imekuwa ikisisitiza kila Mtanzania kufanya usafi kwenye eneo lake.

Ofisa masoko huyo pia aliwataka wafanyabiashara ndani ya masoko hayo kuhakikisha wanalipa ushuru ili yaweze kuboreshwa kutokana na fedha hizo wanazozitoa.

"Pamoja na Halmashauri ya Jiji kwa kushirikiana na serikali kuhusika katika maboresho ndani ya masoko lakini kwa upande wa wafanyabiashara wanastahili kuwa waaminifu katika suala la utoaji wa ushuru," alisema.

Hata hivyo alisema kutokana na ujio wa makao makuu ya serikali ni muhimu wakabadilisha biashara zao kwa kuwa wabunifu ili kujiongezea kipato zaidi na kuwawezesha kumudu maisha yao ya kila siku.

**"Ushauri wangu huu ni kwa masoko yote yaliyopo jijini hapa na yazingatie huo usafi ili kuepukana na milipuko inayoweza kujitokeza kwa wafanyabiashara na walaji wa nyama hiyo ya kuku na samaki," alisema.**



# Waajiri wakumbushwa kufuata sheria za ajira

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Vvyama vya Wafanyakazi Zanzibar limewataka waajiri kuzijua na kuzifuata sheria za kazi ili wafanyakazi waweze kupata haki zao.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu Siku ya Wafanyakazi Duniani, Katibu Mkuu wa shirikisho hilo, Khamis Mwinyi, alisema baadhi ya waajiri wamekuwa na matumizi mabaya ya sheria kwa kuwasimamisha au kuwaachisha kazi wafanyakazi bila ya sababu za msingi.

Katibu huyo aliiomba serikali kuwachukulia hatua za kisheria waajiri hao wanaokiuka sheria za kazi kwa kuwatumikisha wafanyakazi katika mazingira magumu bila kuwalipa stahiki zao kwa wakati.

Alisema bado zipo baadhi ya taasisi zinawakandamiza wafanya kazi ikiwamo kuwalipa maslahi madogo, kuwatumikisha kwa muda mrefu bila ya mishahara pamoja na malimbikizo ya posho ya likizo.

Alieleza kuwa wafanyakazi wa taasisi za serikali na binafsi wanafanyakazi katika mazingira magumu na hatarishi bila ya kuwa na bima za afya.

Katibu huyo aliiomba serikali kufanyia mapitio na marekebisho ya sheria ya kazi kutokana na upungufu uliyopo ambao unasababisha kuminya haki za wafanyakazi hasa katika upatikanaji wa maslahi yao katika sehemu zao za kazi.

Aidha, alisema kuwa ushirikishwaji mdogo wa vyama vya wafanyakazi katika vikao vya maamuzi sehemu za kazi kumekuwa kukiwanyima fursa wafanyakazi kutoa maoni yao.

"Changamoto katika sekta za ajira ni nyingi miongoni mwa hizo ni mazingira hatarishi kwa baadhi ya wafanyakazi wanaotumia mashine za mionzi bila ya kulindwa kiafya na kiusalama," alisema.

Hata hivyo katibu huyo aliipongeza serikali kwa kufanya ugatuzi kwa baadhi ya taasisi, lakini kumekuwa na athari katika ugatuzi huo ikiwamo uhaba wa wafanyakazi wa afya na elimu katika halmashauri, wafanyakazi kuhamishwa kiholela, makato yasiyo ya kisheria ya mishahara kwa wafanyakazi.

Alieleza kuwa jumla ya malalamiko na migogoro 500 ya wafanyakazi yamewasilishwa katika kamati ya utatuzi na usuluhishi wa migogoro ya wafanyakazi, ambapo malalamiko zaidi ya 100 yameshughulikiwa. Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi hufanyika Mei mosi kila mwaka na kwa mwaka huu kwa Zanzibar yanatarajiwa kufanyika Mkoa wa Kusini Unguja, ambapo kauli mbiu ni kuima-




Miundombuni ya barabara ya mabasi ya mwendo kasi ikiwa imeharibiwa kwa muda mrefu bila ya kufanyiwa marekebisho katika kituo cha Kimara Corner, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wafanyabiashara wazungumzia sakata la rushwa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WANACHAMA wa Jumuiya ya Wafanyabiashara na Viwanda Zanzibar, wamesema kuwa vitendo vya rushwa vimekuwa vikiongozeka kwa sababu kumekuwa na vikwazo katika upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii.

Wakizungumza katika mkutano wa kujadili vitendo vya rushwa, ulioandaliwa na mamlaka ya kuzuwia rushwa na uhujumu wa uchumi Zanzibar,(ZAECA), wafanyabiashara hao walisema kuwa iwapo huduma muhimu za kijamii zitapatikana bila ya vikwazo vitendo vya rushwa vinaweza kutoweka.

Akizungumza katika mkutano huo, mfanyabiashara Abdulmalik Haji Jecha, alisema kuwa licha ya kwamba serikali imeunda taasisi ya kupambana na rushwa lakini hakuna mtu aliyehukumiwa kutokana na rushwa.

"Sio kama vitendo vya rushwa havipo, vipo vingi tu, lakini tangu ianzishwe taasisi hii hatujasikia mtu kuhukumiwa kwa rushwa," alihoji mfanyabiashara huyo.

Alieleza kuwa rushwa ndogo ndogo inawaumiza sana wafanyabiashara hali ambayo inasababisha serikali kulalamikiwa.

Alieleza kuwa bila ya kuwa wazazi na kuwakamata wala rushwa vitendo vya rushwa havitoweza kuondoka na vitazidi kuongezeka kila siku.

"Rushwa ni sawa na donda ndugu na la muda mrefu, hivyo kama halitapatiwa tiba stahiki tutaendelea kuuguza," alisema.

Naye mjasiriamali Mayasa Sadi Suleiman, alisema kuwa vitendo vya rushwa vimekuwa vikiwakandamiza wajasiriamali na kushindwa kufikia malengo yao.

Alieleza kuwa baadhi ya watu ambao wamekuwa na nyadhifa kubwa serikalini wamekuwa wakiingiza bidhaa mbalimbali bila ya kulipia ushuru hali ambayo imekuwa ikiwaumiza wafanyabiashara wadogo.

Naye Ofisa Elimu wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa, Yussuf Juma Silim, alisema kuwa rushwa imekuwa ikirudisha nyuma maendeleo ya wajasiriamali wadogo wadogo, kuua viwanda vya ndani na kuhatarisha ustawi wa maendeleo ya jamii.

Alisema kuwa uchumi wa dunia utaendelea kushuka iwapo vitendo vya utakasishaji fedha na rushwa vitaendelea hali inayochangia kudumaa uchumi wa dunia.

Akifunga mafunza hayo mkurugenzi wa mamlaka hiyo Mussa Haji, alisema, ameitaka jamii kuacha kulalamika pembeni kuhusu vitendo vya rushwa na badala yake kuripoti katika sehemu husika ili hatua ziweze kuchukuliwa.

# Waziri awafunda masheha kufuata sheria

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ, Haji Omar Kheri, amewataka masheha kufanya kazi kwa kufuata sheria, taratibu na miongozo ya nchi ili kuepusha migogoro katika jamii.

Alisema ni wajibu wao masheha kufuata kanuni na taratibu zilizopo katika kusimamia na kutekeleza majukumu yao ya kila siku kwa kuwa wao ni wasimamizi wa sheria katika maeneo yao.

Waziri huyo alitoa kauli hiyo wakati akifungua mafunzo ya maadili na kuwajengea uwezo masheha wa Mkoa wa Mjini Magharib katika ukumbi wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Bububu.

Aliwataka viongozi hao wa shehia kutojihusisha migogoro ya ardhi badala yake kusimamia na kutoa elimu kwa jamii juu ya matumizi bora na kuepusha ukiukwaji wa sheria katika mambo mbalimbali kwa wananchi wanaowaongoza.

Waziri huyo alikemea vitendo vinavyofanya na baadhi ya masheha vya migogoro ya ardhi na kuwataka kuwacha mara moja kabla serikali haijawachukulia hatua iwapo watabainika kutenda jambo hilo.

Aidha, aliwataka viongozi hao kuzingatia mafunzo ya maadili wanayopatiwa kwa lengo la kutojihusisha katika matatizo ndani ya jamii na ukiukwaji wa haki.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharib, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema serikali ya mkoa wake imeamua kutoa mafunzo ya maadili na uongozi kwa viongozi hao wa shehia ili kuona masheha wanawajibika ipasavyo katika kufuata miongozo ya uongozi pasi na kujihusisha na masuala ya uvunjifu wa sheria katika maeneo yao.

Ayoub aliwataka masheha hao kuendelea kuwa karibu na wananchi ili kuweza kufanya kazi na kuwatatulia changamoto mbalimbali zinazowakabili na kutimiza malengo ya serikali ya kuwaletea maendeleo wananchi iweze kufikiwa.

Alieleza kuwa mafunzo hayo kwa ngazi za awali za uongozi ni kutekeleza maagizo na miongozo ya serikali kuu juu ya kujengewa uwezo kwa viongozi hao wa shehia ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Kwa upande wake Kaimu Mkuu wa Chuo hicho, Jason Nkyabonaki, alisema wameanza kutoa mafunzo ya uongozi na maadili kwa viongozi wa kada mbalimbali ili kuwajenga uwezo mzuri wa uongozi na utawala bora na kuzitumikia vyema dhamana zao.

Jumla ya masheha 121 wa shehia zote za Mkoa wa Mjini Magharib wamepatiwa mafunzo ya maadili kwa viongozi.

## HABARI KIMATAIFA

## Wasiojulikana waua 15 Burkina Faso

**OUAGADOUGOU,** Burkina Faso

WATU 15 wameuawa ndani ya kipindi cha saa 24 nchini Burkina Faso katika kile serikali inachosema ni mapambano kati ya machifu wa kimila.

Taarifa ya jana iliyotolewa na Waziri wa Utawala, Simeon Sawadogo, ilisema kuwa kundi la watu wenye silaha kutoka vijiji vya mpakani mwa nchi hiyo na Ghana waliivamia nyumba ya chifu wa Zoaga, mapema jana na kuua watu wanane, eneo hilo lililoko umbali wa kilomita 250 Kusini Mashariki mwa mji mkuu, Ouagadougou.

Mbali na watu hao wanane kuuawa, wavamizi waliwajeruhi wengine wanne na kuiba mali pamoja na kulichoma moto soko kabla ya kukimbia. Kwenye uvamizi mwengine jana, watu saba waliuawa katika Jimbo la Sahel linalopakana na Mali.

Mwishoni mwa mwezi Januari mwaka huu, mapigano kati ya makundi hasimu yalisababisha watu watatu kuuawa, kwa mujibu wa meya wa zamani wa kijiji hicho. Mapigano kama haya yanatajwa kupunguza uwezo wa jeshi la nchi hiyo kupambana na wapiganaji wa siasa kali, ambao kwa miaka minne sasa wamelivamia eneo hilo la magharibi mwa Afrika. **DW**

## Kenya yakopa bilioni 48/- kila siku

**NAIROBI,** Kenya

KASI ya ukopaji wa serikali nchini Kenya, inaelezwa kuwa ni wastani wa shilingi bilioni 2.1 kwa siku.

Fedha hizo ambazo ni takribani Sh. bilioni 48.39 za Tanzania, hukopwa kila siku kwa mujibu wa gazeti moja lililoinukuu taarifa ya Benki Kuu ya Kenya (CBK).

Sambamba na hilo, inaelezwa wastani wa jumla ya deni la nchi kati ya Januari na Februari, sasa imefikia Sh. bilioni 126.4 na deni la taifa jumla yake imefikia Sh. trilioni 5.4.

Kwa mujibu wa taarifa hizo kutoka CBK, serikali imekuwa ikikopa fedha za ndani kupitia hati fungani za serikali, ambazo wawekezaji wamekuwa wakihamasika kuzinunua kwa wingi.

Pia, gazeti hilo linaeleza eneo lingine ambalo serikali inakopa ni katika mfumo wa kibenki nchini Kenya na taarifa ya mwaka mmoja katika kipindi kilichoishia Februari iliyopita, kiwango cha ukopaji katika sekta binafsi inatajwa imeongezeka kwa asilimia 3.4, huku kitaalamu kunaelezwa haijafikia wastani unaotakiwa wa kati ya asilimia 12 hadi 15, amabayo ni sahihi katika ukuzaji wa uchumi kitaifa.

Pia, mikopo ya benki za biashara katika mifumo wa kiserikali nchini Kenya ndani ya mwaka huo mmoja imeongezeka kwa wastani wa asilimia 13. **BBC**

# Kigogo Umoja wa Ulaya aikoromea Uingereza

**BRUSSELS,** Ubelgiji

KIONGOZI mkuu wa majadiliano wa Umoja wa Ulaya (EU), katika suala la Brexit Michel Barnier (pichani), ameonya kwamba kadri siku zinavyozidi kusogea mbele Uingereza inazidi kujiweka katika hatari ya kuondoka Umoja wa Ulaya bila makubaliano

Barnier aliyasema hayo mjini Brussels, siku moja baada ya wabunge wa Uingereza kushindwa kuungana ili kupitisha mpango wa kujitoa uliofikiwa na Waziri Mkuu Theresa May mwaka uliopita.

Mjumbe huyo wa majadiliano wa Umoja wa Ulaya alisema, umoja huo hauna nia ya kutengana na Uingereza bila makubaliano maalumu, lakini wako tayari kufanya hivyo kutokana na hali ilivyo hivi sasa. Barnier aliongeza kuwa ingawa mchakato wa Brexit umekuwa mgumu kutekelezeka, Umoja wa Ulaya uko imara.

Akizungumzia mchakato huo Barnier alisema, Bunge la Uingereza limekuwa likikataa kujitoa kwenye Umoja wa Ulaya bila makubaliano. Hata hivyo alisema njia pekee ya kuepukana na kujitoa bila makubaliano ni kupitia fikra chanya za walio wengi.

**Kwa sasa Uingereza inatakiwa iwe imeondoka kwenye Umoja wa Ulaya ifikapo Aprili 12 (Ijumaa ijayo), lakini hadi sasa, wabunge wameyakataa makubaliano kati ya Waziri Mkuu May na Umoja wa Ulaya mara ya tatu mfululizo.**

Barnier alieleza kuwa mjadala wa mpango wa kujitoa unapaswa kuendelea kufanywa kuwa mjadala wa wazi kwa watu. Kwa mujibu wa Barnier, kwa kuwa hapakuwa na mtizamo chanya wa walio wengi juu Uingereza kujiondoa kabla ya Machi 29, kifungu cha 50 kimeongezwa muda hadi Ijumaa Aprili 12, 2019.



Akitoa ushauri iwapo Waziri Mkuu May atakwama tena, na atashindwa kupitisha mpango wake kwa Bunge, basi Uingereza itasalia na njia mbili pekee, kuondoka bila makubaliano ama kuomba upya kuongezewa muda kupitia kifungu cha 50 na kwamba hatua hiyo itapaswa kufanyika kabla ya Uingereza kujiondoa Umoja wa Ulaya kabla ya ama ifikapo Aprili 12.

Bunge la Uingereza limekuwa likikataa mara kadhaa mipango mbadala ya ule wa Waziri Mkuu Theresa May wa kujiondoa EU likiwa limekwisha piga kura mara tatu bila matokeo yenye mafanikio, mpango huo kugonga mwamba kwenye baraza la wawakilishi umeiweka serikali katika wakati mgumu.

Hata hivyo May, ambaye anajulikana kwa nia yake thabiti huenda akajaribu kurudisha tena mpango wake wa makubaliano ya kujitoa Umoja wa Ulaya kwa mara nyingine baadaye wiki hii. Kujitoa kwa Uingereza katika EU bila makubaliano, kutaathiri biashara na safari katika vituo vya ukaguzi na maeneo ya mipaka pamoja na kanuni mpya kati ya Uingereza na nchi 27 za Umoja wa Ulaya.

Kwa sasa Uingereza inatakiwa iwe imeondoka kwenye Umoja wa Ulaya ifikapo Aprili 12 (Ijumaa ijayo), lakini hadi sasa, wabunge wameyakataa makubaliano kati ya Waziri Mkuu May na Umoja wa Ulaya mara ya tatu mfululizo.

Hoja za kufanyika kura nyingine ya maoni na mipango miwili ya kuibakisha Uingereza kwenye muungano wa forodha wa Umoja wa Ulaya zilishindwa hapo jana bungeni. **DW**



Baadhi ya waathiriki wa mafuriko nchini Msumbiji wakipokea chakula na huduma za msaada. **PICHA; MTANDAO**

# Kipindupindu chaibuka Msumbiji

**BEIRA,** Msumbiji

SIKU chache baada kimbunga kuathiri na kuua watu nchini Msumbiji, taifa hili limepata pigo jingine kufuatia mlipuko wa kipindupindu kuripotiwa nchini humo.

Ugonjwa huo umeua mmoja na wengine 517 wameambukizwa.

Mkurugenzi wa Idara ya Afya ya Taifa, Ussen Isse, amenukuliwa kwenye Televisheni ya Taifa (TVM), kwamba kuna vituo vya afya vya dharura vilivyoundwa kudhibiti mlipuko huo mjini hapa.

Inaelezwa kasi ya mlipuko iko juu, kutoka wagonjwa watano wiki iliyopita na ongezeko sasa limezidi asilimia 100.

Kimbunga kilichopita, kiliripotiwa kuharibu vibaya mfumo wa maji wa mjini Beira, tangu kwa mara ya kwanza, tarehe 14, mwezi uliopita.

Hadi sasa inaelezwa kunatarajiwa kufanyika chanjo kwa watu 900,000, kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Afya Duniani (WHO). **BBC**

# Sekondari Dar yapania kuondoa daraja la 3

**Na Yasmine Protace**

UONGOZI wa Shule ya Sekondari Wazo Hill ya jijini Dar es Salaam, imejiwekea mkakati wa kuondoa daraja la tatu katika matokeo ya mitihani ya kidato cha nne na cha sita mwaka huu.

Mkurugenzi Mtendaji wa shule hiyo, Venance Msaki, alieleza katika mahafari ya pili ya kidato cha sita shuleni hapo.

Alisema hayo baada ya shule yao kufanya vizuri katika mitihani ya kidato cha nne na sita mwaka jana, na kufanikiwa kushika kiwilaya nafasi ya pili na kimkoa nafasi ya 29.

"Katika matokeo ya kidato cha nne mwaka jana kulikuwa na daraja la kwanza hadi la tatu katika ufaulu, katika kidato cha sita ufaulu ulikuwa wa daraja la kwanza hadi la pili," alisema.

Aliongeza kuwa ufaulu huo umetokana na ushirikiano uliopo baina ya wazazi, walimu, wanafunzi na uongozi wa shule.

Alisema kama ushirikiano haupo vizuri hata matokeo hayawezi kuwa mazuri.

Alisema palipo na mafanikio hapakosi changamoto na kudai kuwa maji yamekuwa yakikatika mara kwa mara na kusababisha shule kuingia gharama za kununua maji. Aliongeza kuwa hata suala la umeme kukatika ni changamoto na shule huingia gharama kubwa kununua mafuta.

Alitaja changamoto nyingine kuwa ni dawa na vifaa vya maabara kuuziwa bila kupunguziwa bei na akaiomba serikali iwasaidie kuziondoa changamoto hizo.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kitengo cha Saikolojia, Dk. Eduid Shuki, aliyemwakilisha Katibu Mkuu Wizara ya Maji Profesa Kitila Mkumbo, alisema kuwa wazazi ni viongozi muhimu katika maendeleo ya mtoto.

Aliahidi kulifanyia utatuzi suala la maji ili wanafunzi waendelee kupata huduma hiyo kwa uhakika na salama.



Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Elimu na Mafunzo ya Lishe kutoka Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC), Sikitu Simon, akiongea na watoa huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya wa mikoa ya Dodoma na Singida wakati wa mafunzo ya virutubishi mchanganyiko yanayoendeshwa na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) kwa kushirikiana na TFNC jijini Dodoma. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Polisi yakemea madereva bodaboda wasio na weledi

**Na Anthony Gervas,** TARIME

JESHI la Polisi Mkoa wa Polisi Tarime na Rorya limesema kuwa pamoja na serikali kuwa na nia njema ya kuruhusu biashara ya wasafirishaji wa pikipiki maarufu bodaboda, kumekuwapo na changamoto kubwa za usalama barabarani kwa madereva wake.

Kamanda wa Polisi mkoani humo, SACP Henry Mwaibambe, alizitaja changamoto hizo kuwa ni pamoja na ukosefu wa weledi na wengi wao kutovaa kofia ngumu wakati wanapokuwa wakitoa huduma kwa vyombo hivyo.

"Zipo changamoto nyingi zinazosababishwa na madereva waendesha pikipiki hao, kwanza kutovaa kofia ngumu, kutopata elimu ya udereva na leseni za udereva, kubeba abiria zaidi ya mmoja "mishikaki" pamoja na kutokuwa na weledi," Mwaibambe alisema.

Alisema waendesha pikipiki hao wamekuwa ni chanzo kikubwa katika suala la usalama barabarani ambao wanasababisha kuwapo na matumizi holela ya barabara na kuongezeka kwa ajali za barabarani.

TUNAKUFIKIA POPOTE ULIPO TANZANIA
TANGAZA NASI SASA!!




Wawakilishi wetu wa mikoani

Iringa: Siangicha Ngowi- 0658269470
Tanga: Elisha Eliya Eliya 0719923993
Arusha: Hevens Mrema – 0754481773
Zanzibar: Marry Kizuguto- 0714262437
Dodoma, Singida: Sultan Ally -0714889096 & Raymond Mushi:0784 604262
Kilimanjaro, Manyara: Kelvin Lymo- 0715840855
Mwanza, Geita, Simiyu, Kagera, Mara, Kigoma: Abel Manase 0715214119 & Imani Isaya 0652 751 391
Morogoro: Baragash Hassan -0659324138
Ruvuma, Lindi, Mtwara : Gideoni Mwakanosya-0754928752
Rukwa, Mbeya, Njombe: Gibson Mwakatwila 0767318070
Tabora: Halima Ikunzi- 0743868485
Shinyanga: Shaaban Njia 0757209852
Pwani: Mwombeki Mbekomize 0756756122
Dar Es Salaam: Moses Masunga 0755 642851

The Guardian
Nipashe

For More Information Please contact:
Simu: +255 767 223 311, Barua pepe: advertise@guardian.co.tz
Mikocheni Light Industrial Area
SLP 31042 Dar es Salaam

# Korti yatupa maombi wanachama

INATOKA UK.3

ishna wa viapo," alisema Jaji.

Alisema kwa mujibu wa sheria hiyo ni lazima kiapo kionyeshe tarehe na mahali gani muapaji ameapa.

Maombi hayo namba 65/2019 yalifunguliwa mahakamani hapo na wanachama hao akiwamo Tungaraza Frida Msuva, Imelda Tarimo, Jackson Nyella, Thadeo Mgoso na Philemon Mwaluko ambao juzi walikamatwa kwa mahojiano na baadaye waliachiwa na Jeshi la Polisi.

Wengine ni Joseph Kessy, Samwel Tarimo, Nobel John, Aden Kimambo, Jacline Chacha, Vincent Chacha, Christina Mkundi, John Kulwa, Joseph Mnangu, Oliver Ndanshau, Omary Kimossa na Energy Petroleum (T) LTD.

Katika maombi yao ya msingi, walalamikaji waliwasilisha maombi hayo wakitaka walipwe Sh. bilioni 2.4 ikiwa ni sehemu ya fedha zilizotokana na mchezo wa upatu wakati DPP anaomba zitaifishwe na kuwa mali ya serikali.

Mapema mahakamani hapo, wakili wa walalamikaji, Charles Mutakyawa, aliomba kesi hiyo kuahirishwa kusikilizwa kwa kuwa ameshindwa kuwasilisha majibu ya nyongeza ya kiapo kinzani kutokana na kushughulikia baadhi ya wateja wake waliokamatwa jana (juzi) na polisi.

Hata hivyo, jaji alikataa ombi hilo, alimhoji kama hati ya kiapo aliyoiwasilisha mahakanani hapo imekidhi vigezo vya kisheria kutokana na kutokuwa na tarehe iliyoandaliwa.

"Wakili, je, unadhani maombi haya yamekamilika kisheria? Kabla hatujaendelea angalia kiapo ulichowasilisha mbele yangu," alisema Jaji Magoiga.

Wakili Mutakyawa alikagua kiapo na kubaini kwamba kina upungufu kwa kuwa hakuna tarehe na hakionyeshi mahali kilipoapwa.

DPP Biswalo Mganga aliunga mkono hoja kwamba kiapo kina upungufu na kuomba mahakama kutupilia mbali maombi hayo.

Wakati huohuo, jaji aliitisha maombi namba 42/2019 yaliyofunguliwa na DPP dhidi ya waliokuwa viongozi wa DECI Jackson Mtares, Dominick Kigendi, Timotheo Saiguran Ole Loitg'nye na Samwel Mtares.

Katika maombi hayo DPP Mganga akisaidiana na Wakili wa Serikali Mkuu, Mawakili wa Serikali Waandamizi, Shadrack Kimaro, Theophil Mutakyawa, anaiomba mahakama kutaifishwa mali mbalimbali pamoja na Sh. bilioni 14.1 kuwa mali ya serikali.

Aidha, Kimaro alidai wanaomba mali na fedha hizo zitaifishwe kwa kuwa zimetokana na uhalifu kwa kuendesha mchezo wa upatu kinyume cha sheria.

Alidai kwamba, kosa hilo ni moja ya makosa ambayo sheria inayachukulia kama moja ya makosa yenye nguvu (serious offence) na ndiyo maana Mahakama ya Rufani ilimwelekeza DPP kuwasilisha Mahakama Kuu maombi hayo.

Kimaro alidai, utaifishaji wa mali zinazotokana na uhalifu sio jambo geni nchini kwa hiyo wanaomba wahalifu wasinufaike na mali walizopata kutokana na uhalifu.

Kuhusu fedha Sh. bilioni 14.1 alidai, kuna ushahidi wa kutosha kwamba pia zilitokana na upatu kupitia michango waliyokuwa wakiitoa wanachama wa DECI na katika kiapo chao hawajaeleza chanzo kingine tofauti cha upatikanaji wa fedha hizo, hivyo haipaswi kuwanufaisha wajibu maombi.

Naye Kadushi aliiomba mahakama hiyo ikubali maombi yao kwa sababu ushahidi walioupeleka na vielelezo vyake umethibitisha maombi hayo yana mashiko kisheria.

Katika maombi ya msingi, DPP Mganga aliwasilisha mahakamani hapo, akiiomba itoe amri ya kutaifishwa kwa mali za kampuni hiyo yakiwamo magari 11, nyumba na viwanja vinane na fedha ziwe mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311



### KADI YA GARI IMEPOTEA

**HUSSEIN A.GULAM HUSSEIN** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T.822 BFU AINA YA TOYOTA HIACE CHASSIS NAMBA LH1231008236.

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.

TAARIFA POLISI:
**IYU/RB/560/2019**

### CHETI KIMEPOTEA



**BETHORD STEPHEN KILINDO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0183/0005** kilichotolewa na **LIGHANO SEMINARY** mwaka 2009.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **SO/RB/1237/2018.**

### HATI YA KIAPO

**Mimi HASSAN SALIMU** wa Tanganyika Muheza, nikiwa na akili zangu timamu naapa nakuthibitisha haya yafuatayo.

(1) Mimi ndiye Mmiliki wa nyumba Kiwanja No. 14 Kitalu 6 eneo la barabara ya 3 hapa Tanga Mjini.
(2) Kwamba kwa bahati mbaya hati ya kumiliki kiwanja hicho imepotea na juhudi za kuitafuta zimefanyika lakini hadi sasa haijapatikana.
(3) Kwamba nia na madhumuni ya kiapo hiki nikuomba Ofisi ya Ardhi inipatie hati nyingine kwa jina hilo hilo.

Mimi HASSAN SALIMU nathibitisha kuwa maelezo yote niliyotoa hapo juu ni kweli tupu na kwa kutia nguvu kiapo hiki nimefika Mahakamani na kutia sahihi yangu kuwa ni kweli.

**MBELE YA A. YUSUPH**
**CHEO HAKIMU**

### CHETI KIMEPOTEA



**ATHUMANI A. MCHOLI** anatangaza kupotelewa na cheti cha KIDATO CHA NNE chenye **No S0140-0008** kilichotolewa na NECTA TANZANIA mwaka 2007. Cheti cha DIPLOMA YA WANDISI MITAMBO **NO.1005017783** Kilichotolewa na DIT.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi:D**OM/RB/117/2019.**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Remmy Mwarika** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Suzuki EScudo yenye namba za usajili T964 AUL. Chassis namba TD1W225719. Engine **NO.G16A409715.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DOM/TR/RB/717/2018.**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JULIUS NGADI WEBBO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOYA VITZ yenye RANGI SILVER namba za usajili T758 BCM. Chassis namba 3CP100266640. Engine NO. 1SZ0647368.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DOM/TR/RB/29180330/4/2019.**


### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BARAGASH G. KHALID** ANATANGAZA KUPOLELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T. 813 AWM AINA LANDCRUISER RANGI YA LIGHT BROWN,CHASSIS NAMBA JTELB71J407022366.

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.

TAARIFA YA POLISI
**SMT/RB/4481/2019.**

### KUPOTEA KWA VYETI



**SIMON GEORGE METHUSELA** anatangaza kupotea kwa vyeti cha kidato cha nne chenye index namba S 1437-0082 na School Leaving Certificate, kilichotolewa na **FILBERT BAYI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2012,

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi .

Polisi Taarifa:
**STK/RB/2558/2019**

### CHETI KIMEPOTEA



**IRENE CHARLES MALACHA** anatangaza kupotelewa na BASIC CERTIFICATE yenye namba. BTCA/0298/T.2012 ,iliyotolewa na INSTITUTE OF ACCOUNTANTY ARUSHA mwaka 2013.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: CD/IR/763/2019**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHIFORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

Katika mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI
Usimamizi wa mirathi Ombi la MIRAJI YUSUFU SEFU kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu **ABDALLAH YUSUFU SEFU**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA.**
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 16/4/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia ya Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.
Tarehe 2/4/2019

..................................................
Sahihi ya hakimu

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo
MJINI MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;76/2019

Ombi la **ASHA RASHIDI MKWAMA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **SALUMU KONDO ZEVE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 04/04/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 14/03/2019

### CHETI KIMEPOTEA



**LAMECK KAKULU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S343/0096 kilichotolewa na Shule ya sekondari SIHA mwaka 1996.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi:

**CD/RB/2120/2019.**

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**MUHAMAD DILAWAR KHAN** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari **T NOAH** yenye namba za usajili **T 226** BWB . Chassis namba **SR 40-0081765.** Engine namba **3SFE7420243.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KJN/RB/1586/2019**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**KATIKA MAHAKAMA KUU YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**ARUSHA**
**SHAURI LA MIRATHI NAMBARI 04 LA MWAKA 2019**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRTHI YA VALDEZ ESSAU MOSHI...............MAREHEMU**
**NA**
**VICKY VALDEZ MOSHI...............MSIMAMIZI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(KANUNI YA 75).**

Watu wote wanadai kuwa na haki katika mirathi ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 13 mwezi wa Mei mwaka wa 2019.

Imewasilishwa Arusha leo terehe 14 Mwezi Februari mwaka 2019

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**KATIKA MAHAKAMA KUU YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**ARUSHA**
**SHAURI LA MIRATHI NAMBARI 10 LA MWAKA 2019**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRTHI YA MATILDA ALEX MADYANE.................................MAREHEMU**
**NA**
**ALEX STANISLAUS MADYANE ..........MSIMAMIZI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(KANUNI YA 75).**

Watu wote wanadai kuwa na haki katika mirathi ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua za usimamizi wa mirathi kwa mwombaji aliyetajwa hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 10 mwezi wa Juni mwaka wa 2019.
Imewasilishwa Arusha leo terehe 28 Mwezi wa Machi mwaka 2019


JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# CEREZO: GRIEZMANN HAONDOKI ATLETICO

**MADRID,** Hispania

RAIS wa Atletico Madrid, Enrique Cerezo amesisitiza kwamba Antoine Griezmann atabakia klabu hapo msimu huu wa kipindi cha majira ya joto, licha ya mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa kuhusishwa na mpango wa kwenda Barcelona.

Griezmann alikuwa kwenye nafasi nzuri ya kujiunga na Barcelona kabla ya Fainali zilizopita za Kombe la Dunia, lakini uhamisho huo ulishindikana dakika za mwisho.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 alibainisha wazi wazi kukataa kujiunga na Blaugrana hao na akaongeza mkataba wa kukaa hapo Atletico hadi mwaka 2023.

Lakini bado uvumi umeenea kwamba kuna uwezekano wa Barcelona kumsajili mchezaji huyo kwa siku za uzoni, na sasa Griezmann amebainisha wazi kuwa anaweza kutua kwa miamba hao wa Katalunya.

Hata hivyo, Cerezo amekanusha taarifa hizo akisema kwamba Mfaransa huyo hataondoka hapo Atletico kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

"Antoine hataondoka,"alisema akiliambia gazeti la Mundo Deportivo.

"Antoine ataendelea kukaa na Atletico, hilo ni kwa uhakika kabisa."

Kocha wa Atletico, Diego Simeone pia amesema kwamba Griezmann thamani yake inaweza kuwa euro milioni 120 kipindi cha majira ya joto kutokana na mkataba wake wa sasa.

"Kiukweli, sina hofu na suala la Griezmann," Simeone alisema akinukuliwa na Goal.com.

# *Ole Gunnar Solskjaer: Nimezungumza na Pogba*

**MANCHESTER,** England

KOCHA Ole Gunnar Solskjaer amebainisha kwamba amezungumza na nyota wa Manchester United, Paul Pogba kuhusu uvumi unaozungumzia majaliwa ya baadae ya mchezaji huyo.

Pogba alibainisha kwenye mechi za kimataifa kwamba angependa kujiunga na Real Madrid kwa siku za usoni huku kocha wa Los Blancos hao, Zinedine Zidane akisema kuwa angependa kumchukua kiungo huyo.

Hata hivyo, kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail, Solskjaer amesisitiza kwamba kabla ya mchezo wa jana Jumanne dhidi ya Wolves alizungumza na Pogba.

"Kwa sasa hakuna kinachonisumbua kuhusu yeye, nimeshazungumza na Paul. Hakuna kinachoweza kubadilika na kwa sababu anajua kwamba yeye ni muhimu zaidi kwetu."

Aliongeza: "Na ana furaha hapa, atakuwa sehemu yetu. Mara zote nimesema atakuwa sehemu ya timu yetu na hakuna kilichobadilika.

"Paul ni mchezaji mzuri na mtu mpole ambaye anajibu vizuri maswali. Zidane ni alama ya Ufaransa, na kocha mzuri ambaye mchezaji yoyote angependa kuwa naye, hivyo hata yeye kuonyesha kutamani kuwa chini yake ni sawa tu."





# De Gea azidi kuivuruga Utd

**MANCHESTER,** England

DAVID De Gea, mlinda mlango namba moja wa Manchester United kwa sasa amebakiza mkataba wa mwaka mmoja ndani ya kikosi hicho hivyo uamuzi ni wa mabosi wake kuamua kumpa mkataba mpya au kumruhusu aondoke klabuni hapo.

Mpaka sasa De Gea mwenye umri wa miaka 28 amekuwa katika mvutano mkubwa na mabosi zake hao akihitaji kulipwa fedha nyingi zaidi ya wachezaji wengine jambo ambalo limekuwa likileta mkanganyiko ndani ya klabu hiyo.

Imeelezwa kuwa klabu ya Paris Saint German (PSG) imeanza kumvutia kasi mlinda mlango huyo huku ikitenga kiasi cha Sh. bilioni 180 kunasa saini yake.

Pia mlinda mlango huyo amekuwa akiwaniwa na Real Madrid hali ambayo inaongeza ugumu na ushindani wa kuipata saini ya mlinda mlango.



## HABARI MICHEZO

# Man United hati hati kumpoteza Herrera

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United huenda ikapata pigo kwa kumpoteza kiungo wake muhimu katika kikosi chao, Ander Herrera.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail, nyota huyo anaweza akaihama United, kwani tayari yeye mwenyewe ameonyesha nia ya kutaka kujiunga na miamba wa Ligi Kuu Ufaransa, Paris Saint Germain.

Mkataba wa Ander Herrera na United unamalizika Juni mwaka huu, licha ya klabu hiyo kuwa na matumaini ya kumbakiza kikosini.

Herrera hadi sasa bado hajakubali kusaini mkataba mpya utakaoendelea kumweka klabuni hapo kwa kuwa bado hawajafikia makubaliano.

Taarifa zaidi zinasema kwamba, Herrera analipwa mshahara wa pauni 80,000 kwa wiki hapo United hivyo anashinikiza mkataba mpya aongezewe hadi 150,000.

Huku vyanzo mbalimbali baadhi yao vikiripoti kuwa nyota huyo anataka kulipwa pauni 200,000 kwa wiki.

Herrera mwenye umri wa miaka 29 amekuwa na uhakika wa namba tangu kuwasili kwa Ole Gunnar Solskjaer kuonekana kumwamini zaidi toka amepewa Man United, hivyo wengi hawaamini kama itamuachia kirahisi aende kucheza kule League 1.




# PAPA AWAONYA MASHABIKI WA MESSI




**MADRID,** Hispania

KIONGOZI Mkuu wa Kanisa Katoliki duniani, Papa Francis, amewaonya mashabiki wa mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi kwa kuwataka waache kumfananisha mchezaji huyo na Mungu.

Mashabiki wa Messi hasa wale wa Klabu ya Barcelona wamekuwa wakimtaja mchezaji huyo kama 'Mungu' wao kwenye soka na katika kuibeba timu hiyo kwenye nyakati ngumu.

Papa Francis akihojiwa kwenye kituo kimoja cha televisheni cha nchini Hispania wakati alipoulizwa na mtangazaji wa kituo hicho, Jordi Evole kwenye kipindi cha 'Salvados' kuwa, 'kuna baadhi ya watu wanamuita Lionel Messi 'Mungu' wa mpira duniani, je, wewe unaweza kumuita 'Mungu'.

Papa Francis alijibu, 'Kumfananisha Mungu na Messi sio sawa kabisa, nadhani mashabiki wanatakiwa kujua namna ya kutumia vizuri jina la Mungu," alisema Papa Francis.

"Watu wengi wanamtaja Mungu kama wanavyotamka 'Nakupenda sana', jambo hilo limesababisha hadi waone jambo la kawaida kusema 'Messi ni Mungu wa mpira', lakini huo ni utovu wa nidhamu na haikubaliki," amesema Papa.

Lionel Messi na Papa Francis wote ni raia wa nchi moja ya Argentina na kipindi cha nyuma Papa Francis aliwahi kumpongeza Messi kwa kuwashawishi vijana wengi kupenda mpira wa miguu.

# *Chelsea, Malmo zapigwa faini*

**LONDON,** England

SHIRIKISHO la Vyama vya Soka Ulaya (Uefa), limetangaza kuipiga faini ya pauni 11,100 klabu ya Chelsea kufuatia tukio lililotokea wakati wa mchezo wa Kombe la Ligi ya Europa Februari mwaka huu.

Chelsea katika mchezo wake wa Europa ugenini dhidi ya Malmo, shabiki wao alifanya tukio la utovu wa nidhamu kwa kufanya fujo na hivyo kupigwa faini hiyo sawa na zaidi ya Shilingi milioni 33 za Tanzania.

Shabiki huyo wa Chelsea aliyesababisha faini hiyo aliingia uwanjani wakati wa mchezo, tukio hilo lilitokea katika mchezo wa hatua ya 32 dhidi ya Malmo ambapo Chelsea walishinda kwa magoli 2-1.

Klabu zote mbili, Chelsea na Malmo vimepigwa faini kwa mashabiki wao kutupa vitu uwanjani wakati wa mechi.

Malmo nao wamekutwa na adhabu ya kupigwa faini ya pauni 49,000 ambazo ni zaidi ya Shilingi milioni 148 kwa makosa ya mashabiki wao kurusha miale ya moto uwanjani wakati mchezo ukiendelea.



# DONDOO ZA S KA
## MAGAZETI Y A




# VARANE AJIANDAA KUONDOKA MADRID

## ●●● Juventus, United njia nyeupe kumwania beki huyo aliye katika ubora wa juu...

**MADRID,** Hispania

NYOTA Raphael Varane ambaye ameitumikia Real Madrid kwa muda wa miaka nane anajiandaa kuondoka kwa vigogo hao La Liga, amesema wakala wa soka Ufaransa, Bruno Satin.

**Wakala huyo amesema kuwa amefanya mazungumzo na Anthony Varane, ambaye ni kaka wa Raphael na kueleza kwamba beki huyo wa kati Mfaransa ambaye alishinda taji la Kombe la Dunia mwaka jana anahitaji kupata changamoto mpya.**

Varane ambaye kwa sasa ni beki wa kati bora duniani amezivutia klabu mbalimbali za Ulaya, ikiwamo Manchester United, anatakiwa katika kipindi cha majira ya joto.

Akizungumza na kituo kimoja cha televisheni cha Ufaransa cha soka: "Nimetoka kuzungumza na Anthony na kujadiliana mambo mbalimbali lakini kubwa ni kuhusu soko la mchezaji huyo, kwa hiyo tumezungumza.

"Nafikiri kwa kipindi hiki kuhusu uchezaji wake anahitaji kubadilika, sifikirii kama atakuwa na uamuzi wa mwisho wa kuondoka Real Madrid, lakini amekuwa akifikiria kuhusu hilo kwa sababu ameshashinda mataji yote akiwa na Real."

"Kwa sababu anaona ameshapata kila ambacho alifikiria atakipata akiwa hapo, na sasa anaweza akaenda kwingine. Mahali kwingine kutoka hapa, binafsi sijazungumza moja kwa moja na Raphael."

Tangu mwaka 2011 alipojiunga na klabu hiyo, beki huyo wa kati ameshinda mataji 16 akiwa Bernabeu, yakiwamo manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na mawili ya La Liga.

Varane ambaye ana umri wa miaka 25 alikuwa mchezaji muhimu katika kikosi cha Ufaransa ambacho kilifanikiwa kutwaa taji la dunia katika fainali zilizopita ambazo zilifanyika Urusi katika kipindi cha majira ya joto.

Kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, ameshaweka wazi kwamba anajiandaa kutumia kiasi kikubwa cha fedha katika kipindi cha majira ya joto kwa ajili ya kukamilisha malengo ya kuimarisha safu yake ya ulinzi.

Timu nyingine ambayo Varane anaweza kutua ikiwamo Juventus, klabu ambayo ataungana na mchezaji mwenzake wa zamani wa Real, Cristiano Ronaldo.

Varane anatajwa kutaja kiasi kikubwa cha fedha katika kukamilisha uhamisho wake kokote atakapokwenda, akiwa ni mchezaji muhimu wa kikosi cha kwanza wa Madrid na mkataba wake na klabu hiyo utamalizika mwaka 2022.

## ZISIKUPITE

### HERRERA AMFUATA ZIDANE

KIUNGO wa Manchester United Mhispania, Ander Herrera (29) amesaini mkataba wa awali na Paris St-Germain, huku akisubiri kujiunga na klabu hiyo akiwa mchezaji huru katika majira ya joto. ***(Daily Record)***

### UNITED YAMGOMEA HERRERA

MABOSI wa Manchester United wamegoma kumpa mshahara mkubwa kiungo, Herrera kama alivyopendekeza, licha ya kuwapo kwa tetesi za Mhispania huyo kutaka kuondoka akiwa mchezaji huru. ***(Telegraph)***

### KEANE ANUKIA SPURS

TOTTENHAM inajipanga kuweka rekodi kwa kumsajili beki wa Timu ya Taifa ya England na Everton, Michael Keane (26), kwa dau nono la pauni milioni 50. Beki huyo pia anawindwa na Arsenal.***(Express)***

### COSTA AGOMBEWA ULAYA

KLABU ya Tottenham imeingia katika vita ya kuwania saini ya mshambuliaji wa Juventus, Douglas Costa (28) katika kipindi cha majira ya joto. Mbrazili huyo pia anatakiwa na Manchester United na Manchester City, wakati Chelsea na Paris St-Germain nazo zilionyesha kuvutiwa na nyota huyo. ***(Tuttosport, via Metro)***

### FRASER ANUKIA ARSENAL

ARSENAL imeweka wazi nia yake ya kumhitaji winga wa Bournemouth, Ryan Fraser ambaye ana umri wa miaka 25, katika kipindi cha majira ya joto. ***(Mirror)***

### MARTINELLI SOKONI

MABOSI wa Arsenal wako katika hatua za mwisho za mazungumzo na klabu ya Ituano ya Brazil kwa ajili ya kumwania winga, Gabriel Martinelli (17) kwa dau la pauni milioni 6.5. Chipukizi huyo ambaye aliwahi kufanya majaribio Manchester United, anawindwa na klabu zaidi ya 20 za Ulaya. ***(Sun)***

### UNITED YAZIDI KUJIPANGA

MANCHESTER United inakaribia kukamilisha mazungumzo ya kuajiri Mkurugenzi wa Ufundi wa kwanza, huo ni mwanzo wa mchakati wa Kocha Mkuu, Ole Gunnar Solskjaer kukamilisha benchi lake la ufundi. ***(London Evening Standard)***

### TOURE AFUNGUKA

KIUNGO wa zamani wa Manchester City, Yaya Toure (35), amewatupia lawama viongozi mbalimbali wa vyama vya soka duniani kwa kushindwa kuwalinda wachezaji weusi kutokana na changamoto ya ubaguzi. ***(Mirror)***

### AGUERO APUMZISHWA LEO

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola anajiandaa kumpumzisha straika wake, Sergio Aguero katika mechi ya Ligi Kuu England dhidi ya Cardiff utakaochezwa leo na kuongeza kuwa nyota huyo raia wa Argentina atakuwa fiti kuwavaa Tottenham katika mchezo wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya utakaopigwa Aprili 9 mwaka huu. (***Telegraph)***

### ZUBIZARRETA KUTUA ARSENAL

ARSENAL imemtaja Mkurugenzi wa Michezo wa Marseille na golikipa wa zamani wa Barcelona, Andoni Zubizarreta (57) kuwa ndiye mtu sahihi anayefaa katika nafasi hiyo kutua. ***(L'Equipe)***

## HABARI MICHEZO

# Baseball waenda Kenya wakijiamini

**Na Renatha Msungu**

KIKOSI cha wachezaji 14 wa Timu ya Taifa ya WS Baseball inatarajia kuondoka nchini leo kuelekea Nairobi, Kenya ili kushiriki mashindano ya kimataifa kwa ajili ya kutafuta nafasi ya kufuzu Michezo ya Olimpiki.

Akizungumza wakati wa hafla ya kuwakabidhi bendera, Katibu wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Alex Nkeyenge, alisema timu hiyo inakwenda kupambana kuhakikisha inapata nafasi ya kushiriki michezo hiyo ya Olimpiki itakayofanyika mwakani huko Tokyo, China.

Nkeyenge alisema kuwa anaamini wachezaji watafanya vema na kutimiza malengo ya kuona Tanzania inapata wachezaji wengine watakaoshiriki michezo hiyo ya kimataifa hapo mwakani.

"Tunaamini hii timu ina kila sababu ya kupata ushindi kwa sababu wamefanya mazoezi ya kutosha, wamejiandaa kwenda kushindana, hakuna kuleta visingizio," alisema Nkeyenge.

Aliwaambia kuwa michezo ni ajira na watakapopeperusha vema bendera ya Tanzania, watajiweka katika nafasi ya kupata mikataba ya kibiashara kutoka kwa kampuni mbalimbali.

"Mnaona Taifa Stars ilivyotutoa kimasomaso, nanyi igeni mfano wao," Nkeyenge alisema.

Kiongozi huyo aliwataka viongozi wa Chama cha Baseball kusaka vipaji vya wachezaji chipukizi ili kuuendeleza mchezo huo.

### MSIMAMO LIGI KUU BARA



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yanga | 28 | 21 | 4 | 3 | 45 | 19 | 67 |
| 2. Azam | 28 | 17 | 8 | 3 | 46 | 18 | 59 |
| 3. Simba | 22 | 18 | 3 | 1 | 48 | 7 | 57 |
| 4. Lipuli | 31 | 11 | 11 | 9 | 26 | 26 | 44 |
| 5. Kinondoni MC | 29 | 9 | 14 | 6 | 32 | 20 | 41 |
| 6. Mtibwa Sugar | 29 | 12 | 5 | 12 | 30 | 23 | 41 |
| 7. TZ Prisons | 30 | 9 | 11 | 10 | 24 | 25 | 38 |
| 8. Coastal Union | 30 | 8 | 14 | 8 | 27 | 30 | 38 |
| 9. Mbeya City | 29 | 10 | 7 | 12 | 30 | 32 | 37 |
| 10. Alliance | 30 | 9 | 10 | 11 | 23 | 30 | 37 |
| 11. Mwadui | 31 | 10 | 6 | 15 | 35 | 39 | 36 |
| 12. Kagera Sugar | 29 | 8 | 12 | 9 | 23 | 27 | 36 |
| 13.JKT Tanzania | 31 | 8 | 12 | 11 | 18 | 26 | 36 |
| 14. Mbao | 31 | 9 | 9 | 13 | 19 | 32 | 36 |
| 15. Stand Utd | 31 | 10 | 6 | 15 | 29 | 40 | 36 |
| 16. Ruvu Shooting | 31 | 8 | 11 | 12 | 27 | 37 | 35 |
| 17. Singida Utd | 30 | 8 | 9 | 13 | 20 | 31 | 33 |
| 18. Ndanda | 28 | 8 | 9 | 11 | 17 | 29 | 33 |
| 19. Biashara Utd | 29 | 7 | 9 | 13 | 21 | 29 | 30 |
| 20. African Lyon | 31 | 4 | 10 | 17 | 19 | 39 | 22 |

# KINDOKI AFUNGUKA KUHUSU UBINGWA WA KOMBE LA FA



**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kuisaidia timu yake kutinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA, golikipa wa Yanga, Klaus Kindoki, amesema hawapo tayari kuliacha kombe la michuano hiyo ambayo inatoa mwakilishi wa Tanzania Bara kushiriki mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika hapo mwakani.

**Kindoki alisema kuwa wachezaji wa Yanga wamejiandaa kupata ushindi katika mechi mbili zilizosalia katika mashindano hayo.**

Kipa huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) alisema kuwa pia Yanga ambayo inaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, haiko tayari kupoteza taji hilo linaloshikiliwa na watani zao, Simba.


"Kwenye ligi tunapambana na tunashukuru tunaongoza ligi, lakini pia kwenye FA tunaenda vizuri na tumefika hatua ya nusu fainali, tunachotaka ni kuona wachezaji wetu wanahakikisha tunashinda Kombe la FA na pia tunaendelea kufanya vizuri kwenye Ligi Kuu," alisema Kindoki.

Alisema anafahamu mechi na Lipuli haitakuwa nyepesi lakini wamejipanga kuhakikisha wanashinda mchezo huo dhidi ya wenyeji wao, Lipuli FC na kusonga mbele katika michuano hiyo.

"Lipuli walitufunga kwenye mchezo wa Ligi Kuu, lakini hiyo sio sababu ya sisi kushindwa kupata ushindi katika mchezo unaokuja dhidi yao, hatuwezi kukubali kufungwa tena na wao)," alisema.

Lipuli FC itawakaribisha Yanga katika mchezo wa hatua ya nusu fainali ya Kombe la FA kwenye Uwanja wa Samora Mjini Iringa, baadaye mwezi huu.

Vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara wametinga hatua hiyo baada ya kuwafunga Alliance FC ya Mwanza jijini Mwanza penalti 4-3.




Meneja Masoko wa Kampuni ya Michezo ya Kubahatisha ya SportPesa, John Mwakangale (kushoto), akimkabidhi hundi ya shilingi milioni 29.5 mshindi wa bonasi ya Jackpot, Joseph Hugo. **PICHA: SPORTPESA**

# *Mjasiriamali ashinda 'Jackpot Bonus'*

**Na Mwandishi Wetu**

MJASIRIAMALI, Joseph Elipidy Hugo wa jijini Arusha, ameibuka mshindi wa kitita cha shilingi milioni 29.5 cha Bonus ya Jackpot ya SportPesa ya wikiendi iliyopita.

Hugo ambaye ni mkazi wa Ngarenaro amebashiri kwa ufasaha mechi 11 kati ya 13 za Jackpot ya wiki iliyopita ambayo iliyokuwa na thamani ya Shilingi milioni 570.3.

Hugo alianza kucheza na SportPesa mwaka mmoja na nusu uliopita, huku akivutiwa zaidi na kiasi kikubwa cha Jackpot kinachotolewa wiki hadi wiki.

"Mimi ni mjasiriamali mdogo mdogo ninayejishughulisha na biashara za uwakala na uuzaji wa vifaa vya simu, nimeanza kucheza na SportPesa kwa mwaka mmoja na nusu sasa na kinachonivutia kucheza Jackpot ya SportPesa ni kiasi kikubwa cha shilingi milioni 585.2," alisema Hugo.

#### MALIPO PAPO HAPO

Licha ya kuvutiwa na kiasi hicho cha pesa cha Jackpot, Hugo anapenda kucheza na SportPesa kutokana na huduma bora za malipo papo hapo baada ya mechi kuisha.

"Utofauti wa SportPesa na kampuni nyingine ni malipo papo hapo, ambapo ukishinda tu hela inaingia muda huo huo. Huhitaji kwenda kwa wakala kutoa na unaipata popote ulipo bila usumbufu.

#### KUBORESHA BIASHARA

Mwisho wa siku, Hugo kama wajasiriamali wengine amepanga kukitumia kiasi hicho cha pesa kuboresha na kuiongezea ufanisi biashara yake.

"Ushindi huu utanipa mabadiliko kwenye biashara yangu kwa kuwa hela hii itaingia kwenye mzunguko wa biashara yangu, hivyo nathubutu kusema kuwa SportPesa imenibadilishia maisha yangu.

# Michezo

Jumatano Aprili 3, 2019

Nipashe




Varane ajiandaa kuondoka Madrid UKURASA 30



Straika Mfaransa wa Arsenal, Alexandre Lacazette (kushoto), akijiandaa kupiga shuti huku beki wa Newcastle, Jamaal Lascelles (katikati) akijaribu kumzuia katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa juzi usiku. Arsenal ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YAWAZA POINTI 3 BARA

## Ni katika mchezo dhidi ya JKT Tz wakati TP Mazembe wakitua nchini...

**Na Isaac Kijoti,** MOROGORO

WAKATI mabingwa wa zamani wa Afrika, TP Mazembe wakitarajiwa kutua nchini leo mchana, Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, amesema kuwa kikosi chake kiko tayari kuendelea na kasi ya ushindi katika mechi zake Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Simba inatarajia kuikaribisha JKT Tanzania katika mchezo wake wa 23 wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani hapa.**

Aussems aliliambia gazeti hili kuwa wachezaji wake wote wako kambini na walishiriki kikamilifu katika mazoezi ya jana, ili kujiandaa na mchezo huo muhimu.

Mbelgiji huyo alisema kuwa bado benchi lake la ufundi linaendelea kuwapa nafasi nyota wote waliosajiliwa kuitumikia timu yao na wanafahamu ushindani uliopo katika vita ya kuwania ubingwa wa ligi hiyo.

"Tuko tayari, kila mchezaji anajua tuko katika ushindani, kesho (leo) tunacheza mechi ya Ligi Kuu na Jumamosi tutakuwa katika mchezo mwingine wa kimataifa wa Ligi ya Mabingwa Afrika, hakuna mechi rahisi, tukimaliza mchezo huu, tunaanza kujipanga kwa ajili ya TP Mazembe," alisema Aussems.

Naye Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Abdallah Mohamed, alisema kuwa mechi zote za ligi hiyo ni ngumu na kwa upande wake hana hofu kwa sababu anaifahamu Simba.

"Tumeiangalia katika mechi zake za ligi na za kimataifa, wakifuata vema maelekezo na kila mmoja kutimiza jukumu lake, ninaamini tutapata matokeo mazuri," alisema kocha huyo mpya.

**MAZEMBE WAWASILI**

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema jana kuwa TP Mazembe kutoka Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo itawasili nchini leo saa saba mchana kwa ajili ya mechi yao ya hatua ya robo fainali itakayochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Manara alisema tiketi kwa ajili ya mchezo huo zimeshaanza kuuzwa, huku akieleza kuwa shabiki atakayenunua mapema atalipa Sh. 4,000 badala ya Sh. 5,000 kwa tiketi za eneo la mzunguko.

Aliitaja kauli mbiu ya mechi hiyo ni ile ile ya "YES WE CAN" ambayo waliitumia katika michezo yake iliyopita katika mashindano hayo yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF). Imeandaliwa na Somoe Ng'itu, Dar es Salaam.

# Uchaguzi Yanga kizungumkuti

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI Kamati ya Uchaguzi ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) likitangaza tarehe rasmi ya uchaguzi wa Yanga kuwa ni Mei 28 mwaka huu, baadhi ya wanachama wa klabu hiyo wameendelea kuupinga uchaguzi huo wakidai katiba inayotumika kuendesha mchakato huo ni batili.

Kamati ya Uchaguzi ya TFF ilitangaza kuwa katiba itakayotumika katika uchaguzi huo ni ya mwaka 2010 na wanachama watakaoshiriki ni wale ambao majina yao yapo kwenye leja ya klabu hiyo.

Akizungumza katika ofisi za gazeti hili jana kwa niaba ya wanachama wenzake, Juma Mwambelo alisema kuwa katika hiyo wanayotaka kuitumia haitambuliki kwa Msajili wa Vyama na Klabu za Michezo nchini.

Mwambelo ambaye pia alijitambulisha kuwa ni mmoja wa wadhamini wa Yanga alisema kuwa katiba halali ya klabu yao ni ya mwaka 1968 ambayo ilifanyiwa mabadiliko 2011.

"Kuna mchezo mchafu unachezwa ndani ya klabu yetu, huu uchaguzi unafanyika kwa katiba ya 2010, inatambulika wapi katiba hii? Katiba iliyopo kwa msajili ni ya mwaka 1968, uchaguzi huu ukifanyika ni batili," alisema Mwambelo akiungwa mkono na mwanachama mwingine, Geofrey Mwaipopo mwenye kadi ya Yanga namba 2481.

Aliongeza kuwa barua iliyotolewa Novemba Mosi mwaka jana na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) yenye kumbukumbu namba ADG/T.I/596/12 inaitambua katiba ya mwaka 1968 na si nyingineyo.

"Uchaguzi huu hautafanyika, tunajiandaa kwenda mahakamani kupinga kwa kigezo cha katiba inayotumika," alisema Mwambelo.

Pamoja na tishio hilo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya TFF, Ally Mchungahela, alisema kuwa uchaguzi huo wa Yanga utafanyikia kama ilivyopangwa kutokana na makubaliano yaliyofikiwa.

Mchungahela alisema kuwa viongozi waliokuwa wamesalia madarakani wameshatangaza kujiuzulu ili kupisha mchakato huo ambao sasa utahusisha nafasi zote na si uchaguzi mdogo kama ilivyokuwa awali.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042